Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

**Kikao cha Sita - Tarehe 9 Novemba, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*(Saa 3.02 asubuhi Bunge liliahirishwa kwa muda kutokana na vipaza sauti kutofanya kazi vizuri)*

*(Saa 3.40 asubuhi Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hali yetu ya umeme ndani ya ukumbi haijatengamaa sawa sawa, lakini *microphone* za hapa mbele zinafanya kazi vizuri. Nashauri kwa wenye maswali yao kwenye *Order Paper* wafanye kama Mawaziri wanavyofanya inapofika zamu yake ya kujibu swali anakuja kwenye *podium* anajibu swali anarudi kwake.

Sasa nashauri kwa Waheshimiwa Wabunge ambao maswali yao yako kwenye *order paper* wafanye hivyo hivyo waje watumie vyombo vya mbele. Akiona zamu yake inakaribia anakuja na napenda niliarifu Bunge kwamba vyombo vyote vilivyomo humu ndani ni vya Spika, hakuna cha Upinzani wala cha Serikali vyote ni vya Spika. Kwa hiyo, wauliza maswali watatumia chombo cha kushoto kwangu na Mawaziri watatumia chombo cha kulia kwangu kujibu maswali haya. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu Katika Nchi za *Tropical* kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2003 *(The Annual Report and Account of the Tropical Pesticides Research Institute for the year ended 30th June, 2003).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Korosho Tanzania kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Septemba, 2003 *(The Annual Report and Accounts of the Cashewnut Board of Tanzania for the year ended 30th September, 2003).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 75

**Rushwa Kama Kikwazo cha Maendeleo**

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, rushwa ni kikwazo kikubwa cha maendeleo hasa ikizingatiwa kuwa rushwa hiyo imeshamiri katika usiri uliokithiri na kutowawajibika katika utoaji wa maamuzi yanayogusa maslahi ya mtu, vikundi au umma kwenye medani ya Utawala, Uchumi na Utoaji wa huduma za Kijamii; na kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu imedhamiria kupambana na rushwa katika sura zake zote kwa kubaini na kuziba mianya ya rushwa kwa kuzingatia Utawala wa Sheria:-

(a) Kwa kuwa umma wa Watanzania wanaona kuwa moja ya sababu ya rushwa katika chaguzi mbalimbali ni takrima *(traditional hospitality)* kipengele ambacho mipaka yake haiko wazi; je, Serikali haioni kuwa upo umuhimu wa kuifanyia marekebisho sheria husika?

(b) Kwa kuwa, tuhuma za rushwa kubwa *(Grand Corruption)* zinaelekezwa kwa Taasisi za dola hususan Serikali na Mahakama; je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu baadhi ya maoni ya wadau kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuunda taasisi huru *(Independent Commission)* itakayoshughulikia masuala yote ya rushwa?

(c) Kwa kuwa kiwango cha fedha kinachotumika kinakuwa kikubwa kuliko vipato halali vya wagombea na kwa kuwa upo uwezekano mkubwa kwa baadhi ya wagombea na washirika wao kutumia fedha haramu zinazotokana na madawa ya kulevya, ujangili na ufisadi, je, Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y. WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na mjadala kuhusu dhana ya takrima katika uchaguzi. Baadhi ya Watanzania wanaona kwamba dhana hii imetoa

mwanya wa vitendo vya rushwa wakati wa chaguzi mbalimbali kwa kuwa ni vigumu kutenganisha malipo au vitu vinavyotolewa kwa nia njema na vile vinavyotolewa kwa nia mbaya. Kwa sababu sheria imefafanua vema juu ya takrima wakati wa uchaguzi na kuelekeza kwamba utata wowote utatatuliwa na Mahakama. Serikali inaheshimu msimamo huo wa Kisheria.

Mheshimiwa Spika, mjadala kuhusu takrima upo kwenye Tume ya Marekebisho ya Sheria ukifanyiwa utafiti ili kupata maoni zaidi kama sheria iliyopo iendelee au ibadilishwe. Kwa hiyo, kwa sasa hakuna uthibitisho kwamba umma wa Watanzania unaona sababu ya rushwa katika chaguzi ni takrima. Maoni zaidi na subira vyote vinahitajika.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli tuhuma za rushwa kubwa huwa kwa kiwango kikubwa zinawahusu watumishi wa umma wa ngazi za juu wa Serikali na Idara ya Mahakama kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Lakini pia uwahusu viongozi wa kisiasa na viongozi wa makampuni au mashirika binafsi. Kwa mantiki hiyo, ufanisi katika kuchunguza tuhuma za rushwa kubwa unategemea uwezo wa chombo kinachoshughulikia tatizo la rushwa kama Taasisi ya Kuzuia Rushwa *(PCB)* kutoingiliwa. Ndio sababu chombo hiki kimewekewa utaratibu kuhakikisha kwamba kinawajibika ipasavyo na kinaendesha shughuli zake kwa misingi ya sheria za nchi bila kuingiliwa yaani *operational independence.* Maoni yamepokelewa juu ya namna ya kuiboresha Taasisi ya Kuzuia Rushwa na Tume ya Kurekebisha Sheria inayafanyia utafiti maoni hayo ili hatimaye iweze kutoa mapendekezo.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa hadi sasa hakuna uthibitisho unaoonesha kwamba kiwango cha fedha kinachotumiwa na wagombea katika chaguzi ni kikubwa kuliko vipato vyao halali. Hata hivyo, ili kuhakikisha kwamba wagombea hawatumii fedha zinazotokana na dawa za kulevya, ujangili na ufisadi katika kugharamia shughuli za uchaguzi, kuna sheria mbalimbali dhidi ya biashara ya dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na kupatikana kwa mali iliyotokana na biashara hiyo au inayotokana na vitendo vya uvunjaji wa sheria. Hivyo, ikidhihirika kwamba mgombea ana mali iliyotokana na biashara ya dawa za kulevya, mgombea huyo anastahili kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Aidha, vyama vya siasa vina wajibu wa kuwasilisha kwa Msajili wa vyama vya siasa vyanzo vyao vya mapato. Serikali inategemea sana ushirikianao wa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla ili kuepusha hali aliyoieleza Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

(i) Kwa kuwa taasisi zinazohusishwa mara nyingi kwa kuongoza kwa rushwa ni Polisi na Mahakama, Taasisi ambazo kimsingi ndio Serikali yenyewe na kwa kuwa mishahara ya watumishi katika Taasisi hizo ni kidogo sana chini ya shilingi 100,000/=

*take home* kwa mwezi, je, kwa nini Serikali isianze kurekebisha mishahara ya watumishi hawa muhimu katika jamii yetu kama vile tulivyofanya *TRA?*

(ii) Kwa kuwa rushwa kubwa imeonekana zaidi inaanzia kwenye mikataba inayosainiwa na kwa kuwa kimsingi kwa miaka mingi nchi yetu imekuwa na uchumi ovyo, je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuhakikisha kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inapata wataalam waliobobea kabisa katika sheria za mikataba ya Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika maoni ya watu, katika redio, magazeti na katika mikutano ya hadhara. Taasisi alizozitaja, zinatajwa sana na wananchi kwamba zinajihusisha na rushwa ikiwemo Polisi na Mahakama. Sasa swali la Mheshimiwa Mbunge anasema watu hawa wakipewa mishahara mikubwa itakuwa ndio dawa ya tatizo la rushwa. Nataka kusema kwamba rushwa kwa msingi kabisa ni tabia ya mtu mwenyewe, tabia ya kutokudhibiti tamaa, tabia ya uchoyo na uroho. Sasa mtu mwenye tabia hiyo awe na mshahara mdogo, awe na mshahara mkubwa, bado tu ana mshahara mkubwa kwa sababu ya uchoyo na uroho atakwenda kuomba rushwa kwa mwananchi maskini kuliko utajiri wake.

Kwa hiyo, kwa kiwango kikubwa tunapambana hapa na tabia ya watu, hili la mshahara kwa kweli linashughulikiwa si tu kwa Mahakama na Polisi linashughulikiwa kwa watumishi wote wa umma. Kila siku Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma anatuambia kwamba Watanzania tukikazana, tukaboresha uchumi, uchumi ukiwa mpana mapato ya Serikali yataongezeka na mishahara vile vile itaongezeka.

Swali la pili kuhusu swala la mikataba, nashauri kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ifanya bidii kuwafundisha watumishi wake wawe na utaalam mkubwa sana ili ufanane na matatizo ya sasa, nafikiri ni ushauri mzuri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo hapa atauzingatia.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea jibu la ziada kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utawala bora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Naibu Waziri kwa kujibu swali hili vizuri kwamba rushwa ni suala la hulka zaidi kuliko mapato ya Serikali. Maadili ya Utumishi ya Umma yanakataza suala la rushwa na Sera ya Manejimenti na ajira ya Utumishi Umma inahusisha mishahara na tija na ufanisi sio tu katika uchumi wa nchi bali katika utendaji kazi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba kwa sasa hivi mishahara ya watumishi wa Umma ni asilimia zaidi ya 35 ya Bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, utaona kwamba Serikali inatenga mishahara kwa kadri ya uwezo wake na vile vile inabidi itendeshe kazi zingine kama za kujenga barabara, kujenga zahanati na

miundombinu mingine na kwa hiyo, kuongezeka kwa mishahara itategemea mapato ya Serikali ambayo yanatokana kwa kiasi kikubwa na tija ndani ya uchumi wetu. Lakini ni marufuku kwa watumishi wa Serikali kupokea hongo au rushwa kwa sababa ya mishahara na vile vile si kweli kwamba watumishi wengi wa Serikali wana nafasi za kupata rushwa. Ni wachache sana na hao wachache wasiachiwe kuharibu sifa na heshima ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Na. 76

**Ujenzi wa Miji Midogo na Vijiji**

**MHE. PHILIP S. MARMO (k.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza: -

(a) Je, ujenzi wa Miji Mikubwa na Miji Midogo nchini Tanzania unazingatia vigezo gani hasa ikitilia maanani kuwa Miji Midogo nchini sio Miji ya viwanda bali ni Miji ya kilimo na ufugaji na upimaji wa viwanja vya kujenga hauzingatii tofauti kati ya miji ya viwanda na miji midogo ambayo wananchi wake wanategemea kilimo na ufugaji?

(b) Je, ni lini upimaji wa viwanja vya kujenga Miji Midogo na Vijiji utazingatia hali halisi ya uchumi wa wakazi hao?

(c) Kwa kuzingatia utaratibu wa sasa, je, sio kweli kuwa ukubwa wa miji baadaye utatisha kwa ukubwa ikiwa ujenzi na matumizi ya maeneo hayazingatii ujenzi wa nyumba za ghorofa zaidi katika miji?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miji mikubwa na miji midogo nchini unazingatia vigezo vilivyoainishwa, miongozo, kanuni, sera na sheria kama ifuatavyo: -

(i) Sheria ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Na.4 na Na.5 ya mwaka 1999 ambayo inatoa mwongozo wa upangaji miji kwa Mamlaka za Miji na Wilaya.

(ii) Sera ya Maendeleo ya Makazi ambayo nayo imetoa kwa kina na kutoa ufafanuzi kuhusiana na eneo hili.

(iii) Vigezo vilivyoainishwa kwenye kada ya Mipango Miji *(Town Planning)* na Upimaji wa ardhi *(survey).*

(iv) Mazingira halisi ya eneo la mji au kijiji kwa kuzingatia kiwango cha ujenzi ambacho kimefanyika.

(v) Maelekezo yanayotolewa kwenye miongozo na nyaraka mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, miji mikubwa hutengewa eneo kubwa zaidi kwa ajili ya kukidhi ongezeko la watu na la kutosha kwa shughuli nyingi zaidi ukilinganisha na miji midogo. Maeneo haya ni kwa ajili ya miundombinu, viwanda, biashara, makazi, Ofisi za Serikali, maeneo ya kuabudu, huduma za jamii, maeneo ya wazi na bustani za umma. Aidha, ujenzi wa miji huzingatia pia eneo la utawala lililoidhinishwa na Mheshimiwa Rais kwa kushauriwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

(b) Mheshimiwa Spika, upimaji wa viwanja kwa kuzingatia hali ya uchumi wa wakazi umeanza kutekelezwa tangu mwaka 1999 kwa kuweka utaratibu wa mpangoshirikishi jamii katika matumizi ya ardhi yao uliobuniwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Chini ya mpango huu zimeundwa Kamati za ugawaji wa ardhi katika ngazi za Vitongoji, Mitaa, Vijiji na Kata. Majukumu ya Kamati hizi ni kuainisha eneo lao, kupanga matumizi ya ardhi na kugawa maeneo kufuatana na mahitaji, shughuli na mazingira ya eneo lao. Mpangoshirikishi wa ugawaji wa ardhi kwa taarifa tulizonazo umeonyesha matokeo mazuri.

(c) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa umezingatia ujenzi wa nyumba za ghorofa, kwa kutoa Hati za kumiliki Ardhi *(offer)* kwa kipindi cha miaka 33. Baada ya kipindi hicho, masharti ya Hati za kumiliki Ardhi hubadilika na kuelekeza ujenzi wa nyumba za ghorofa kutegemeana na hali halisi ya wakati husika. Mfano Miji mingi mikongwe hapa nchini Hati zake za umiliki wa ardhi zimefanyiwa mabadiliko ya masharti ya ujenzi kulingana na mazingira.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, mapema mwaka jana Wizara hii ilitangaza kwamba ilikidhi maendeleo ya miji, ilitangaza Makao Makuu yote ya Wilaya na miji mingine midogo kuwa Mamlaka kamili kusimamia ukuaji wa miji na maandishi yalitolewa ilipofika mwezi Julai, 2003 kwamba ifikapo mwezi Oktoba, 2003 Mamlaka hizi zingeanza kazi rasmi sasa imekuaje?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Philip Marmo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kauli ilitolewa hapa Bungeni na Serikali, lakini kama mtakumbuka tulifanya marekebisho ya kauli hiyo na kuamua kwamba Mamlaka za Miji hii midogo tumeona zianze mwaka kesho mwezi Januari kwa sababu tulihitaji maandalizi ya kutosha na kuzipa Halmashauri nafasi ya kuweza kujipanga vizuri. Kwa hiyo, tuna hakika itakapofika wakati huo sehemu nyingi kabisa zitakuwa zimeshatekeleza agizo hilo.

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea Waheshimiwa Wabunge, mwanzoni mwa kikao nilighafilika, kuna wageni wawili wa Kimataifa ambao nilipaswa kuwatambulisha na kuwakaribisha Bungeni na ningependa nifanye hivyo sasa.

Tunaye Mheshimiwa Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Mheshimiwa Wolfang Ringe na tunaye Balozi mdogo wa Ufaransa nchini Tanzania, Mheshimiwa Terence Wills. Tunawakaribisha waangalie shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Na. 77

**Kuziongezea Halmashauri Ruzuku**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA (k.n.y. MHE. RAPHAEL N. MLOLWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu imekuwa makini kuongezea ukusanyaji wa mapato na katika kupanga matumizi yake imekuwa ikitoa kipaumbele kwa masuala ya utawala bora na kwa kuwa maboresho yanayoendelea katika Serikali za Mitaa ni mchakato ambao hatma yake ni kuimarisha utawala bora.

Je, Serikali itakuwa tayari kuongeza ruzuku kwa Halmashauri nchini ili kuwezesha Mabaraza ya Madiwani kuwa na muda mrefu zaidi wa kujadili mapendekezo ya makadirio ya mapato yaliyowasilishwa kwao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria Na.9 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 Kifungu 10(1) na (2), Serikali hutoa ruzuku kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma muhimu katika sekta za Elimu, Afya, Maji, Barabara na Kilimo. Lengo la kutoa ruzuku katika maeneo haya ni kuimarisha ubora wa huduma zitolewazo kwa jamii na hivyo kuwawezesha wananchi kujishughulisha na shughuli za maendeleo zenye lengo la kupambana na umaskini.

Aidha, kwa mujibu wa takwimu zilizopo, Serikali imekuwa ikiongeza kiwango cha ruzuku inayotolewa kwa Halmashauri kadri mapato yake yanavyoongezeka kila mwaka katika matumizi ya kawaida na vile vile katika Bajeti ya maendeleo. Hata hivyo kufuatia mpango wa pili wa kuondoa umaskini kuanzia mwaka 2005/2006 maeneo yote sasa yatakuwa na haki ya kupatiwa ruzuku kulingana na vipaumbele vya sekta.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina nia ya kutoa ruzuku kwa Halmashauri ili kuyawezesha Mabaraza ya Halmashauri kuwa na muda mrefu zaidi wa kujadili mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi yaliyowasilishwa kwao. Msingi wa uamuzi huu, ni mpango mzima uliobuniwa hivi sasa wa ushirikishaji wananchi ambao huanzia katika ngazi ya kijiji hatimaye kwenda kwenye Kata na mwisho katika Baraza la Madiwani.

Utaratibu huu huwezesha wadau wote kuchambua kwa kina mapendekezo ya mipango ambayo yatagharamiwa na ruzuku ya Serikali Kuu pamoja na ile itakayogharamiwa na mapato ya Halmashauri yenyewe. Serikali wakati wote itakuwa tayari kuongeza ruzuku kwa Halmashauri kulingana na uwezo wake ili kulipia huduma muhimu kwa wananchi na wala si kulipia posho ya vikao vya Madiwani. Aidha, Halmashauri zimepewa maelekezo yanayoeleza ruzuku inayotolewa kutokana na kufutwa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato kamwe isitumike kugharamia vikao vya Madiwani.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Halmashauri nyingi zimekuwa zikilaumiwa kwa kutosimamia vizuri Bajeti zao na kwa kuwa hii inatokana na Baraza ya Madiwani kukosa muda wa kutosha wa kupitia na kuchambua Mapato na Matumizi ya Bajeti hizo kwa sababu wanakaa siku moja au mbili.

(i) Je, Serikali iko tayari kutenga angalau siku saba kwa Mabaraza ya Madiwani kuweza kuchambua Bajeti zao kwani hata Bunge huwa linakaa miezi miwili mizima kupitia Bajeti ya Serikali?

(ii) Je, Serikali imeshafikia wapi kuhusu ombi la Madiwani kuongezewa posho zao za madaraka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika maelezo ya msingi, suala la kuongeza posho au muda wa vikao kwenye Mabaraza ya Madiwani umewianishwa vizuri sana na mfumo mzima wa namna shughuli zinavyoendeshwa. Ni tofauti kabisa na Bunge lako linapokutana hapa kujadili mapendekezo ya Bajeti kwa sababu ninyi kama Serikali au Bunge kama sehemu ya Serikali ndio tunaopanga mipango yote kwa nchi nzima. Katika majadiliano hayo ipo *component* kubwa sana ya Bajeti ya Halmashauri ambayo nayo huwa inapitishwa kupitia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, *component* inayobaki inakuwa ni ile inayotokana na vyanzo vya mapato yake ambayo nimesema kwa mpangoshirikishi vinaanzia ngazi za Vitongoji, Vijiji na hatimaye Kata ambayo Madiwani ndio Wenyeviti na inakwenda katika *Full Council.* Kwa kweli katika hali ya kawaida wala hawahitaji muda mwingi na uzoefu niliouona mimi wengi siku za nyuma walikuwa wanatumia muda mrefu zaidi mpaka saa 4, saa 5 usiku hivi sasa wengi wanamaliza majukumu yao katika muda mfupi kabisa. Nadhani kutokana na mpangoshirikishi. Kwa hiyo, bado tunaamini jambo hili linaweza kabisa likaendelea kufanyika hivyo kwa kadri tunavyoliona hivi sasa, lakini kama hali itaibuka hapo baadaye Serikali haitasita kuchukua hatua zinazostahili.

Kuhusu posho za madaraka kwa Waheshimiwa Madiwani, jambo hili limekuwa likiulizwa mara nyingi na tulichofanya kama Serikali mwaka 2003 wakati tulivyokutana kwenye *ALART* Arusha, tuliagiza kupitia chombo chao cha *ALART* waunde Kamati, itazame si posho tu, lakini maeneo mengine yote yanayomgusa Diwani, kisha

tushirikiane nao kujaribu kutatua tatizo hili ambalo ni la muda mrefu na nafurahi kusema kuwa zoezi hilo linaendelea, ni matumaini yangu kwamba tutafika mahali tutafikia muafaka juu ya jambo hili.

**SPIKA:** Kwa kuwa muda mwingi ulipotea wa maswali kwa sababu ya tatizo la vipaza sauti, naomba tupunguze maswali ya nyongeza.

Na. 78

**Malipo ya Pensheni**

**MHE. ERNEST G. MABINA (k.n.y. MHE. KABUZI F. RWILOMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilishaahidi kuwalipa wastaafu waliochukua mafao yao kwa mkupuo na bado wako hai:-

(a) Je, ni wastaafu wangapi waliopo nchini hadi sasa?

(b) Je, ni wastaafu wangapi wa aina hiyo waliopo Geita na wametengewa kiasi gani cha fedha?

(c) Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi yake ya kuwalipa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wastaafu waliopo nchini ambao wanalipwa pensheni za miezi sita ni 35,739. Wastaafu ambao walilipwa mafao yao kwa mkupuo na sasa wamekwisha jitokeza kwa kutambuliwa kwa ajili ya kuwarejesha kwenye malipo ya pensheni ni 15,000. Hivyo, idadi ya wastaafu wote nchini mpaka sasa ni 50,739.

(b) Mheshimiwa Spika, wastaafu waliopo Geita ambao wanapokea Pensheni ya miezi sita ni 196. Kiasi cha fedha walichotengewa ni shilingi 79, 387,362.30 mwaka 2004/2005. Idadi ya wastaafu waliolipwa mafao yao kwa mkupuo waliopo Geita baada ya zoezi la kuwatambua ni 187.

(c) Mheshimiwa Spika, kutokana na zoezi la kuwatambua wastaafu waliochukua mkupuo kuchukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa, imebidi muda wa maandalizi na muda wa kuanza malipo kuongezwa na kusogezwa hadi Januari, 2005. Pensheni italipwa kwa muda wa miezi 12 kuanzia Julai, 2004 hadi Juni, 2005.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa uzee ni lala salama na unapofikia uzee huna nguvu tena ya kuweza kukidhi kupata mahitaji yoyote na wafanyakazi wengi wamefanya kazi kwa muda mrefu na kuweza kuitumikia Serikali hii. Lakini malipo yao yamekuwa madogo kiasi ambacho wakachukua uamuzi wa kuchukua mkupuo pesa zao, je, Serikali itafanya mpango gani wa kuweza kuwaongezea pesa nyingi zaidi ukilinganisha na hali ya maisha inavyokwenda?

(b) Kwa kuwa wastaafu wengi wanapata shida ya kusubiri kwa muda wa miezi sita kupata malipo yao, je, Serikali itaonaje kama itarudisha utaratibu wa kulipwa kwa muda wa miezi mitatu mitatu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kama tulivyokuwa tunasema mara nyingi kwamba kila tunapotengeneza Bajeti huwa tunafikiria namna ya kuongeza wastaafu, fedha za pensheni kulingana na hali yetu ya kifedha inavyoendelea kuwa bora na hivyo bado hatusiti kufanya hivyo kila siku zinavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyokubali na kukubaliana kwamba wale ambao wamepata kwa mkupuo warejeshwe, wawe wanapata mshahara, wawe wanapata pensheni sasa hivi. Kwa hiyo, utaratibu huo kila mwaka utakuwa unaendelea kuangalia namna tunavyoweza kuwasaidia kupata mapato zaidi. Kwa shida ya kusubiri nimejibu mara nyingi sana kuhusu suala hili ni kwamba hata ukisema ulipe kwa miezi mitatu lazima itupe muda wa kutengeneza hizo hesabu na kuhakikisha kwamba miezi sita iliyowekwa ndio inaweka utaratibu wa kuweza kuwalipa hawa na kuweza kuyakamilisha yale yote bila kuwa na matatizo yoyote. Bila hapo katika Bajeti yetu itakuwa inasumbua vile vile.

Na 79

**Umeme Katika Kijiji cha Mandawa, Kilwa**

**MHE. OMAR M. MWENDA** aliuliza:-

Kwa kuwa mawe ya kutengenezea saruji yanapatikana katika kijiji cha Mandawa, Kilwa na mawe hayo kwa sasa yanachukuliwa na kupelekwa katika kiwanda cha *Wazo Hill,* Dar es Salaam bila wananchi wa kijiji cha Mandawa kunufaika na chochote; na kwa kuwa wawekezaji wanashindwa kuwekeza katika kijiji hicho kutokana na ukosefu wa umeme:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa wakati umefika sasa wa kupeleka umeme kijijini Mandawa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni vema umeme wa gesi ya Songosongo utakaotoka Somanga hadi Kilwa Masoko ukafikishwa hadi kijiji cha Mandawa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kupeleka umeme katika kijiji cha Mandawa ili kuchochea kasi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika kijiji hicho. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali tayari imeiagiza *TANESCO* ifanye tathmini ya mahitaji ya umeme katika kijiji hicho kwa lengo la kuangalia njia mbali mbali za kupeleka umeme huko kwa gharama nafuu kutegemea mahitaji ya kijiji hicho.

(b) Kwa kuwa kuna njia kadhaa za kupeleka umeme kijiji cha Mandawa kama nilivyoeleza awali, inabidi kwanza tusubiri tathmini ifanyike ili kujua njia yenye gharama nafuu ya kupeleka umeme kijiji cha Mandawa.

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri naomba nimwulize swali moja dogo. Kwa kuwa aliyepewa eneo hili la kuchimba mawe yeye amepewa bila kushirikishwa wananchi na kumfanya awe kiburi ya kutolipa mrabaha, je, Serikali iko tayari kuwaruhusu wanakijiji wenyewe kuchimba mawe haya na kumuuzia mtu yeyote?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omar Mohamed Mwenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye sehemu anayoitaja Mheshimiwa Mbunge kuna kampuni tatu zinazofanya kazi ya uchimbaji wa *Gypsum* na kuiuzia Kampuni ya Wazo. Kampuni hizo ni *Kusini Africa Ltd, Mazongera Enterprises* na Michael Wanzara Mkama. Kampuni hizi zina leseni halali na wanalipa kodi kulingana na sheria ya madini nchini.

Nadhani pengine hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni kutaka kujua namna gani hawa pia wanaweza pia wakasaidia katika maeneo husika kwa maana kama ambavyo Kampuni nyingine za wachimba madini zinavyofanya ni hoja kama hiyo ambayo alishawahi kuifikisha Wizarani, nadhani ni hoja nzuri na sisi tutawashauri hawa wajenge pia uhusiano mzuri na wana kijiji husika wasaidie pale inapobidi katika kuendeleza kijiji hicho.

**SPIKA:** Tunaendelea maswali kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, hapo ulipo.

Na. 80

**Ujenzi wa Shule za Sekondari**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa Watanzania wengi wameamka sana kielimu na kuanza kujenga shule nyingi za sekondari na hata mahali pengi kuathiri maendeleo ya ubora wa elimu *(quality)* iliyokusudiwa:-

(a) Je, ni sekondari na *High School* ngapi za Serikali na za binafsi zilizopo katika kila Wilaya?

(b)Je, kitakwimu au hata kiasilimia ni wanafunzi wangapi waliokwisha hitimu kwa kila Mkoa na hata Wilaya?

(c) Je, ni Mikoa ipi yenye walimu wachache zaidi na walio wengi zaidi kwa wastani wa asilimia ya shule zilizopo ikilinganishwa na walimu wote waliopo?

**SPIKA:** Litajibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi Mei, 2004 zilikuwepo jumla ya shule za sekondari 828 za Serikali zikiwemo 744 za kidato cha kwanza hadi cha nne na 84 za kidato cha tano hadi cha sita. Aidha, zipo jumla ya shule za sekondari 463 zisizo za Serikali zikiwemo 336 za kidato cha kwanza hadi cha nne na 127 za kidato cha tano hadi cha sita. Idadi ya shule hizo kwa kila Wilaya zimeonyeshwa kwenye Jedwali Na. 1 ambalo Mheshimiwa Mbunge atapewa kwa sababu ya kuokoa wakati.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge katika swali lake hakutaja kipindi husika cha takwimu alizohitaji, imekuwa vigumu kulifanyia kazi swali hilo ipasavyo. Hata hivyo kwa ujumla katika mwaka 2003 kulikuwa na jumla ya wahitimu 57,303 wa kidato cha nne wakiwemo 35,653 wa shule za Serikali na 21,650 wa shule zisizo za Serikali. Wahitimu wa kidato cha sita walikuwa 11,744, wakiwemo 6,885 wa shule za Serikali na 4,859 kutoka shule zisizo za Serikali. Takwimu za wahitimu wa Sekondari hazitunzwi Kimkoa na Kiwilaya kwa sababu kufanya hivyo inakuwa haina faida wakati wanafunzi wa shule hizo ni mchanganyiko wa mikoa na Wilaya mbalimbali.

(c) Mheshimiwa Spika, idadi ya walimu wa shule za sekondari kwa kila mkoa imeonyeshwa katika Jedwali Na. 2 ambalo pia Mheshimiwa Mbunge atapewa. Kwa mujibu wa jedwali hilo mikoa mitano yenye walimu wachache kwa wastani wa asilimia ni Lindi, Singida, Rukwa, Pwani na Tabora.
Mikoa mitano yenye walimu angalau wa kuridhisha ni Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Iringa na Mwanza. Walimu hawapendi kwenda katika baadhi ya mikoa na shule kwa sababu shule zimejengwa bila nyumba za walimu. Wengine wako tayari kukaa

bila ajira kuliko kwenda kusiko na nyumba za walimu, hasa kule ambako hata zinazofaa kupanga haziko.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa katika shule nyingi katika Mikoa ambayo kuna shule nyingi ambazo zimeendelea na Wizara ina mpango wa *MMES* wa kusaidia sekondari kutoa fedha.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kusaidia mikoa ambayo ina shule chache kuwapa fedha nyingi kuliko mikoa ambayo tayari ina sekondari nyingi. Mfano mkoa wa Rukwa hauna sekondari nyingi, Lindi kwa mfano, Tabora aliyoitaja, Kigoma na kwingineko. Kwa nini hiyo isiongezewe fedha nyingi kuliko kuendelea kutoa fedha nyingi katika mikoa ambayo ina mashule mengi? Hilo ni la kwanza.

Pili kwa kuwa swali langu linaongelea suala linalohusu ubora wa elimu na kwa vile ubora wa elimu sasa hivi inaonekana na kuathiriwa sana na kuvuja kwa mitihani ya kidato cha nne na cha tano na mwaka huu ndiyo imezidi zaidi kwa ushahidi.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa tamko kwamba mikoa ile kama ya Rukwa ambayo haipati mitihani hiyo ya kuvuja lakini mikoa ile ambayo ina shule nyingi, inapata mitihani hiyo ya kuvuja, kwa nini mitihani hiyo isifutwe ili mikoa kama ya Rukwa, Kigoma, Tabora ambayo haipati mitihani ya kuvuja kwa sababu ya kuwa na shule chache iweje na yenyewe kufaidika kihalali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kama ifuatavyo:-

La kwanza anauliza ni kwa nini Serikali isizitengee au isiitengee Mikoa yenye shule chache ikilinganishwa na mikoa ile ambayo imepiga hatua kwa kuwa na shule za sekondari nyingi?

Mheshimiwa Spika, baadaye katika mpango ambao uko hapa tutamthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo limezingatiwa, lakini pia napenda niongeze kwamba hivi sasa nchi nzima kama alivyosema mwenyewe katika swali lake iko vuguvugu la wananchi kujenga shule za sekondari, sasa ni kule ambako wananchi watajituma kwa kuona umuhimu wa kujenga shule za sekondari huko Serikali haitowavunja moyo itawaongezea nguvu kusudi shule hizi zishamiri *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili Mheshimiwa Mbunge anauliza kwamba hivi sasa kumezagaa maneno hasa mijini kwamba mitihani imevuja, ukweli kwa hakika hatujaupata lakini pendekezo lake ni kwamba katika mikoa ile ambayo wanafunzi wanajituma kama enzi zetu wengine tulivyosoma.

Mheshimiwa Spika, anachosema ni kwamba kwa nini huku ambako mitihani imevuja ikithibitika kama mitihani imevuja kwa nini huku ambako wanaendekeza utaratibu huu mitihani isifutwe, lakini kule ambako hakuna hata fununu ya mitihani kuvuja ikabakishwa hivyo ili kuwatia adabu wale wanaoendekeza vitendo vya kuvujisha mitihani.

Mheshimiwa Spika, wazo hili Serikali inalichukua na litafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Na. 81

**Matatizo katika Sekondari za Wasichana Masasi na Ndanda**

**MHE. ARIDI M. ULEDI (k.n.y. MHE. RAYNALD A. MROPE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeandaa mpango mkubwa wa Elimu ya Sekondari *(MMES)* wenye lengo la kujenga upya na kukarabati shule za sekondari; na kwa kuwa shule nyingi za sekondari zilizojengwa zamani zipo katika hali mbaya:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati na kujenga uzio, kununua samani na usafiri wa uhakika kwa shule ya Sekondari ya Wasichana Masasi na Sekondari ya Ndanda?

(b) Je, ni lini tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama Sekondari ya Wasichana Masasi litapatiwa ufumbuzi?

(c) Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha walimu wa kutosha wanapatikana katika shule hizo hasa wenye taaluma ya masomo ya sayansi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* 2004 hadi 2009, Shule za Sekondari ya Wasichana Masasi na Sekondari ya Ndanda ni miongoni mwa sekondari kongwe zilizopangwa kufanyiwa ukarabati ambao utaenda sambamba na kuongeza nafasi zaidi katika shule hizo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwezo mdogo wa Kibajeti, Wizara hununua magari kulingana na uwezo wa wakati huo na kuyagawa kimkoa. Gari linaweza kukabidhiwa kwenye shule moja, lakini hutakiwa kutoa huduma kimkoa. Utaratibu huo utaendelea hadi tutakapokuwa na uwezo wa kuzipatia magari shule zetu zote za sekondari za Serikali. Katika mwaka 2003/2004 Wizara ilinunua magari aina ya *Toyota Double Cabin* manne na kuyagawa katika sekondari kama zifuatazo:-

(i) Loleza - Mkoa wa Mbeya
(ii) Kantalamba - Mkoa wa Rukwa
(iii) Mwenge - Mkoa wa Singida na
(iv) *Musoma Day* - Mkoa wa Mara

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalifahamu tatizo la ukosefu wa maji safi na salama katika mji wa Masasi ikiwemo Shule ya Sekondari ya Wasichana Masasi. Ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo unapaswa kushughulikiwa na Mamlaka husika za wilaya na mkoa. Hata hivyo hatua zinazochukuliwa na Wizara yangu za kuipatia maji shule hiyo ni pamoja na kuchimba kisima na kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua. Wizara yangu inalifuatilia kwa karibu sana tatizo hilo.

(c) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuwa na walimu wa kutosha katika shule zote za sekondari kwa masomo yote. Wizara yangu imechukua hatua mbalimbali za kuwapata walimu ikiwa ni pamoja na kuongeza nafasi katika Vyuo vya Ualimu vilivyopo na kugeuza Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam na Shule ya Sekondari Mkwawa kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kuongeza upatikanaji wa walimu wenye shahada. Aidha, Serikali imeendelea kuajiri walimu na kuwapanga katika shule zote kulingana na mahitaji. Kwa kipindi cha Mei hadi Agosti, 2004 Shule za Masasi imepangiwa walimu sita, wanne wakiwa wa masomo ya sayansi na Ndanda walimu nane kati yao ni wa masomo ya sayansi.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa shule ya Sekondari ya Masasi na shule ya Sekondari ya Ndanda zipo katikati ya miji ya Masasi na Ndanda, je, Serikali ni lini basi itajenga uzio kuzunguka shule hizo ili kuzuia uvamizi wa watu na mifugo katika maeneo hayo ya shule?

Swali la pili, kwa kuwa wanafunzi wengi wanaochukua masomo ya sayansi hukimbilia kuchukua ajira katika sehemu zingine badala ya kwenda kwenye ualimu, kutokana na maslahi duni ya kazi hiyo ya ualimu, je, Serikali itachukua hatua gani ili kuwavutia wanafunzi wengi wanaochukua masomo ya sayansi na walimu wengi waliochukua masomo ya sayansi kukimbilia kwenda kufundisha shuleni badala ya kukimbilia kwenye kazi ambazo wanaona kuwa kuna maslahi mazuri zaidi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimwa Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimwa Aridi Uledi, kama ifuatavyo:-

Kuhusu suala la ujenzi wa uzio ili kuzuia uvamizi wa watu wasiohusika na mifugo katika maeneo ya shule baadaye katika mkutano huu liko swali limeulizwa kuhusu suala la ujenzi wa uzio na tunachokisema katika Wizara ya Elimu na Utamaduni ni kwamba katika mpango huu wa kuboresha shule za sekondari ujenzi wa uzio ni moja ya maeneo yatakayotiliwa maanani na kupewa umuhimu upasao.

Mheshimwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba wahitimu wa masomo ya sayansi wanakwenda katika ajira nyingine badala ya kuzingatia ualimu ili waweze kufundisha masomo hayo kwa wanafunzi wengine, ningependa niseme kwamba kwanza ni kweli kuwa masomo ya sayansi wengi hawapendi kuyafundisha na haijulikani ni kwa nini.

Mheshimwa Spika, lakini la kuzingatia hapa si kwamba suala la uduni wa maslahi ya walimu hakuna ambaye anapenda kuona hili jambo linaendelezwa, sote hapa lazima tukiri tumepitia mikononi mwa walimu na kama isingekuwa ni hali ya uchumi wa nchi yetu pengine tungependa kuona walimu wanapewa kipaumbele.

Kwa hiyo, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, tufanye juhudi, tukuze uchumi wetu ili tuweze kulipana maslahi yanayolingana na jasho la kila mmoja wetu mahali pake pa kazi.

**SPIKA:** Maswali kwa Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuberi.

Na. 82

**Mpango wa Maendeleo ya Michezo**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kuhakikisha kwamba michezo inaendeshwa kisayansi, Serikali imeandaa muundo wa kutengeneza mpango wa maendeleo ya vyama vya michezo ikiwa na maeneo kumi.

(a) Je, ni maeneo gani hayo?

(b) Ni vyama vipi vilivyoonyesha mafanikio?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:

Kwa niaba ya Mheshimwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeandaa muundo wa kutengeneza mpango wa maendeleo ya vyama vya michezo yenye maeneo kumi. Maeneo hayo ni uongozi na utawala, ushiriki katika michezo, maendeleo ya wachezaji, maendeleo ya ufundishaji na maendeleo ya uamuzi.

Maeneo mengineyo ni mpango wa mashindano, mpango wa ugharamiaji wa michezo, maendeleo ya sayansi ya michezo, miundombinu ya michezo na siku maalum kwa chama husika

Mheshimiwa Spika, nakala ya mpango huo atakabidhiwa Mheshimwa Mbunge baada ya kipindi hiki cha maswali.

(b) Mheshimiwa Spika, vyama vilivyoonyesha mafanikio angalau kuyafanyia kazi baadhi ya maeneo ni Chama cha Kriketi Tanzania, Chama cha Mpira wa Wavu Tanzania, Chama cha Riadha Tanzania, Chama cha Olyimpiki Maalum na Chama cha Mpira wa Mikono Tanzania.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza na pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka kuuliza kama hivi ifuatavyo:-

(a) Katika mipango yote aliyoitaja hiyo inahitaji pesa na gharama, je, Wizara imejiandaa vipi kuhusu suala hili?

(b) Halafu suala la pili kwa kuwa unapoandaa mambo ya kisayansi ujitahidi angalau ulingane na wakati tulionao wa kisayansi lakini tatizo kubwa la vyama vyetu vinakabiliwa na migogoro, je, sayansi itaingia kwenye migogoro?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba michezo inahitaji gharama lakini kuifahamu gharama yenyewe na namna ya kuipata hiyo gharama utapataje hizo pesa, unahitaji kwanza kuwa na mpango wa aina hii, huu mpango ndiyo utakaokujulisha gharama halisi unayohitaji na namna ya kuipata. Bila kuwa na mpango wa aina hii ukatanguliza kwanza gharama sijui utazipataje maana hata mpango wenyewe huna, kwa hiyo, mimi ningeshauri tuanze kwanza na mpango huu ujue gharama zako halisi ili wanachama au wahusika na klabu hiyo au chama hicho waweze kuwa na mpango wa kuwa na gharama hizo.

(b) Ni kweli baadhi ya vyama vinaongozwa na migogoro lakini mimi ni imani yangu kwamba sisi ambao tuko nje tuna jukumu kubwa la kuwasaidia wenzetu ambao wako humo ndani maana aliyemo kisimani hawezi kujiokoa ila aliyekuwepo nje.

Kwa hiyo, migogoro inatia kichefuchefu, migogoro inarejesha nyuma maendeleo ya michezo yetu lakini maadamu ipo ni lazima tuhakikishe kwamba sote kwa umoja wetu tunasaidiana ili kuhakikisha migogoro hiyo hatimaye inaondoka kwenye vyama vya michezo na taratibu tunaona kwamba migogoro imeanza kuondoka kwenye Chama cha *Boxing* kwa mfano, Chama cha Riadha sasa hivi mambo yanakwenda vizuri. Ninaamini na vyama vilivyobakia migogoro nayo itaondoka.

Na. 83

**Maskini Omba Omba**

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU** aliuliza:-

Kwa kuwa ni utaratibu uliokubalika Kitaifa kuwa siku ya Ijumaa ni siku ambayo maskini/wahitaji huwa wanapita mjini na sehemu nyingine zenye mkusanyiko wakiomba chochote kwa riziki zao:-

(a) Je, inakuwaje maskini wa Dodoma wanaomba kila siku?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo hilo, ili waombe Ijumaa tu?

(c) Je, tunawatambuaje maskini, jirani mahitaji na tapeli?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haina utaratibu wa Kitaifa wa siku ya Ijumaa kuwa siku ya omba omba. Tunachofahamu ni kwamba siku ya Ijumaa kunakuwapo na mkusanyiko mkubwa wa waumini wa dini ya Kiislam na kwamba kutokana na imani yao wanatoa sadaka. Kutokana na kuelewa huko watu maskini omba omba hujitokeza kwa wingi kuomba siku ya Ijumaa.

Mheshimiwa Spika, maskini mwenye njaa na omba omba wa kweli hana siku maalum ya kuomba na si kweli kwamba omba omba wa Dodoma pekee ndiyo wanaoomba kila siku. Omba omba wapo kila siku katika miji ya Dodoma, Dar es Salam, Morogoro, Arusha na kwingineko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tendo la kuomba linamdhalilisha mwombaji na ni kielelezo cha umaskini. Serikali kwa kushirikiana na wadau na wananchi wenyewe imeweka dhamira ya kuondokana na umaskini. Mkakati sahihi wa kuondokana na tatizo la omba omba ni kuweka mazingira muafaka kwa wananchi kuweza kujiletea maendeleo ya kiuchumi na siyo kuhalalisha omba omba.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wapo omba omba wa kweli ambao ni maskini na hawana uwezo na wapo watu wenye nguvu zao na uwezo wa kufanya kazi lakini wanazunguka wakiomba. Mamlaka zinazohusika na tatizo hili zimeweka utaratibu wa kuwatambua omba omba wa kweli na matapeli. Omba omba wa kweli wanasaidiwa kuondokana na tatizo hilo kwa kupewa ushauri ili walelewe majumbani kwao au kupatiwa nyenzo za kumwezesha kumudu maisha. Omba omba wanaogundulika kuwa ni matapeli wanachukuliwa hatua chini ya sheria zilizopo kama Sheria ya Manispaa na ya Kanuni ya Adhabu.

**MHE. TEDDY L. KASELLA - BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya ngongeza:-

Kwa kuwa Dar es Salaam ilifanikiwa kuwarudisha omba omba makwao na makwao hapo ni nchi nzima na siyo sehemu moja ya nchi.

(a) Kwa kuwa hawa omba omba waliopo hapa Dodoma siyo wa Dodoma peke yake kama alivyosema Naibu Waziri, kwa hiyo, kwa nini hawa omba omba wa Dodoma wasirudishwe makwao kama wale wa Dar es Salaam, makwao maana yake nchi nzima pamoja na Mkoa wa Dodoma ambao unaishirikisha Wilaya zake zote?

(b) Kwa kuwa, hawa omba omba ni sehemu ya jamii yetu, kwa nini Serikali isiwatambue kwanza halafu wale kweli kweli ambao hawana ndugu na hawana makwao wapelekwe kwenye makambi na wakishirikisha *NGOs* ambazo zinashughulika na makazi ya wazee na Mashirika ya Kidini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli ipo sababu ya omba omba siyo tu wa Dodoma lakini katika miji yote kurejeshwa makwao hili litahitaji ushirikiano baina ya mji unaohusika kuwaondoa omba omba, mji au kijiji kinachopokea omba omba huyo lakini vile vile na jamii kwa sababu haiingii akilini kuamini kwamba omba omba tunaowaomba mijini hawana watoto wao, hawana wajukuu zao, hawana wajomba zao na hawana shangazi zao.

Kwa hiyo, ni lazima jamii sasa ibadilike tuone kwamba jukumu la kusaidia familia ni la kwetu sote badala ya kufikiria tu kwamba kuna *NGOs* au kuna Serikali ya kutoa huduma zile.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitambua omba omba kwa kushirikiana na taasisi na vikundi visivyo vya Kiserikali lakini bado tunasema ili tuweze kukamilisha suala hili ni lazima kila mwanajamii alipo ahakikishe kwamba tatizo hili ni la kijamii badala ya kulifikiria kwamba ni jambo la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho wapo omba omba wengine ambao ni matapeli kama walivyozungumzwa katika swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge, kuna matapeli omba omba wanaokuja na tai, lakini hata ukienda nje ya ukumbi wako wa Bunge, kuna siku watu wanakuja na kadi nyingi za harusi, *kitchen party* na kadhalika. Harusi ambazo hazipo lakini ndiyo omba omba nyingine ya kisayansi ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, naamini Watanzania tutajitahidi kufichuana ili tuweze kuishi kwa amani na salama. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, ingawa tulichelewa kuanza kipindi cha maswali lakini ili tusimege sehemu kubwa na kuathiri muda wa mjadala wa Miswada na Maazimio yaliyoko mbele yetu, mimi nitaishia hapo. Kwa upande wa maswali yaliyobaki tutayapangia muda mwingine, yaweze kujibiwa maana yake tukiendelea na maswali tutakula muda mkubwa sana wa mjadala na kwa hiyo, sasa ni matangazo.

Mheshimiwa Rosemary Nyerere, aliniarifu mapema kwamba anaye mgeni wake hapa Bungeni leo ambaye angependa nimtambulishe naye ni Ndugu Madaraka Nyerere, kutoka Butiama yuko pale. *(Makofi)*

Matangazo ya vikao vya Kamati, ziko Kamati tatu ambazo zinakutana leo, ya kwanza ni Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba Wajumbe wakutane saa sita mchana chumba namba 227 ghorofa ya pili. Saa sita mchana Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje.

Kati ya pili ni Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mgana Msindai, anaomba Wajumbe wa Kamati ya *LAAC* na Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kumbe Kamati zote mbili zinakuwa na kikao cha pamoja leo Jumanne, saa tano asubuhi katika ukumbi namba 219 ghorofa ya pili. Kamati mbili za *LAAC* na *PAC.*

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya mwisho ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Lephy Gembe, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, anaomba Wajumbe wakutane saa tano asubuhi hii katika chumba namba 231 ghorofa ya pili.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho wa matangazo ya vikao, tunaendelea na *Order Paper,* Katibu

## MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Shughuli za Bandari wa Mwaka 2004 *(The Ports Bill, 2004)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, walibaki wachangiaji wanne lakini mmoja katika hao wanne ameondoa jina lake kwa hiyo, sasa nimebaki na wachangiaji watatu, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na Mheshimiwa Rished Mohamed Abdallah. Nitawaita kwa mpangilio huo. Mheshimiwa Benedict Losurutia, kama *microphone* yako inafanya kazi, kama haifanyi kazi hamia mahali pengine.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu ya Muswada wa *The Ports Act* ya mwaka 2004.

Kabla sijasema neno kubwa sana na mimi nichukue nafasi hii ya kuunga mkono hoja hii, pili nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, pamoja na Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu na wataalam wote pamoja na wadau ambao wameshiriki kikamilifu kuandaa Muswada huu ambao utaleta Mapinduzi makubwa sana katika bandari zetu.

Sheria hii ambayo imeletwa mbele yetu ni kuweza kurekebisha sheria ya mwaka 1977 ya Bandari na kuweza kuimarisha na kuboresha kwa wakati ambao sasa tupo. Lakini la muhimu sana ambalo limeleta mabadiliko makubwa ni kuunda Mamlaka ya Usimamizi yaani *Tanzania Ports Authority* badala ya *THA,* mamlaka ambayo itaendesha Bandari zetu.

Mamlaka hii ambayo ni mpya ambayo ni Shirika, ni Mamlaka ambayo kwa sasa itakuwa ikiendesha bandari ya Dar es Salaam na Pwani, mwambao pamoja na Bandari ambazo zimezunguka Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. La muhimu sana bandari ni lango la uchumi baada ya kuwa lango la uchumi na sasa tunakodisha vitengo vyake wala siyo kubinafsisha.

Mheshimiwa Spika, kukodisha vitengo vyake kwa watu binafsi kwa suala hili naomba hii mamlaka mpya ambayo imekabidhiwa madaraka makubwa ya kuendesha bandari ndogo ndogo ni dhahiri kabisa kama Serikali haiwezi kusaidia chombo hiki hakitakuwa na uwezo kabisa wa kujiendesha, kwa sababu Bandari hizi zote zinaendeshwa kwa hasara.

Mimi sijaona mwekezaji yeyote anakuja kwenda kuwekeza mahali penye hasara, kwanza, unachukua ng'ombe mnono ndiyo unachinja baadaye ukiishiwa unakwenda kuchinja ng'ombe ambaye amekonda ndiyo utaratibu. Katika Bandari mali nono ilikuwa *Container Terminal* ilikimbiliwa na kuchukuliwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa wawekezaji wanafata mahali ambapo kunaleta faida. Kwa hiyo, naomba Serikali isichezee kwamba itajiondoa na kuwapa watu binafsi waendeshe hizi bandari ndogo ndogo lazima Serikali izinenepeshe ili iweze kuchukuliwa. Hizi bandari zikishakuwa nono na zikishapendeza ndiyo zitachukuliwa. Ukiacha zimekonda namna hiyo hakuna mtu atakayezichukua. Kwa hiyo, naomba Serikali isaidie *TPA* kwa hilo. *(Makofi)*

La pili, ambalo nataka nilizungumzie kuna suala zima la kwamba bandari ni suala la Muungano na liko kwenye Katiba. Nataka Mheshimiwa Waziri ajaribu kufafanua hili kwa sababu suala la Muungano ni suala nyeti kabisa, linahitaji kuimarishwa. Lakini biashara sio suala Muungano na bandari zinafanya biashara na Bandari ni Muungano, biashara sio Muungano. Sasa bandari ikifanya biashara inatoka nje ya Muungano, kwa sababu ni suala la biashara.

Mheshimiwa Spika, sasa tunataka kuelewa migongano hii maana yake Bandari ya Zanzibar inafanya biashara yake si suala la Muungano, bandari ya Dar es Salaam

inafanya biashara yake sio suala la Muungano. Lakini suala la usalama na bandari ni suala la Muungano.

Naomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie suala hili ili tuweze kuimarisha Muungano wetu na ndiyo mimi ninavyoelewa. Lakini tupate kwa kina kwa sababu ni muhimu sana kama bandari ni suala la Muungano, basi tuunganishe vyombo hivi vyote kwa pamoja, biashara pamoja na Muungano ili tuweze kupata ufafanuzi wa kutosha. Mimi naomba hilo kwa sababu ilileta utata na inatuletea utata tupate ufafanuzi mkubwa sana.

Tatu, nataka nisisitize tena kuhusu *TPA* kuna suala la wawekezaji. Mimi sina uhakika suala la malipo ya Shirika kwa *PSRC* na Hazina wanapomkodishia mtu au wanapompa mtu ni mara nyingi sana inakuwa suala la siri, hatujui fedha hizo ni kiasi gani wanapouza wala haziko wazi au wanapewa bure. Tunasikia sikia hata Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro kwa mwaka kinalipia sijui dola 1,000. Sasa kwa nini inakuwa siri, tujue kwamba wanapouza na kukodisha kwa nini hawawi wazi? Maana yake hizo fedha sisi tutajuaje? Mtu anaweza kukodisha kumbe ni chetu, hazipo wazi.

Naomba Serikali iwe wazi katika mikataba hii ili tuweze kujua. Nasema hivi kwa sababu tuna wasiwasi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, la nne, kuna mrabaha, suala hili naomba sana Wizara pamoja na *PSRC* katika kubinafsisha vitengo vya bandari wazingatie sana mapendekezo ya wataalam. Kwa sababu tukiuza hivi hivi kwa urahisi kitakachoumia ni *TPA,* lazima tujue kabisa kwamba unapomkodisha mtu miaka kumi, sasa fikiria vile vile na vyombo. Hiyo Mikataba unamkodisha mtu miaka kumi hanunui chombo chochote ndani ya Mkataba inabaki chini ya Serikali, anapomaliza miaka kumi yeye anaondoka. Yeye anakuja anavuna akishamaliza kwenye mikataba haipo kuimarisha bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana suala la mrabaha iangalie *percentage* yake. Tunayo mifano mingi sana pamoja na kwamba tunasema tumefanikiwa katika *Container Terminal,* lakini kitu tunachopata ni kidogo mno, hakilingani kabisa, wao wanapata zaidi. Lakini kwa sasa hivi ambapo kuna ushirikiano mkubwa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na napenda kuipongeza kabisa hii Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri aliyepo sasa hivi, kwa kweli anaendesha suala hili la ubinafsishaji katika bandari kwa makini sana, anakwenda kwa utaratibu na masuala ya wafanyakazi anahakikisha kabisa kwamba hakutakuwepo na mgogoro wa aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyakazi kutoka *THA* kwenda *TPA,* kwa kweli mimi nashauri kwa upande wangu kwamba walipwe mafao yao yote ili waanze upya. Wakianza upya watafanya kazi mpya na kama ni suala la kurithi unaweza kuhamisha ugonjwa ukapeleka ugonjwa mwingine. Kiwe chombo kipya na waweze kuchagua nani mzuri na nani ambaye ni mbaya, sio suala la kurithi waombe kwa sababu hii inatoka kwenye Taasisi ya Serikali inakwenda tena kwenye Taasisi nyingine, Shirika la Umma vile vile. Kwa hiyo, ifanyiwe uchunguzi wa kutosha katika suala hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa siku za usoni *TPA* kuangalia bandari zote hizi katika Tanzania nzima limepitwa na wakati kabisa na ni mzigo mkubwa. Tufate kwa mfano hili ni wazo ambalo kwa kweli nalifikiria kwamba kwa nini *TPA* Dar es Salaam iangalie *Mwanza Port,* kwa nini isiundwe mamlaka ya *Mwanza Port* chini ya *Mwanza Municipal* au Kigoma kule waunde Taasisi, wataelimishwa na kadhalika. Kwa sababu hainyimi, kuna madini sasa hivi Kahama, kuna Almasi, *Tanzanite* kama ni mrabaha au fedha za kupelekwa Hazina zitatoka huko huko kuliko chombo kimoja kuhangaika katika nchi nzima kwenda Kigoma, Nyasa, Mwanza, Tanga ni ya kazi gani hiyo?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Tanga isiendeshe *Port* ya Tanga na kuundia mamlaka yake huko huko? Kwa nini Mtwara isiendeshe *Port* ya Mtwara, Dar es Salaam inakuwa Dar *es Salaam Ports?*

Mheshimiwa Spika, halafu tunapata tu kuliko kutengeneza kitu kikubwa ni kuhangaika tu eti, *Engineer* mmoja wa Dar es Salaam ndiye anaangalia *Ports* zote za Tanzania nzima, hiyo imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, ni suala la ukiritimba tu na ni suala la kukumbatia mambo tu wala haziendi wala hazisogei. Kwa hiyo, siku za usoni tujifunze kwa wenzetu wanavyofanya. Kwa hiyo, naomba sana katika kipindi kijacho tupitishe hii ifanyie kazi. Halafu uje tena Muswada wa kugawanya gawanya ndiyo maana kuna Wilaya, Kata, Vijiji kuliko vitu vikubwa mtu mmoja anakaa katika meza moja kutoka hapa mpaka kwa Spika. *(Kicheko).*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kuhusu Mamlaka Mpya ya Bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane na hoja hii na niiunge mkono kwa sababu mabadiliko ni kitu muhimu kuanzia mwaka 1977 mpaka leo ni mambo mengi yamepita hapo katikati. Kwa hiyo, ni lazima twende na wakati. Kwa hiyo, mabadiliko ni kitu muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize kwa makini kwa sababu suala la bandari ni suala nyeti. Nasema hivyo kwa sababu zaidi ya asilimia 90 ya mapato au kodi ya nchi nzima ya Tanzania inatoka Dar es Salaam kwa maana ya bandari. Kwa hiyo, ni uhai wetu uko pale. Kwa hiyo, nina mapendekezo au ushauri katika Serikali hii kuhusu suala la bandari ambayo ningeomba yaangaliwe wakati wa utendaji.

Mheshimiwa Spika, bandari yetu kwa kweli tunasema tuwape watu binafsi waendeshe kwa ufanisi. Mimi naona kama kweli wataendesha kwa ufanisi sioni kama ni jambo baya, kama kweli wataendesha kwa ufanisi. Lakini kuwe na *Regulatory Board* ambayo itaangalia kwa karibu kwa sababu bandari ya Dar es Salaam na bandari zetu zote ni uhai wetu.

Mheshimiwa Spika, nalisema hilo kwa sababu gani. Ukiangalia Mawakala waliopo sasa hivi ndani ya bandari zetu ukifanya mahesabu fedha wanazokusanya kwa mwezi na fedha wanazolipa Serikalini ni chini ya asilimia kumi. Sasa tukiendelea bila kuangalia na kuweka *Regulatory Board* tutaendelea kusema tunafanya ufanisi, lakini mapato Serikali inakuwa haipati. Kwa hiyo, kama hizi wanazosema *Container Terminal* na vitengo mbalimbali vya bandari zetu tuangalie namna ya kuwadhibiti hawa watu ili kikubwa tupate sisi Serikali na wao wapate kidogo, wao ndiyo wanatakiwa wapate asilimia kumi, sisi ndiyo tupate asilimia 90, siyo wao wapate asilimia 90 na sisi tupate asilimia kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naomba Wizara inisikilize na iliangalie kwa makini ni juu ya ufanisi ndani ya bandari zetu. Hali ya bandari zetu sio kama tunavyozifikiria au tunavyoona hapa, inatisha. Kama ungekuwa na darubini ukawa juu labda kwenye *satellite* ukaangalia mizigo ambayo ingepaswa kuteremshwa Dar es Salaam inavyoteremshiwa Mombasa. Ukiangalia *Customs* za mipakani kwetu hata sasa hivi tunavyoongea hapa namna ya mizigo na magari na mali nyingine zinapitia pale baada ya kuteremshwa kwenye bandari ya Mombasa inatia kichefuchefu.

Mheshimiwa Spika, pia na hili kwa nia nzuri kabisa namwomba Mheshimiwa Waziri na namfahamu ni mchapakazi wala hakuna ubishi kwenye hilo aunde Tume kwani tunapoteza fedha Tanzania. Aunde Tume ya kuchunguza matatizo gani ambayo tunayo katika bandari zetu watu wanakimbilia Kenya kuteremsha mizigo Mombasa, tunapata hasara kubwa kwa kuteremshia mizigo Mombasa. Mtu anateremshia mizigo Mombasa anakuja Mpakani Horiri au Horohoro au Namanga, anasema huu mzigo ni wa *transit,* unakwenda Zambia, lakini hauendi Zambia anakuja kuteremshia hapa Tanzania wanauza katika maduka yetu. Hilo nasema ni la kuundia Tume wala sio la mchezo. Hayo ndiyo matatizo ambayo yapo sasa hivi kama ukienda Mheshimiwa Waziri kwenye barabara hii ya kwenda Arusha utakutana na magari yamefuatana namna hii! Yanatoka Mombasa yanakuja Tanzania. Kwa hiyo, hilo siyo jambo la kufumbia macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nchi hii tunaamini kwamba bandari ndiyo uhai wetu, tunatengeneza barabara kutokana na kodi zetu na tunaamini kwamba asilimia 90 ya kodi zinatokana na bandari zetu, basi ni lazima hilo tulifuatilie kwa karibu. Mimi nina ushahidi na nasema sasa hivi ukienda katika barabara ya kwenda Arusha utakutana na magari ya mizigo yanayotoka Kenya kupitia Mpakani! Ikiwa mizigo hiyo imepakuliwa katika bandari ya Mombasa, je, sisi tunafanya nini? Hivyo hatutakwenda!

Mheshimiwa Spika, sasa sababu nyingine ambayo naifahamu mimi mwenyewe nimejaribu kufanya utafiti katika bandari yetu ya Dar es Salaam. Mimi mwenyewe nilikuwa na gari bandarini, nikaenda na fedha zangu pale *Dar es Salaam Port,* nikasema hebu niangalie wala siendi kwa mkubwa anisaidie kwani kuna wakati nilienda kwa mkubwa akanisaidia nikalipata lile gari mapema. Haikuwezekana, nilikuwa na fedha zangu pale pale sikuweza kukomboa lile gari bila kulipia *storage charges* na fedha nilikuwa nayo na wakala nimemweka wa kunisaidia nipate mzigo wangu mapema.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema iundwe Tume. Niliwauliza wale Mawakala wakasema sio rahisi kuweza kutoa mzigo bila kulipia *storage charge.* Sasa kama wametoa siku saba wamefuatilia kwamba hizi siku saba zinamtosha mtu kutoa mzigo wake bila kulipia gharama zingine? Au je, bandari inafanya hivyo kwa makusudi ili ipate mapato ambayo hayana mpangilio? Mtu ukiagiza mzigo wako nje unajua kabisa hapa bandarini nitalipa shilingi 10/=, *handling* nitalipa shilingi 20/= na *time* ikifika nitachukua mzigo wangu. Lakini unaenda pale wanakwambia aah, lipa za kuchelewesha mzigo, nimeuchelewesha wapi? Mimi nimekuwa hapa hapa bandarini nimeuchelewesha vipi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sio mimi pekee kwani hakuna mtu yeyote ambaye anatoa mzigo bila kulipia *storage charges.* Naomba hiyo Tume ikachunguze haya maneno yangu nikikutwa ni mwongo basi waje waniadhibu hapa. Hakuna mtu anayetoa mzigo bila kulipia *storage charge.* Haya wanasema siku saba, *public day* wanakwambia wewe mteja unahesabiwa, wao kwao hawahesabu, wewe mteja unahesabiwa kwamba ni siku ya pili au ya tatu, lakini wao hawafanyi kazi lakini wewe unahesabiwa. Sasa hayo mambo mtayaona ni madogo, lakini yanafanya wafanyabiashara wanaikimbia bandari yetu wanakimbilia Kenya ambako wanaona ni rahisi unapakua haraka mzigo wako unalipa fedha zao. Sasa hizi fedha zote zinaenda Kenya na ni fedha za kigeni, kwa nini Wizara isiamue haya niliyoshauri ya kuunda Tume ili fedha hizi zipatikane na zirudi kwetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye wenzetu ambao tunahitaji kuwatumikia. Tunahitaji kuwatumikia watu wa Rwanda, Burundi, Kongo na Zambia sisi tuko *centre* kuliko tunavyosema bandari ya Kenya, tuko *centre* zaidi sisi. *South Africa* sasa hivi wanaunganisha reli za *SADC* ili waweze kufanya ufanisi mzuri katika bandari zao kiuchumi. Kwa sababu wamekwishajua fedha zinapatikana bandarini hilo ndiyo nataka Serikali hii ijue, fedha zinapatikana pale bandarini.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna mpango gani wa kuunganisha reli zetu mpaka Uganda ili ziweze kupeleka mizigo kwa urahisi Burundi na Rwanda na hata Kongo? Je, tuna mikakati gani? Kwa sababu wenzetu wanakimbia, angalau sisi tulikuwa tumesimama angalau tutembee basi labda kukimbia hatuwezi kama wa *South Africa.* Lakini angalau tutembee na kutembea maana yake tufikirie sasa kwamba hawa wateja wetu ambao ni Burundi, Rwanda, Kongo na hawa wateja ambao ni Zambia basi tuweke miundombinu ya kutosha ili tuweze ku-*capture* hizo fedha zao ili tuweze kupata fedha nyingi na uchumi utakua zaidi katika nchi yetu na kwa kufanya hivyo tutapata uchumi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa hivi hii mizigo niliyosema inapita hivi sasa tunavyozungumza hapa katika *custom* za Mipaka yetu na naomba nipate hiyo ripoti ya mwaka mzima kwamba imepita mizigo kiasi gani katika *custom* za Kaskazini ya Mipaka yetu. Horiri, Horohoro na Namanga nipate taarifa kwa mwaka mzima ili Mheshimiwa Waziri aweze kujua mwenyewe hata kama ni kwa faida yake mwenyewe. Lakini sio hiyo tu mizigo mingine inapitia huko huko Kenya kwenda Uganda na kwenda Burundi ni hasara ngapi tunatengeneza? Je, hizi hasara tutazi-*cover* namna gani?

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema kwamba mimi naunga mkono mabadiliko haya. Lakini haya mabadiliko basi yaende na wakati. Tuangalie wenzetu na tuwe na hiyo *Regulatory Board,* tuchunguze kitu gani kinakosekana hapa kwetu na kikapatikana pale Mombasa na kwa nini tusikifanye hapa Tanzania? Kama unapata shilingi 80,000 x 200 na mwingine anapata shilingi 90,000 x 100 sasa huyo wa shilingi 90 atakuwa hajapata kitu. Kwa hiyo kama mnazidisha fedha nyingi za kodi kwa ajili ya kufikiria labda mnapata sana, hazipatikani kwa sababu mizigo inakuwa michache yaani kazi inakuwa ndogo kulingana na Mombasa ambako labda wanapunguza kidogo mambo fulani na wanakuwa *efficient.* Sasa wanapata kazi nyingi na mapato yao yanakuwa ni makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni nafuu kupunguza kodi ili tuweze kupata kazi nyingi na ili tuweze kuwa na fedha nyingi kuliko kusema hapa tuweke fedha nyingi kwenye *charges* ambazo nimesema ni *charges* za ajabu ajabu ambazo zinazunguka kwa watu hata hizo fedha hazifiki Serikalini. Tupunguze urasimu huo, tukishapunguza huo urasimu na tukifuata hayo niliyosema mimi naamini kwamba tutachangamka na kazi zitakwenda na huo ni ushauri kwa rafiki yangu Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, ambaye ni Mheshimiwa Waziri mchapakazi, naamini kabisa kwamba anaweza akalifanyia kazi hilo jambo kwa mwezi mmoja likawa tayari na sisi tukapata matokeo mazuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kabla sijazungumza lolote, kwanza niseme naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba lengo ni kuongeza ufanisi bandarini na hatimaye kuongeza Pato la Taifa na vile vile kuongeza ajira. Lakini la msingi vile vile ni usalama wa mali za watu ambazo zinapita katika bandari hizi. Sasa kuna tofauti ya bandari zetu zilizoko nchini na kati ya bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Bandari ya Dar es Salaam karibu ina-*facility* zote za kuteremsha mizigo na kupakia mizigo kwa maana vile vile na meli ndogo ndogo za abiria.

Mheshimiwa Spika, sasa naamini kwamba hiki chombo kipya tunachokizungumzia sasa hivi kiweze kutoa kipaumbele kwa maana ya kuongeza ufanisi na kuongeza mapato katika Taifa letu wazingatie hizi bandari nyingine za Tanga na Mtwara zinakuwa na *facility* kama zile za Bandari ya Dar es Salaam. Inawezekana labda itagharimu fedha nyingi, lakini angalau basi kama kuna mipango ya maendeleo ambayo imekwishaanzishwa huko nyuma. Kwa mfano, pale Tanga kuna suala zima la kujenga bandari mpya kule Mwambani, hili litiliwe mkazo kwa sababu huko tunakokwenda shughuli za biashara zinazidi kupamba moto na kuna *competition* kubwa ukilinganisha na nchi jirani zinavyokwenda mbele kama Msumbiji na bandari ya Mombasa. Kama hatutatilia mkazo kuhakikisha kwamba hizi bandari nyingine za Tanga

na Mtwara hazitofanyiwa marekebisho haraka ili kuweza kushindana na bandari zingine za majirani zetu, mimi naamini tutaachwa nyuma kwa hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa nashauri hiki chombo kipya kinachoundwa kitoe kipaumbele katika bandari hizi nyingine ili ziweze kwenda na wakati kutokana na hali halisi iliyokuwepo. Tumesaini na tumeridhia Mikataba mingi sana ya Afrika Mashariki na *SADC*. Kwa hiyo, ili tusiwe ni soko kwa nchi nyingine, basi na sisi tutumie bandari zetu kwa ajili ya kusambaza mizigo ya nchi jirani na *potential* kubwa ipo Burundi, Rwanda pamoja na Kongo. Tunayo nafasi nzuri na kubwa zaidi kwa kupeleka mizigo katika nchi hizi tatu nilizozisema kuliko Kenya na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, sasa niulize swali pale Tanga zamani kulikuwa na kiwanda cha mbolea na wamejenga *Jet* kwa ajili ya kuteremshia vifaa mbalimbali au malighafi kwa ajili ya kiwanda kile. Kile kiwanda kimefungwa na hivi sasa kimekwishauzwa kwa mtu binafsi, lakini bado zile *infrastructure* ziko pale. Lakini ile *Jet* haifanyi kazi nafahamu kwamba ina matatizo na ni kituo muhimu kwa kuweza kuegesha meli mpaka kwenye gati lile na ikatumika kama bandari ndogo kwa ajili ya kuteremshia bidhaa maalumu au zingine zozote kama vile magari tunaweza tukateremshia pale.

Mheshimiwa Spika, hivi utaratibu wa *Jet* ile imefikia wapi au Serikali au Mamlaka husika ina mpango gani wa kuishughulikia *Jet* ile au imeuzwa kwa yule aliyenunua kiwanda cha mbolea? Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kutufahamisha hatma ya ile *Jet* kwa sababu kila muda unapopita inazidi kuharibika.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niulize swali lingine, *powers* walizopewa hii *Tanzania Ports Authority* kama vile sasa hivi hii *Tanzania Port Authority* itakuwa inaendesha shughuli za biashara na kwa ajili ya kufanya *investment* katika hizi bandari kama Waheshimiwa Wabunge wengine waliokwisha kusema kwamba ili kuvutia meli nyingine kuja nchini ni lazima tuziweke hizi bandari katika hali nzuri ili na wao waweze kuvutiwa kuteremsha mizigo yao hapa kwetu. Lakini katika kuwekeza sioni kama sheria inasema kwamba Taasisi hii inaweza ikachukua mikopo benki na kufanya *investment* katika bandari zake.

Sasa hebu tungepata ufafanuzi kama wanayo nafasi na fursa hiyo tuna taasisi nyingine ambazo zinachukua mikopo benki na zimepiga hatua kubwa kama vile *NSSF,* wanakopa, wanajenga majumba, ile ni *investment* kubwa na wao wanajiendeleza vizuri.

Je, hii *Tanzania Port Authority* itakuwa na uwezo huo wa kuweza kukopa katika Mabenki siyo tu ya Tanzania hata Mabenki mengine ya Kimataifa ili waweze kuwekeza katika bandari zetu na hatimaye kuwezesha biashara hii ambayo wataifanya wao na hatimaye taifa liweze kuingiza pato la kutosha na kuweza kupata ajira kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, lingine katika Muswada inazungumzia suala zima la kuondoa mabaki ya meli ambayo meli hizi zimezama kwa njia moja au nyingine. Ziko meli ambazo zimezama toka Vita vya Dunia vya Kwanza na vya Pili na mpaka hii leo meli hizo hazijaondolewa katika sehemu yake. Sasa sijui katika Muswada huu inazungumzia

meli ambazo zimeegeshwa katika bandari mbalimbali za Dar es Salaam labda na Tanga na Mtwara lakini yako maeneo mengine ambayo tunayaona kwamba ni bandari muhimu ndogo katika nchi yetu ambazo zitaweza kuongeza ajira na kupata mapato katika Wilaya zetu ndogo ndogo.

Natoa mfano halisi wa Wilaya ya Pangani kuna meli iliyozama katika milango ya Mto Pangani na Bahari ya Hindi, meli ile ilizama wakati wa Vita vya Dunia vya Pili. Meli ile iyozama pale inatukosesha mapato mengi katika bandari ndogo ya Pangani kwa sababu imekuwa ni kikwazo kwa meli nyingine kuweza kuingia pale, meli ile ikishakuwa ni kubwa kidogo inakuwa ni matatizo kuingia pale. Je, utaratibu huu wa meli kama hizi, chombo hiki kitaweza kushughulikia namna gani kwa sababu tuna wasiwasi kwamba labda meli ile ilikuwa ni ya kivita na imezama pamoja na mabomu yake sasa je, ni mpaka lini Serikali itachukua utaratibu wa kuondoa mabaki ya meli ile ili angalau na sisi pale Pangani tuweze kutumia ile bandari ndogo kwa shughuli zetu?

Mimi naishauri Serikali kwamba kuna bandari kama hizi za Pangani, Bagamoyo ndogo ndogo ni kwa nini majahazi yote yaende katika zile *Port* kubwa kama za Dar es Salaam, Tanga ni vema basi kama kuna vyombo maalum kama majahazi haya yakateremsha mizigo katika hizi bandari ndogo na hatimaye sasa kuwapa nafasi bandari hizi ndogo angalau kuwe na mwamko wa shughuli na kuongeza ajira kwa vijana walioko pale na kupata mapato. Hii iende sambamba na kuweka maboya ambayo yataweza kuelekeza meli ambazo zitaweza kuingia katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, mwisho nilikuwa nataka nizungumzie suala zima la *survey,* nina amini bahari yetu imekuwa *surveyed* pamoja na baadhi ya Maziwa lakini nitoe taarifa kwamba nina uhakika Ziwa Tanganyika mpaka dakika hii halijakuwa *surveyed.* Hii ni hatari kwa Ziwa kama lile kubwa lenye kina kirefu zaidi ya pili katika dunia na kwamba Ziwa lile mpaka leo halijafanyiwa *survey.* Hakuna *navigation system* yoyote ambayo inaweza ikamwongoza mwongoza chombo akasafiri kutoka Kigoma kwenda katika nchi nyingine ya Kongo.

Nashauri kwamba hii *Authority* itakayoundwa itizame upya suala zima la kuweka *charts* au *navigation charts* kuwekwe na *landmarks* kuwe na *light houses, bowyers* ambazo ni *channel bowyers* na *middle ground bowyers* ili angalau basi kuwe na taarifa muhimu za *survey* ya Ziwa lile ili vyombo vinavyoondoka pale Kigoma kwenda katika nchi jirani na sasa hivi ni mlango mzuri wa kufunguka kwa biashara kati ya Tanzania na Kongo na Burundi kwa kutumiwa Ziwa Tanganyika, hivi sasa wawekezaji wanapeleka *boat* za abiria ambazo zitakwenda kwa kasi kule.

Lakini napata wasiwasi kwamba *boat* hizi zitakapo safiri na hasa wakati wa usiku hakuna alama zozote zitakazo mwezesha *navigator* huyu kuweza kufika salama na abiria wale au meli yoyote ya mizigo kuweza kufika salama katika maeneo anayokwenda.

Mimi nashauri kwamba hili lizingatiwe na vile vile pale Kigoma kwa vile tumetembelea, tumekuta kwamba gati la Kigoma linajumuisha shughuli za usalama kwa maana Jeshi la Polisi pamoja na raia, sasa hii kwa kweli hatuwezi tukafanya mikakati ya

kiusalama pale na wakati wengine wapo upande wa pili kwa maana ya hatua labda mita hamsini au mia moja wanaona shughuli zote zinazofanyika pale.

Sasa huu usalama tutaupata vipi na sisi Serikali tunaelewa kwamba tumepakana na watu ambao kwamba nchi zao zina matatizo, kuna wakimbizi na kuna vita, ni hatari vile vile kwa usalama wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vilivyokuwepo katika bandari ile ya Kigoma. Mimi nashauri kuwepo na taratibu ya kupima maeneo ya kuweza kuegesha *boat* za ulinzi na usalama na zile za kiraia ziwe zinatenganishwa. Hii italeta ufanisi wa shughuli nzima katika usalama wa Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mwisho kabisa katika suala la usalama, Serikali ifanye juhudi kubwa ya kuweka vyombo vya kutosha kwa ajili ya ulinzi wa bahari yetu ili kuepukana na wizi wa mali au raslimali, maliasili zetu zilizokuwepo katika Bahari ya Hindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, raslimali zetu nyingi zinaporwa kwa sababu ya kutokuwa na *facility* za kutosha za kuweza ku-*detect* au kufuatilia mwenendo au vyombo vingine vya kigeni zinazoingia katika maeneo yetu ya maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niseme kwa mara ya pili naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, ninayo machache juu ya hoja hii ya kubadili sheria ya bandari ya Mwaka 1977na kuweka sheria mpya ambayo inaendana na wakati tulionao hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni muda mrefu sasa tangu sheria hii ya mamlaka ya bandari kuwepo bila mabadiliko yoyote na hasa ukizingatia mabadiliko mbalimbali yanayotokea duniani kama vile utandawazi. Aidha kuwepo meli za kisasa zenye kupakua mizigo zenyewe na kadhalika. Hivyo kuna haja ya kubadilika kufuatana na hali halisi.

Mheshimiwa Spika, ninayo machache ambayo nitayasema hapa ili Mheshimiwa Waziri atakapomalizia atoe ufafanuzi kuhusu maswali yafuatayo:-

(i) Ni kwanini kila mwenye mizigo inayopitia bandari ya Dar es Salaam lazima alipe gharama za ucheleweshaji wa mizigo bandarini wakati aliyechelewesha ni mamlaka yenyewe kutokana na urasimu uliopo ndani ya mamlaka yenyewe?

Mimi mwenyewe nimekuwa na gari langu na nikawa na fedha zangu za kulipia kodi pamoja na madai ya bandari yaani *handling charges* lakini pamoja na mimi mwenyewe kuwepo pale sikuweza kupata lile gari bila ya kulipia ucheleweshaji.

Kama mimi mwenyewe ni kiongozi na nimekuwa bandarini na fedha zangu za kulipia ili nipate mzigo wangu, ni vipi imeshindikana hadi nikalipia gharama za ucheleweshaji? Nimejaribu zaidi ya mara nyingi lakini ni wakati mmoja tu nilifanikiwa kwa kumtumia kiongozi na kuandika kwenye karatasi yangu:”Haraka Sana.”

Mheshimiwa Spika, mimi ni kitu kidogo sana kwani ukilinganisha na mapato ya bandari ila tuangalie kuhusu Watanzania wengi ambao kwa kukosa pa kusemea wanatumia bandari ya Mombasa! Angalia takwimu kwenye Mpaka wa Tanzania na Kenya kuwa ni mali ngapi zinazopitia hapo na za thamani gani? Je, zinazokwenda Zambia ni ngapi? Je, Burundi na je, ukijumlisha kama zingepitia Tanzania tungepata mapato ya kiasi gani? Ni kwa nini hatuangalii mapungufu yetu ili tukafanikiwa kiuchumi? Kwani mdharau mwiba tende litamuota miguuni. Dosari ndogo ndogo zinaipa bandari ya Mombasa heshima isiyopaswa. Tupunguze urasimu ili twende sambamba na hali halisi.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii iunde Tume kwenda *physically* kwenye bandari ya Dar es Salaam na kuchunguza haya niliyosema humu na pia waende kwenye mipaka yetu na Kenya ili kuangalia mali zilizopitia hapo kwa kipinidi cha mwaka mmoja na mwisho mali zinazopitia Mpakani kuelekea Zambia au Burundi Ruanda na Kongo pia.

Mheshimiwa Spika, nikipata majibu sahihi ya wasiwasi huu unaona uchumi wetu, nitaunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Kabla ya yote naomba kuunga mkono hoja. Nashukuru Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Katibu Mkuu na timu yao kwa ushirikiano wao ambao unaleta ufanisi kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo ninalotaka kulisisitiza ni juu ya Bandari ya Kilwa ambayo ina kina zaidi ya mita 40. Katika hali ya kawaida kuna meli kubwa zimeshaweza kutia nanga na kushusha vifaa vya uchimbaji mafuta katika miaka ya 2001 hadi 2002.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa bandari hii utatuondolea tatizo la kubeba mizigo ya kibiashara kutoka Kilwa kwenda Dar es Salaam na kutoka Kilwa kwenda Lindi na Mtwara. Hivi sasa kuna tatizo kubwa la kusafirisha bidhaa za wananchi kutokana na ongezeko la mafuta ya *Diesel* na *Petrol* pia tatizo la hali ya barabara ilivyo sasa.

Pendekezo la mwisho ni kwamba katika Bodi ambayo itaundwa kila eneo kijiografia lazima iwakilishwe. Mfano kuwepo na mwakilishi wa Kanda ya Kusini mfano, Njombe mmoja ambaye atawakilisha bandari za Kilwa - Lindi na Mtwara hata kama kuna wawekezaji binafsi. Mwakilishi ni muhimu kwa ajili ya ufanisi wa kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, namaliza kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuleta Muswada huu muhimu ambao una maneno muhimu yanayozidi kuboresha huduma katika bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kukuomba tu uzidi kusukuma mizigo mingi ipitie bandari ya Tanga.Tumeamua kuanzisha soko la Kimataifa pale Segera hivyo shehena zitakuwepo baadaye za matunda na mboga.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja zaidi.

**SPIKA:** Sasa watoa hoja watahitimisha hoja yao naanza na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kidogo kwenye hoja iliyopo mbele yetu lakini kabla ya kuchangia napenda nichukue nafasi hii kuishukuru Kamati ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo na Makamu wake, Mheshimiwa Henry Shekiffu, kwa ushirikiano mkubwa walionipa wakati nikiwasilisha Muswada huu katika Kamati.

Pili, napenda niwashukuru wataalam wetu wote wa bandari, wa Wizara, wale wa *TCFB,* wa *AG Chambers,* wa *Marine Services* na wa *PCRC* kwa ushirikiano wao ambao ulituwezesha kufanikisha kazi yetu hii ya Muswada.

Mwisho kabisa napenda kupitia Bunge lako Tukufu niwashukuru wadau wote walioshiriki kutoa maoni yao mbalimbali ambayo yalisaidia sana kuboresha vyema Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, sasa noamba nichangie machache katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, takriban Wabunge wote waliochangia wameunga mkono Muswada huu, tunashukuru sana mawazo yao mengi yamesisitiza yale ambayo tumekwishayatolea maelezo ya awali na sisi tunasema tunawahakikishia utekelezaji wake. Maoni mengine ni kama yafuatayo: -

Kwanza tumetakiwa tufanye maandalizi ya haraka ya kumalizia uudwaji wa vyombo vya usimamizi kama vile *SUMATRA, TICRA* na kadhalika. Nasema hili liko katika hatua za mwisho. Bodi ya *SUMATRA* imeshateuliwa na Mwenyekiti yupo tayari kwa mujibu wa sheria na Mtendaji Mkuu ameshateuliwa, labda Mheshimiwa Waziri atapata nafasi kulieleza Bunge lako Tukufu hatua iliyofikiwa.

Mheshimiwa Spika, pili Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, alihoji tu mambo yanayohusu masuala ya *SUMATRA* kifungu 51 (1) kifungu kidogo cha pili na alidhani yeye kwamba *SUMATRA* inapanga bei lakini tunasema kwamba *SUMATRA* haipangi bei, *TPA* inayo mamlaka ya kupanga bei. *SUMATRA* inahakikisha tu kwamba bei zilizopo haziumizi mlaji wala mtoa huduma ili kumwezesha kuendelea kutoa huduma na kuimarisha ushindani.

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo nitalizungumzia ni suala alilolizungumzia Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, ni kuhusu chelezo Ziwa Nyasa. Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, aliomba Serikali ijenge chelezo Ziwa Nyasa badala ya kutumia chelezo cha *Monkey bay* kilichoko kule Malawi.

Mheshimiwa Spika, labda nichukue nafasi hii Mheshimiwa Spika niseme kwamba kama atakumbuka Mheshimiwa Luoga mwaka 1974 Wizara ya Ujenzi wakati ule zilikuwa hizi ni Wizara mbili Mawasiliano na Uchukuzi na Ujenzi zilikuwa pamoja ilikuwa na nia ya kujenga chelezo pale *Itungi Port.*

Lakini ujenzi huo ukasitishwa mwaka 1976 baada ya kuona mradi huo haukuwa na manufaa kiuchumi. Lakini tunasema kwa sababu mambo yanabadilika na biashara nazo zinabadilika hili linahitaji kuangaliwa upya na *TPA.* Kwa sasa utaratibu tuliokuwa nao bado tunaendelea kutumia *Monkey bay* kule Malawi kwa sababu tunayo mikataba na ushirikiano ya karibu.

Mheshimiwa Spika, pia nadhani tukumbuke tu kwamba sisi katika Ziwa hili tuna meli mbili tu, unajenga chelezo kwa kutengeneza meli mbili mpaka pale zitakapoharibika, kiuchumi haileti faida sana. Tumeona *cost effective* ni kupeleka Malawi lakini kama haja itajitokeza hapo baadaye ya kufanya hivyo *TPA* haitasita kuliangalia hilo kwa uzito wake.

Pia kulikuwa na wazo la Bandari ya Ndumbi na Mheshimiwa Mbunge alinung'unikia sana kuhusu Bandari ya Ndumbi kwamba ina mawe, ina matatizo mazito.

Mheshimiwa Spika, hapo zamani kweli meli za kampuni hii ya *Marine Service* zilikuwa zinafunga gati pale Ndumbi lakini huduma hizi zikasitishwa baada ya meli zile kupata ajali kama watakumbuka wenzangu walioko maeneo yale *M.V. Songea* ilipata ajali mara mbili mwaka 1991 na mwaka 1992. *M.V. Iringa* ikapata ajali mwaka 1990 na 1991 na zote zilitokea katika eneo hilo hilo moja. Hivyo kwa kufuatana na ajali hizo na baada ya kuangalia utafiti kidogo waliona kwamba maeneo yale si salama kuegesha meli kwa hivyo tukasitisha huduma zile pale mpaka pale sehemu mbadala ya usalama ya karibu na Ndumbi itakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na wazo la upimaji wa maeneo ya bandari, sisi tunasema ni wazo jema na tuna hakika *TPA* itazingatia hali hii kutokana na uwezo wake hata kama watafanya kwa awamu lakini ni muhimu kupima maeneo na kumiliki na kuona kwamba haya ndiyo maeneo ya bandari.

Mheshimiwa Spika, lingine lilitolewa wazo la ujenzi wa bandari moja kati ya bandari za Ukanda wa Ziwa Tanganyika. Lazima niseme kidogo kwamba mimi nilipata bahati na niliamua kwa makusudi kusema ukweli halali kusafiri kutoka Kigoma kwenda Kasanga na nilichukua siku mbili kwenye meli. Nia yangu ilikuwa ni kuona kwa macho yangu hali halisi ya usafiri na uchukuzi katika Ukanda huu na kwa kweli nilijionea mengi na ndiyo maana tukashauriana na Mheshimiwa Waziri tukaona hoja ya kuziboresha bandari zetu na kama mtakubaliana nasi tumeanza kujenga bandari za Maziwa.

Mheshimiwa Spika, hapo nyuma tulikuwa hatupati hata senti tano za kutengeneza bandari hizi, tunashukuru Serikali kwa kutufikiria hivyo ni wakati muafaka kufikiria tutaendelea kufanya hivyo na pale penye uwezekano katika ule Ukanda kuna maeneo au vituo kama kumi na nane nadhani, sasa Mheshimiwa mmoja alitoa wazo kwamba angalau katikati pale pajengwe kituo kimoja.

Tunasema *TPA* italiangalia hilo na hivi sasa nia ni kujenga Karema kama tulivyoahidi na tutaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lilitolewa wazo la *hydrographic survey, navigationally charts* na hata Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, amesemea hilo na mimi nakubaliana nae kwamba tunahitaji kufanya *survey* ya Maziwa yetu. Sisi tumeanza, tunayo miradi kupitia *East African Community* ambayo imegawanyika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza tunafanya *survey* na *mapping* na mradi huu utahusu Ziwa lote, ambayo hatima ya *survey* ni kutengeneza *charts* zitatumiwa kwa ajili ya usalama wa vyombo vinavyosafiri katika Ziwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili ni *Navigation Aids* yaani vile vifaa vya kuongozea, mradi huu utahusu kujenga minara na kuweka taa za kuongozea meli katika Ziwa Victoria na mradi wa tatu ni mradi wa uboreshaji wa bandari na mradi huu unahusu kukarabati bandari kubwa zilizoko katika Ziwa Victoria nchini Tanzania, Kenya na Uganda na mradi huu utahusu kutoa vifaa vya kupakulia mizigo na huduma nyingine za kibandari. Nasema tumeanza kwa *Lake Victoria* na tutaendelea kwa Maziwa mengine yaliyobakia hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, naamini mimi katika miradi hii niliyoisema sasa *TPA* itapata nafasi nzuri ya kufuatilia utekelezaji wake na kwa kushirikiana na *IMO* tutaendelea kufanya tathmini katika Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika kama tulivyofanya kwa Ziwa Victoria na pale fedha zitakapopatikana shughuli hizi zitaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na wazo lililotolewa na Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, kwamba kuna mrundikano wa meli mbovu pale bandarini na makontena yamejaa sana na magari sisi tumeangalia pale *boat,* meli tuliyonayo ni moja tu ya *M.V. Zahara* tumejitahidi kuondoa meli zote zilizokuwepo pale, nyingine zimekatwa wamechukua mabaki na nyingine zimeondoshwa kabisa tumebakiwa na *M.V. Zahara* na hii hatukuweza kuiondosha kwa sababu inautata wa kisheria lakini tunategemea mapema mwakani sheria ikimaliza mkondo wake na hii meli nayo pia itaondoka. Mheshimiwa tunakushukuru kwa *concern* yako hiyo.

Mheshimiwa Spika, magari yaliyoko bandarini yana subiri wenyewe kuyachukua na yale ambayo wenyewe wameshindwa kuyachukua upo utaratibu wa *TRA* kuyapiga mnada, kwa hiyo, yale unayoyaona pale mengi tu yanasubiri forodha kuchukua hatua zinazohusika kwa sababu huwezi tu kupiga mnada unawapa watu muda maalum wa kutafuta hizo fedha za kulipia magari yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakishindwa kuyalipia magari yao huwa yanapigwa mnada. Yakitoka kwetu huwa hayako kwetu tena bandarini yako kwenye mikono ya forodha. Kwa hiyo, tutaendelea tu kuwasiliana na wenzetu wanaohusika kuona kwamba yale magari yaliyokaa muda mrefu pale yanachukuliwa hatua zinazofaa.

Mheshimiwa Spika, lingine kusema ukweli halali pale kila siku tutaona magari yanaendelea kuwepo kwa sababu meli zinakuja, zinateremsha magari, wengine wanachukua magari yao na mengine yanakuja. Kwa hiyo, bandarini kutakuwepo tu na mrundikano wa magari kwa sababu ni mahali ambapo panashusha na kupokea bidhaa hizi za magari ya kwetu Tanzania na ya nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kontena zilizoko bandarini ni za mizigo ya wateja nyingine ziko pale kusubiri kupakiwa katika meli na kurejeshwa zilikotoka lakini mengine yapo yakiwa na mizigo yanasubiri kusafirishwa nje ya nchi lakini nakiri kwamba makontena yote yaliyoko pale yamehifadhiwa vizuri na hadhi ya mandhari ya katika *Container Terminal* ni nzuri. Nadhani Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, ulipata nafasi ya kutembelea bandarini na ukaona hali halisi.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kulichangia lile limezungumziwa na suala la urasimu bandarini. Kama tunavyojua bandari ya Dar es Salaam inatumika na wadau wengi na wateja wengi ukiacha mamlaka ya bandari peke yake wapo watu wa *TRA,* wa *custom,* kuna *clearing and forwarding agents,* kuna wenye meli, kuna *inspectors,* kuna watu wa afya, wa kilimo, wa usalama na kuna masuala ya reli.

Kwa hiyo, watumiaji wa bandari ya Dar es Salaam si bandari peke yake kwa hivyo urasimu utazorotesha shughuli zote za bandari mmoja au iwapo kama hakufanya kazi zake vizuri kunafanya na shughuli nyingine vile vile zisiwe nzuri zaidi.

Ufanisi wa bandari utapatikana tu pale vyombo vyote nilivyovitaja vitashirikiana kwa pamoja kurahisisha utoaji wa huduma zao. Hivi sasa tayari mamlaka ya bandari na *TRA* wanapeana taarifa za malipo ya ushuru kwa kutumia mtandao wa *computer* ili kuondoa urasimu suala ambalo limezungumziwa na kila mwenye kuchelewesha kutoa mizigo bandarini tumeweka alipe gharama za *storage charges* mtatusamehe sana lakini hii tumeiweka kwa makusudi kabisa mtu asijisahau akafanya bandari ndiyo *warehouse* yake na hayo yalikuwa yanafanyika mtu anaiacha mizigo yake kwa miaka miwili, mitatu, bila kuilizia, sasa tunafanya nini kama hatukumtoza *demurrage charges?*

Mheshimiwa Spika, tunamtoza tozo ajue kwamba pale ni mahali na kupitisha tu mizigo si *storage* ya kuweka mizigo yake. Tunaomba radhi kama kuna tuliyemkwaza, lakini hata katika hili kuna nafuu Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, unaweza kuomba ukapunguziwa *demurrage charges from 25 to 50 to 75%* ukieleza maelezo yako na yakakubalika vizuri.

Nakuomba uitumie nafasi hiyo na watu wa bandari watakusikiliza. Lakini isitoshe katika masuala haya ya bandari kuna kuchelewa kwa *Bill of Landing* kutoka kwa wenye meli utakuta mizigo imefika lakini *Bill of Landing* hazijafika kwa hiyo wale wanao *clear* mizigo wanachelewa ku-*clear* mizigo yao, lakini sisi bandari tunahakikisha mizigo yako

inapokuja taratibu za bandari *within three days* tunakuwa tumemaliza. Linalobaki inakuwa ni vyombo vingine ambavyo vinafuata taratibu ambazo wameziweka.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kulichangia ni suala la bandari ya Lindi, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, amelizungumzia hili na kwa muda mrefu kuhusu kujaa kwa mchanga katika bandari ya Lindi kama mtakumbuka mwaka 1999 tulichimba pale kadri ya tulivyoweza kwa shilingi bilioni 1.9 na kuondoa mchanga, lakini ulijaa tena. Lakini tuseme sasa tumetafuta mtaalam mwelekezi wa kufanya utafiti na tunaahidi mtaalam huyu atakapokuja tutampa mawazo ya Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mawazo ya Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tumezuia sehemu ambayo haipaswi kuzuia.

Kwa hiyo, hayo mawazo tutampa na tutamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mtaalam atakapokwenda kule atamwona na watapata maelekezo ya kufanya shughuli zao kwa ushirikiano wa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kulisema ni utaratibu wa kiusalama unaohusu bandari zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, imekuwa ikisimamia udhibiti wa usalama wa usafiri wa majini, meli na bandari.

Aidha, katika kutekeleza wajibu wa nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa mwanachama wa *IMO* imekwisha ridhia marekebisho ya mikataba mbalimbali ya Kimataifa yanayohusu usalama na usafiri wa majini naomba niwashukuru kwa sababu ni Bunge hili tu mwanzoni tumepitisha Miswada mingi tu.

Mheshimiwa Spika, tuna Muswada unaitwa *Solar Convention* ambayo imeanzishwa, *International Ship and Port Received Cord* kwa ajili ya kutoa taratibu na mwongozo wa namna ya nchi kuweza kulinda usalama wa meli na bandari na haya sisi tunayachukulia *seriously* hasa katika masuala haya ambayo yalijitokeza tarehe 11 Septemba, kama mtakumbuka na mkitazama bandari na viwanja vya ndege tunakwenda sambamba.

Mheshimiwa Spika, viwanja vya ndege sasa huwezi kupita pale bila kupita kwenye *screen* ukachekiwa na mizigo yako vizuri tunataka na sisi huku bandarini tufikie hatua hiyo. Aidha, kumeundwa Kamati inayoitwa *The National Maritime Security Committee* yenye wajumbe kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Uhamiaji, Wizara ya Fedha yaani *customs, KMKM,* Mamlaka zinazo husika na bandari, Wizara zinazohusika na usafirishaji, ulinzi na Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii ni pamoja na kuishauri Serikali kuhusu masuala yote ya usalama wa majini. Kutoa ushauri wa kiwango cha usalama kinachofaa kutumika bandarini na kuratibu taarifa za usalama zinahusu shughuli za majini nchini kote na ili kutekeleza taratibu na miongozo ya kanuni hiyo wahusika wakuu wa utendaji ni *Port Security Officer, Facility Security Officer* na *Ship Security Officer* wa kila bandari.

Mheshimiwa Spika, sisi tutaendelea kudumisha usalama wa bandari zetu tukishirikiana na ninyi Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni yale ambayo ameyachangia Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, tunakubaliana nawe kwamba tunahitaji kuboresha bandari zetu za Tanga na Mtwara kwa kuzipatia vifaa vinavyofaa kama vile walivyonavyo Dar es Salaam naamini *TPA* itazingatia hilo na umesema lazima tujiandae katika ulimwengu huu wa ushindani na ni kweli tusipoangalia tunaweza tukajikuta na sisi hatuwezi kufanya biashara. Biashara ya bandari ni biashara ya ushindani na napenda niwashukuru wafanyakazi wa bandari ya Dar es Salaam kwa sababu mpaka sasa bandari ya Dar es Salaam tunafanya vizuri sana lakini hilo lisiwafanye wao walegeze kamba.

Mheshimiwa Spika, tuepuke tusiwe soko kwa nchi nyingine, mimi nasema ni wazo zuri sisi kama tutaweza ku-*produce* na tukasafirisha basi tufanye hivyo ili ni jukumu letu sote. Nakubaliana nawe Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, kwamba tuna *stand a good chance* kuhudumia *Land Lock Countries* na mara nyingi Mheshimiwa Ally Karavina, alikuwa analizungumzia hili suala la uchumi wa kijiografia na mimi nasema lina umuhimu wake na sasa ndiyo wakati kabisa wa kusisitiza uchumi wa jiografia ni lazima tufungue za Tanzania pembe zote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima tufungue sehemu nyingi tu ambazo tunaweza kupitishia mizigo yetu kwa urahisi zaidi na lazima ushindani uwe ndani ya damu yetu. Suala la kuipa uwezo *TPA* kukopa fedha mimi nasema Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, lipo katika sheria ukiangalia sheria kifungu namba 4 (c) cha Muswada kama ilivyo kwenye jedwali la marekebisho utakuta hili kwamba mamlaka hii imepewa kisheria nafasi hiyo.

Nyingine ni kuongeza mapato na ufanisi, iwepo mipango ya maendeleo, ujenzi wa bandari mpya mwambani, *master plan* ipo mbioni kutengenezwa, tunahamu sana kuona tunaweza kutekeleza hilo na nia ni kwamba kama tutaweza kuunganisha reli ya Arusha - Musoma na tukaboresha tukaweka bandari ya mwambani tutaweza ku-*capture* uchumi wa jiografia ambao anauzumzia Mheshimiwa Ally Karavina.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Benedict Losurutia, alizungumzia bandari ni lango kuu la uchumi sasa tunakodisha vitengo kwa watu binafsi ombi mamlaka mpya kama Serikali haikusaidia chombo hiki itashindwa kutekeleza wajibu wake mimi nakubalinana nae na ndiyo maana tukaweka kifungu kwamba tupate hela tutakuja hapa Bungeni kuwaomba mtupe fedha tuboreshe hizi huduma na imo katika sheria. *(Makofi)*

Bandari ni suala la Muungano lakini naomba hili nimwachie mwenyewe Mheshimiwa Waziri atalizungumza. Katika kubinafsisha vitengo vya bandari ni vyema kuchukua ushauri wa wataalam, Mheshimiwa Benedict Losurutia, hili tutalichukua na wanaohusika katika ubinafsishaji wamesikia wazo hilo. Kuhusu wafanyakazi kutoka *THA* kwenda *TPA* Mheshimiwa Waziri atalizungumzia hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache naomba nichukue nafasi hii niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa dhati kabisa kwa ushirikiano mzuri ambao wanaipa Wizara yangu na mimi binafsi unaotufanya kufanya kazi zetu kwa bidii na ufanisi zaidi, tunawahakikishia kwamba tutaendelea kuwa nao na kutekeleza wajibu wetu kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba yangu mwenyewe lakini kwa niaba ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwanza kabisa kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu ambayo imetusimamia kwa maana ya kusimamia utekelezaji na vile vile imepitia, imefanya mapitio ya Miswada mbalimbali na Maazimio na imekuwa ni kama mwanga au dira kwa kazi zetu za kila siku, imetoa ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishukuru tena Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue na kuwashukuru kwa dhati kabisa wale waliochangia.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue na kuwashukuru kwa dhati kabisa wale waliochangia na kwa hakika wote wameunga mkono hoja iliyo mbele yetu.

Waliochangia kwa maandishi pamoja na kwa kusema hapa Bungeni katika ukumbi ni kumi na sita, kumi na tatu wamechangia kwa kusema na watatu wamechangia kwa maandishi. Kwa ruhusa yako naomba niwataje waliochangia na nitaanza na waliochangia kwa kusema hapa Bungeni. Nao si wengine bali ni Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, ambaye alisema kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Profesa Damian Mwaga, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na mwisho wala si kwa umuhimu Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Omar Chubi. Narudia tena kuwashukuru wote kwa michango yao ya kina, mizuri na itatusaidia sana katika utekelezaji wa sheria kwa matumaini kwamba itapitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo ya utangulizi naomba kutumia fursa hii kutoa majumuisho ya masuala ya kijumla ya kisera ambayo yanahitaji ufafanuzi zaidi kwa

sababu Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Naibu Waziri amechangia kwa undani sana masuala mengi. Amefafanua hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge kwa ufasaha na umahiri kama tulivyozoea kumsikia akichangia hoja mbalimbali. Kwa hiyo, mimi namshukuru sana kwa sababu wakati mwingine nasema bila ya Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, sijui kazi yangu ingekuwaje? Namshukuru sana tena na tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita katika maeneo manne yafuatayo. Moja ni suala la Bandari zisizo na mvuto wa kibiashara, tunafanya nini au tunasema nini kuhusu suala hili. La pili ni suala la usalama katika maeneo ya Mwambao na katika Maziwa Makuu, suala la usalama limezungumziwa kwa kina sana. Tatu, ni suala la hatma ya Mamlaka ya Bandari na vile vile wafanyakazi wa Kampuni wa Huduma za Meli na mwisho nitalizungumzia suala alilolozungumzia kwa ufasaha na kwa kina na kwa umahiri tuliomzoea vile vile kumsikia Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, nalo mimi nitaliweka vizuri tu kwamba linahusu Bandari kuimarisha Muungano.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kuhusu suala la maeneo mbalimbali ya nchi katika Pwani na vile vile katika Maziwa Makuu maeneo yenye Bandari zisizo na mvuto wa kibiashara. Hapa niseme tu kwamba ni jukumu la Serikali kutoa au kuwezesha kutolewa kwa huduma pale ambapo hakuna mvuto wa kibiashara na pale ambapo njia pekee ya uchukuzi ni hiyo ambayo inabidi tuiendeleze.

Hili ni suala ambalo katika uchukuzi kwa kitaaluma tunaliita ni *(Public Service Obligation)* wajibu wa Serikali kutoa huduma kwa umma. Kwa sababu sehemu zingine na sehemu nyingi katika Ziwa Nyasa kwa mfano hakuna njia nyingine yoyote ambayo inaweza kuwafikia wananchi au wananchi wanaweza kufika sehemu nyingine na ni wajibu wa Serikali kama hakuna Mwekezaji ni wajibu wa Serikali kuwachukua wananchi kutoka kule au kuwezesha kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, nimetoka Ufaransa juzi juzi nilikuwa nafuatilia masuala ya ubinafsishaji wa huduma za reli katika Umoja wa Ulaya. Pale Ufaransa nilikuwa na mazungumzo na Waziri mwenzangu Waziri wa Uchukuzi. Alielelezea suala hili la ufanisi katika maendeleo ya reli Ufaransa akasema kwa kweli reli Ufaransa hakuna biashara kabisa, ni hasara tupu. Lakini anasema wananchi wanaitaka reli na hilo tu kisiasa linawafanya Wafaransa waiendeleze reli mpaka imekuwa moja ya reli bora katika Ulaya ya Magharibi. Kwa hiyo, hilo ni suala la msingi sana. Hata kwetu hapa kama ni njia moja tu inayohitajika au iliyopo ni kutumia reli au kutumia njia ya maji ili kuweza kuwachukua au kuwasafirisha wananchi na bidhaa zao basi ni jukumu la Serikali kufanya hivyo. Ni siasa lakini vile vile ni jukumu na wajibu.

Kwa hiyo, naahidi kwamba tutafanya hivyo kama Serikali. Tumeliweka vizuri katika kifungu kipya cha 71 katika Muswada huu. Serikali inaweza kutekeleza wajibu huo kwa kutoa fedha kufidia hasara, inaweza kupunguza tozo au kodi mbalimbali kuwezesha uchukuzi, inaweza kununua au kusaidia ununuzi wa vyombo vya usafiri. Vile vile inaweza kuingia Mikataba ya utoaji huduma na watu binafsi au na sekta binafsi katika mtindo tunaoita ama joint venture au vile vile *Public Private Partnership (PPP).*

Kwa hiyo, ni maeneo mengi ambayo tunaweza tukashirikiana na *Private Sector* lakini tukawawezesha kutokana na fedha za Serikali ili waweze wakatoa huduma au Serikali moja kwa moja itoe huduma. Kwa hiyo, hili tutalizingatia. Lakini vile vile kwa kuendeleza Bandari na kujenga gati katika maeneo ambayo haya mvuto wa kibiashara basi katika kufanya hivyo tunawawezesha wananchi kutekeleza majukumu yao ya kujiendeleza na huu ni wajibu wa Serikali. Ni wajibu wa msingi kabisa kwa Serikali yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, nimegusia reli na nimesema vile vile kwa upande wa Ziwa Nyasa hili ni suala muhimu sana kwa sababu kwa kweli kama nilivyosema hakuna njia nyingine katika Mwambao wa Ziwa Nyasa wa kuwasafirisha wananchi isipokuwa kutumia uchukuzi wa majini. Itatuchukua muda mrefu kupata mwekezaji katika maeneo yale na Serikali kwa upande wa Ziwa Tanganyika na upande wa Ziwa Nyasa tutaendelea kutoa msaada. Kwa kweli si msaada ila tutaendelea kuwajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, amezungumzia kuhusu anachofikiri inaweza kuwa ukandamizaji wa Waziri anapotangaza kwamba eneo hili ni la Bandari au eneo si la Bandari au Mamlaka makubwa aliyonayo. Waziri haamki akatangaza tu kwamba leo mahali fulani itakuwa Bandari pamoja na kwamba ana Mamlaka hayo, hapana. Inatokana na mlolongo au mchakato unaopelekea kutoa tamko hilo. Kwanza itatokana na hali ya kibiashara, mahitaji ya uchukuzi na ushauri wa kitaalam, lakini vile vile itatokana na nia ya wananchi wenyewe wa maeneo hayo kupitia vyombo vyao halali, vikao halali na maazimio halali kutaka kuwepo Bandari au itamkwe kwamba kunakuwa na Bandari au kutaka kufutwa kwa Bandari. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, kwamba tutalizingatia suala hili na si rahisi kama inavyofikiriwa kwamba Waziri anaweza akaamka siku moja akatangaza kuwepo kwa Bandari au kutokuwepo kwa Bandari.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kwa kupitia tu suala muhimu lakini ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri ameligusia nalo ni kwamba kwa mara ya kwanza niseme katika historia ya Tanzania suala la kutumia jiografia tuliyonayo kwa manufaa ya nchi yetu, jiografia ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia bahati kubwa linawekwa katika sheria, kama ni suala la msingi ni jambo kubwa sana na litakuwa ni mwongozo mkubwa katika utekelezaji wa kuendeleza uchumi wa nchi lakini vile vile kuendeleza uchukuzi. Kwa maana hii nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwa sababu hili suala tumelisukuma kwa pamoja mpaka sasa limeweza kuwekwa katika sheria, kwa hiyo litazingatiwa.

Vile vile Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, amelizungumzia, Mheshimiwa Benedict Losurutia, amelizungumzia, amelisisitizia, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, nawashukuru sana kwa kulisisitizia suala hilo. *(Makofi)*

Narudia kusema kwamba kwa kweli Singapore, Hong Kong ni visiwa vidogo kwa kweli ni mawe tu, lakini vina jiografia nzuri, wameweza kuitumia jiografia ile kubadilisha hali ya uchumi na baadaye kuingia katika hali ya teknolojia ya kisasa

kutokana na msingi imara wa kuwa na hali nzuri ya kijiografia. Hakuna sababu kwa nini wananchi wa Tanzania waendelee kusisitiza na kusema uchumi au uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania ni kilimo. Kwa kweli jiografia tumeikalia hatuitumii, tunaweza tukabadilisha ili tukisaidie kilimo kimebeba mzigo wa uchumi huu sasa ni wakati ambapo hata uchukuzi nao uchangie. Hili limetamkwa bayana katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la usalama katika maeneo ya Mwambao na Maziwa Makuu. Suala hili alilizungumzia Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, kwa kirefu sana lakini vile vile Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na Mheshimiwa Edward Ndeka na wengine waliochangia. Moja ya majukumu makubwa ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari itakuwa ni ulinzi na usalama wa Bandari zetu. Hilo ni jukumu la Serikali kupitia kwa Mamlaka hiyo. Hilo hatuwezi kulikwepa wala sio jukumu la Wawekezaji. Sasa kuna mambo ya ndani ya Mamlaka yenyewe. Itajizatiti kujiweka sawa ili iweze ikasimamia ulinzi na usalama. Lakini vile vile kuna mambo ya Kitaifa kwa sababu Taasisi nyingi zinahusika katika Bandari na hili litakuwa jukumu la Mamlaka hii kuweza kuratibu shughuli za usalama katika Bandari zetu. Taasisi nyingine zinazohusika hata hivi sasa katika ulinzi wa bandari yetu ni kama Taasisi na Asasi na Wizara kama vile Mambo ya Ndani kwa maana ya Polisi, Usalama wa Taifa, Mamlaka ya Mapato, Idara ya Uvuvi na siku hizi vile vile Idara ya Mazingira, Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa kwa maana Kikosi cha Wanamaji na vile vile Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo *(KMKM)* Zanzibar.

Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, alizungumzia vile vile je, tunawapekua au tunafanya upekuzi kwa hawa Wawekezaji wanapokuja kwenye Bandari zetu? Niseme tu kwamba tunafanya ila siwezi kusema tunafanyaje kwa sababu hili hapa si mahali pake nitakuwa kama natoa siri za upekuzi unafanywa namna gani. Lakini kwa yale ambayo tunaweza tukayapata hivi hivi kutoka kwa wenzetu kwa kuwaliza kuhusu hayo tunapata moja kwa moja na mengine tunatumia vyombo vyetu vya usalama kuweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, nielezee zaidi tunafanya nini kulinda Bandari zetu. Baada ya vitendo vya Ugaidi vilivyotokea Marekani tarehe 11 Septemba, 2001 ambapo vyombo vya uchukuzi kwa mara ya kwanza vilitumika kama silaha za maangamizi basi ilifuatiwa na tukio lililotokea kule Yemen ambapo meli zilishambuliwa kwa kigaidi mwaka 2002.

Sasa kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Usalama wa Uchukuzi Majini *(International Maritime Organisation)* tulikubaliana baada ya hayo matukio mawili tulipokutana London kwamba tuanzishe taratibu za usalama wa Bandari, meli pamoja na wanaofanya kazi katika maeneo hayo. Kwa hiyo, kupitia hiyo *IMO* tumeanzisha kitu kinachoitwa *The International Ship and Port Facilities Code or (ISPSC).*

Mheshimiwa Spika, *ISPSC* inatokana na Mkataba wa Usalama Majini yaani *The International Convention on Safety and Life at Sea (Solas)* wa mwaka 1974 ambao Bunge lako Tukufu liliuridhia. Sasa taratibu hizo za *ISPSC* zina lengo la kudhibiti ulinzi na usalama wa meli na Bandari. Ilibidi masharti hayo tuwe tumeyatekeleza ilipofika tarehe 1 Julai, 2004. Sisi kwa upande wetu tumetekeleza kikamilifu kwa sababu ilibidi tuyazingatie hayo masuala katika sheria zetu na tumeyazingatia katika *Merchant*

*Shipping Act,* kwa hiyo, hilo tumefanya. Halafu baada ya hapo tumetunga kanuni maalum zinazozingatia usalama wa Bandari na meli na wafanyakazi katika maeneo hayo yaani tumetunga *ISPSC Code Regulations.* Kama Waziri mwenye dhamana ya uchukuzi tayari nimezitangaza katika Gazeti la Serikali na zimetolewa kama kanuni, kwa hiyo zina nguvu ya kisheria.

Halafu tuna Kamati ya Usalama wa Usafiri Majini, Kamati ya Kitaifa yaani inaunganisha Zanzibar pamoja na Tanzania Bara. Kamati hii ina wajumbe wafuatao Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa maana ya Uhamiaji na Polisi, Wizara ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Ofisi ya Rais kwa maana ya Usalama wa Taifa, *KMKM,* Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Mamlaka ya Bandari Tanzania, Mamlaka ya Bandari Zanzibar, Chama cha Wataalamu wa Uchukuzi Majini na Msajili wa Meli ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati.

Kwa hiyo, utaona kwa maana ya usalama hili suala tumelichukulia Kitaifa, kwa hiyo, halina tatizo ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, kwamba pamoja na mambo mengine tunaamini kwamba waasisi wa Muungano walilifikiria suala la usalama walipoweka Bandari liwe suala la Kimuungano na sisi tumelichukulia kwa uzito huo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la wafanyakazi. Nianze kwa kuwashukuru kwa dhati kabisa wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari na wafanyakazi wa Kampuni wa Huduma za Meli Tanzania *(The Marine Services Company)* na vile vile wa *Tanzania Harbours Authority* wamefanya kazi nzuri sana katika miaka yote hii ya kusaidia uchumi. Wamekuwa wavumilivu na vile vile tumesaidiana sana katika kuendeleza uchukuzi katika nchi hii. Naomba kuweka kwenye rekodi shukrani za Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa maana hiyo shukrani za Serikali kwa wafanyakazi.

Sasa kuhusu nini kitatokea, naomba nitaje misingi, maana yake mambo lazima tuanzie kwenye misingi. Serikali kwa maana ya wafanyakazi tumejikita katika misingi miwili. Moja ni kuendeleza ajira kwa kadri inavyowezekana na sio kufuta ajira na hili ndilo kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilipigia kelele mara kwa mara kwamba kurekebisha Mashirika na vile vile kuuza Mashirika au kubinafsisha haina maana kwamba tuwafukuze wafanyakazi au wafanyakazi wakose ajira. Sasa hili tumeliona na tumelisikia na katika Muswada huu tunatekeleza matakwa ya Waheshimiwa Wabunge kwamba tungependa kuendeleza ajira wala sio kufuta ajira. *(Makofi)*

Msingi wa pili ni kwamba pale ambapo ajira inasitishwa basi wafanyakazi walipwe haki zao kikamilifu, kwa haraka, bila usumbufu. Bahati nzuri kwa maana ya Muswada huu na vile vile kwa maana ya Mamlaka ya Bandari Tanzania hili hatuna tatizo nalo kwa sababu kama nilivyowasifia wamejijengea uwezo wa sisi kutekeleza hili suala la kuwalipa kikamilifu, haraka na bila usumbufu. Kwa hiyo hili halitakuwa ni tatizo kabisa kama ilivyokuwa tatizo katika Mashirika mengine.

Mheshimiwa Spika, sasa tumetekelezaje hii misingi. Waheshimiwa Wabunge walituruhusu tutumie misingi hii kufanya ajira ziwe endelevu katika Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano. Tumetumia misingi hii na ajira zimekuwa endelevu na wala haikuwa na maana kwamba tusitishe ajira, walipwe halafu waanze upya ajira, hapana na wamefurahi sana kwani kila mtu alikuwa na wasi wasi ajira itakuwaje. Tulipotangaza kwamba ajira ni endelevu wameshukuru sana.

Kwa hiyo, kwa msingi ule tusisitishe ajira wala tusichochee kusitisha ajira kwa watu kupokea kiinua mgongo halafu waombe ajira. Niseme uzoefu kwa wale waliochukua kiinua mgongo na baadaye wakamaliza ajira zao katika Shirika la Reli Tanzania wengine leo hii wanatafuta kazi wangependa kurudi tena. Kwa hiyo, kiinua mgongo hata upate shilingi milioni 100 si sawa sawa na ajira hata siku moja. *(Makofi)*

Wengine tunasikia baada ya kupata kiinua mgongo walichukua teksi kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya, sasa haya ni matumizi mengine. Lakini ajira ni muhimu zaidi kuliko kiinua mgongo, nilitaka kusisitiza hilo. Tumefanya hivyo kwa maana ya baada ya kupokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kuhusu Mamlaka ya Udhibiti au Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga na vile vile kwa maana ya Udhibiti wa Shehena waliokuwa wafanyakazi katika *TCFB* ajira yao inakuwa endelevu sasa na wao wameshukuru sana kuingia katika *SUMATRA.*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine mmezungumzia kuhusu *SUMATRA* na Mashirika mengine haya kuchelewa kuanzishwa. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kweli *SUMATRA* sasa imeanza rasmi baada ya uteuzi wa Mwenyekiti Ndugu Peter Bakilana ambaye nafikiri yupo hapa ananisikiliza. Ni mzoefu wa siku nyingi sana, amechangia sana katika maendeleo ya nchi hii na vile vile kuanzia jana uteuzi wa Bwana Israel Zakayo Sekirasa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa *SUMATRA,* nachukua nafasi hii kumpongeza sana Bwana Sekirasa kwa uteuzi huo. *(Makofi)*

Kwa maana ya sheria hii itakapoanza kufanya kazi ajira itaendelea hasa wafanyakazi wa Bandari wa sasa waliopo. Kwa hiyo, hawatasitishwa ajira. Mwajiri ni Serikali kwa sasa na vile vile hata katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. Kwa hiyo, hakuna mwajiri mpya isipokuwa mwajiri amebadilisha tu majina ya chombo chake hicho. Kwa hiyo, sio kwamba kuna ajira mpya, hapana, wanaendelea na ajira ile ile na mwajiri ni yule yule, Serikali. Kwa hiyo, ile ya kusema tusitishe wapate hela zao, wakipata hakuna uhakika kwamba wataajiriwa itakuwa ndio wamesema kwaheri.

Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge tusiwachochee kabisa, wale ambao wanahitajika na ajira yao iwe endelevu, wapate kiinua mgongo, wakipata kiinua mgongo maana yake ni kwaheri. Itabidi tutangaze kazi zote upya. Itakuwa tatizo kubwa. Tutakuwa hatujawafanyia haki wafanyakazi.

Kwa kuwa ukodishaji utachukua muda basi ajira inakuwa endelevu lakini pale ambapo vitengo vitakodishwa basi mfanyakazi atakuwa na hiari ya kuendelea au kustaafu. Hatalazimishwa kuingia mkataba na huyo mwajiri mpya ambaye sio Serikali na kwa maana hiyo sio Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. Wafanyakazi katika vitengo

hivyo watalipwa mafao yao yote kabla hawajaingia ajira mpya na kabla hawajastaafu. Hii yote imewezekana kwa sababu ya kazi nzuri wafanyakazi wenyewe wameifanya kwa kuzalisha na kufanya Mamlaka ya Bandari iendeshwe kwa faida.

Kwa hiyo, mambo hapa tumeyaweka safi kabisa na tumezingatia kabisa matakwa ya sheria lakini vile vile sheria za ajira lakini vile vile matakwa ya Waheshimiwa Wabunge na uzoefu tulioupata wa siku nyingi. Limekuwepo suala la kwamba aah, sasa fedha labda zitapoteza thamani, lakini nimelieleza kwamba unapozungumzia ajira inayoendelea suala la fedha kupoteza thamani halipo kwa sababu mategemeo yetu ni kwamba uchumi unakua mishahara inapanda kwa hiyo hili suala la thamani ya fedha linachukuliwa katika mipangilio yote ya kupanda mishahara na mchango wa mwajiri kwa maana hii Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa mfanyakazi.

Kwa hiyo, hili suala limeshajiweka sawa. Mashirika yetu haya ya *PPF* na *NSSF* yanafanya kazi nzuri yanawekeza katika maeneo mazuri yote hii ni kulinda michango ya wafanyakazi. Kwa hiyo, suala lile limezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nizungumzie suala muhimu alilolizungumzia Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, mimi nitasema Bandari kuimarisha Muungano nitaliweka *positively.* Labda nianze na lile aliloanzia yeye kuzungumza lilikuwa ni, au amelizungumzia mwishoni lakini nitaanza nalo, taratibu za kuzuia meli ambayo inadaiwa. Amewatetea sana hao wawekezaji kwa matumaini kwamba kila mwekezaji ana nia njema lakini katika michango yenu mmeshazungumza kwamba Mwekezaji ni binadamu tu, wakati mwingine hana nia njema. Katika suala la wenye meli tuna tatizo na hii ni dunia nzima. Meli ikija bandarini mwenye Bandari anatoa kile kinachoitwa *(interim bill),* bili ya awali kwa makisio kutokana na taarifa alizotoa na inambidi mwenye meli atoe amana *(deposit).* Halafu kutakuwa na kuweka uwiano wa kusahihisha mahesabu ili anapoondoka kama anadaiwa alipe au kama alilipa fedha zaidi basi Mamlaka ya Bandari iweze kumrudishia hizo fedha. Wenye meli wanao wawakilishi wao hapa wana wakala wa meli na wengine wenye meli wana ofisi zao.

Kwa hiyo, suala lolote linalotokana na matatizo ya kulipana ni la kawaida. Lakini si la kawaida kama vile huyu anayedaiwa angekuwa ndani ya nchi. Kwa sababu huyu ukimwachia, uzoefu unaonyesha kwamba ataondoka. Kama ana ruhusa ya kuondoka aseme tutadaiana baadaye na akiondoka nje ya maji ya eneo lako huna kabisa udhibiti juu yake na kama anadaiwa sana atauza hata meli wewe huwezi hata ukajua na gharama zote hizi ambazo inabidi alipe tunakuwa tumezitangaza katika kitabu cha gharama ya huduma za meli, kwa hiyo inaeleweka. Ni mara chache kunatokea na tatizo la mgongano wa kutolipana. Lakini hapa ukiondoa huo uwezo wa kumpa mwenye Bandari kuweza kufanya meli isiondoke basi ni sawa sawa na kumfanya asiwe kabisa na haki, haki yake asiipate kabisa, unampa haki kubwa yule mwenye meli.

Hili suala liko katika mikataba ya biashara ya meli duniani si Tanzania tu, ni sehemu nyingi duniani kwamba mwenye Bandari anaweza akasimamisha meli papo anapoidai. Ni kwa sababu hiyo nasema kwamba akiondoka mwenye meli basi huna udhibiti juu yake. Lakini huyu mwenye meli kama nilivyosema ana wawakilishi wake

lakini vile vile anaweza kwenda kortini ana haki ya kutumia wanasheria na hapo wanasheria watapata fedha kama kawaida yao, kwa hiyo tatizo hakuna.

Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, kama ninavyofahamu kwa uelewa wake na busara zake ni za hali ya juu, hili suala labda asiliendeleze. Isipokuwa angojee tu kwamba watu watakuja kortini na watafika ofisini kwake kuomba haki, awasimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa la mwisho ni zito kidogo, lakini si zito kama kwa sehemu mbili za Muungano zinazoelewa na zenye undugu wa siku nyingi, haijawahi kutuletea matatizo. Najua kama lipo tatizo tuna vikao mbalimbali, kama ni mambo ya kisera, ya kichama, tutayazungumza huko na kuyaweka sawa. Kama ni mambo ya utendaji basi tutakuja hapa tutayazungumza na naamini halitakuwa tatizo kwa Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, kuhusu suala hili la bandari kuwa katika maeneo yaliyoainishwa kama ni maeneo ya Muungano. Ni kweli katika maeneo ya awali kabisa moja ya maeneo yaliyoainishwa ni hili la bandari.

Kwa hiyo, alichozungumza ni kweli kabisa, amelizungumza kwa nia njema na kwa mtazamo mimi nasema wa kuimarisha muungano na namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai.

Katika hili kwa kweli tuna uzoefu wa miaka mingi, tuna uzoefu katika sheria, hapa nazungumzia sheria tu, ya utekelezaji tutakuja kuzungumzia baadaye. Kama nilivyosema kuna vikao vingine vya kuainisha utendaji katika masuala ya Muungano hasa utekelezaji wa sheria. Kwa maana ya kisheria na hapa nasisitiza tena na tena kwamba ni sheria, kwamba ni vema tukatumia uzoefu ambao tunao kupitia kitu kinachofanana au yale yanayofanana na yaliyomo katika sheria ya sasa, Sheria ya Mamlaka ya Bandari ya mwaka 1977 ambayo naamini Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, hana utata na sisi kwa maana hiyo, kwa maeneo mawili tutakubaliana nayo. La msingi tutakubaliana naye na tumesambaza mabadiliko ambayo tungependa yafanyike katika Muswada huu ambayo kwa kiwango kikubwa yanakidhi yale aliyozungumza Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai. Na kwa sababu yanakidhi na ni ya msingi ambayo tunataka kuyabadilisha basi ni mategemeo yetu ni kwamba atakubaliana na sisi ataridhika na vile vile Mheshimiwa Spika, Bunge lako tukufu vile vile litaridhika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi nimalizie hapo kama nilivyoanza kwa kuwashukuru sana Kamati ya Bunge ya Miundombinu na vile vile niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, waliochangia Muswada huu kwa mambo mengi ambayo yamezungumzwa ambayo mengi ni ya kutuasa namna ya kutekeleza sheria pale ambapo wakati ambapo Bunge litapitishwa na Mheshimiwa Rais, atakapotoa idhini yake. Kweli hayo yanatosha kwa sasa, nakushukuru wewe kwa kunivumilia na kunipa nafasi ya kutoa maelezo hayo niliyoyatoa, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa uvumilivu wao kwa kunisikilizwa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu inahitaji uamuzi ni kwamba Muswada unaoitwa *The Port authority Bill* wa mwaka 2004 sasa usomwe mara ya pili.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Ahsante, sasa mimi nimepangiwa kuzungumza na wageni wa Kimataifa niliowatambulisha asubuhi, kwa hiyo, namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anipokee kiti.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Hatua inayofuata, Katibu.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Shughuli za Bandari
### *(The Ports Bill, 2004)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada ni mrefu kidogo kama mlivyouona. Kwa hiyo, nafikiri tusome sehemu zile. Sijui kama linaafikiwa hilo. Katibu tuongoze.

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Sehemu ya 1

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Wakati natoa mchango wangu nilionyesha wasiwasi wangu juu ya kifungu cha 2(1) kwa maana kwamba kilikuwa kinapendekeza kwamba hii sheria itakayopitishwa itumike tu Tanzania Bara. Mheshimiwa Waziri ameleta marekebisho ya pili na kuondoa kifungu cha 2(1) na kuweka kifungu kipya. Mimi kwa mawazo yangu hayo marekebisho yaliyopendekezwa na Serikali hayakidhi ile hoja yangu niliyokuwa nimeitoa kwa sababu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza, ukiangalia kifungu ambacho kinapendekezwa sasa kiletwe badala ya hicho kifungu kitakachofutwa ni marudio ya kifungu kidogo 2, havina tofauti. Kwa hiyo, tutakuwa na vifungu vidogo viwili vya kifungu cha 2 ambavyo vina maana moja. Kwa hiyo, hatujatatua ule mgogoro ambao nilikuwa nafikiria upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi kwa kutumia haki yangu chini ya Kanuni namba ya 70 (4) nimetoa pendekezo ambalo nafikiri litakidhi hofu ambayo baadhi yetu na baadhi ya Watanzania wanayo.

Kimsingi Mheshimiwa Waziri, anakubali kwamba suala la bandari ni suala la Muungano. Ikiwa ni suala la Muungano basi hii sheria itamke waziwazi kwamba hii sheria itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ndiyo utaratibu wa kutunga sheria ulivyo. *(Makofi)*

Lakini ikiwa kama ilivyopendekezwa na Serikali bado ile dhana ya kwamba inatumika pande mbili haijitokezi kwa sababu gani? Ili sheria iliyotungwa na Bunge hili itumike Tanzania Zanzibar ni lazima Baraza la Wawakilishi liiridhie. Sasa hatuwezi kupeleka sheria hii ikaridhiwe na Baraza la Wawakilishi kama hii sheria haitatamka kwamba inatumika kule Zanzibar. *(Makofi)*

Jambo la pili, hatuwezi tukasema tu Bandari ya Zanzibar, Bandari ya Wete, Bandari ya Mkoani, basi iingizwe kwenye nyongeza ile kwa sababu kule Zanzibar kuna mamlaka ya Bandari ya Zanzibar. Sasa tunatunga sheria na tunasema kuwe na Mamlaka ya Bandari ya Tanzania ambayo itakuwa na Mamlaka kwenye Bandari ya Zanzibar na pale pale Zanzibar kuna Mamlaka ya Bandari Zanzibar ambayo Serikali ya Muungano haina mamlaka nayo. Hii sheria iko kimya kabisa juu ya matokeo sasa *consequential development* ambazo zinatokea, maana sasa huyu atakayeteuliwa kuwa Mkuu wa Mamlaka, hii tunayounda akienda Zanzibar akataka kutumia madaraka yake kule atakutana na Mkuu mwingine yule atamwambia hapa ni *out of bounds.*

Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba pendekezo langu kwamba hii sheria ibadilishwe kwa jinsi nilivyotoa pendekezo langu kwenye *schedule (e)* kwamba yaongezeke maneno Tanzania Zanzibar, kile kifungu kibaki kama kilivyokuwa kabla ya Serikali kuleta hii *schedule amendment* na sasa kisomeka: *"This Act shall apply to Sea Ports and Inland Waterways Ports in Mainland Tanzania and Tanzania Zanzibar,"* ili ikubaliwe na Bunge. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, maelezo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maelezo mafupi tu kwenye eneo hili. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Philip Marmo.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelekezo kuhusu kinachoendelea sasa. Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, ametoa hoja ya kufanya mabadiliko katika Muswada na imeungwa mkono. Tumesimama hapa tumeunga mkono sasa kinachoendelea ni nini katika hatua hii sasa, katika hoja aliyotoa Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, hapa mbele yako? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwenye hoja alitaka maelezo na mimi nikampa mtoa maelezo. Sasa baadaye yeye kama hajaridhika ataleta hatua ambayo wewe mwenyewe Mheshimiwa Philip Marmo, unaifikiria. Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kutuongoza barabara, naona kiti kimejaa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema namshukuru Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, kwa jitihada zake za kuboresha Muswada katika hatua hii kwenye kifungu hicho cha 2. Lakini kabla sijaenda mbali napenda nikubaliane kwa kitu kimoja ambacho ni *over site* kwa upande wa uandishi wa Muswada huu kwa upande wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali napenda kusema kwamba hicho kifungu kidogo cha 2 ambacho ndiyo hoja yetu hapa, hakipaswi kuwa katika Muswada huu. Kwa hiyo, napendekeza nilete juu ya mabadiliko kwamba *clause 2 (2)* ifutwe. Sasa ukishafika hapa sasa ndiyo tunarudi kwenye hoja ya Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu wote suala la Bandari ni la Muungano liko kwenye Katiba. Unapotunga sheria kwa suala la Muungano siyo lazima utaje kwamba itatumika pande zote za nchi yetu, ndiyo utaratibu wa sheria zetu. Sheria sasa hivi ya Mamlaka ya Bandari ya mwaka 1977 haitumii hii lugha kwamba itatumika na Zanzibar inasema wazi kwa sababu ni suala la Muungano na ndiyo maana Serikali katika kuleta marekebisho yake tumesema tutambue ukweli kwamba *ports* ni suala la Muungano, halafu twende sasa katika jedwali la pili tuziainishe bandari hizo kwa sababu ziko ndani ya nchi yetu na tunazifahamu hizi bandari na katika utaratibu huo ndiyo tumependekeza marekebisho hayo ambayo yanakidhi kabisa hoja ya kuona kwamba chombo hiki ambacho kinaanzishwa kinakuwa na jukumu la kusimamia kuendesha na kuendeleza hizi bandari za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya uendeshaji tusiyachanganye na matakwa ya Katiba. Muswada huu unataka uzingatie kwamba suala hili linatekelezwa kwa sura. Muswada huu unachukua matakwa ya kuheshimu Katiba kwamba suala hili ni la Muungano na mapendekezo yaliyo mbele yetu kama Kamati yako itakubali kwa maoni yangu kama mshauri wa Serikali kwa masuala ya sheria naamini yanakidhi. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, baada ya maelezo hayo.

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na utaratibu wa kutamka wazi wakati tunapotunga sheria kama itatumika Tanzania Zanzibar.

Kama nilivyosema ili kulipa Baraza la Wawakilishi, nafasi ya kujadili na kuridhia, Baraza la Wawakilishi halichukui tu sheria hivi hivi na kudakia ni pale ambapo Bunge linasema hii sheria itatumika Tanzania Zanzibar ndiyo *Attorney General* wa Zanzibar anaweza akalipeleka mbele ya Baraza la Wawakilishi, akasema kuna sheria imetoka Bungeni sasa itumike. Siyo *presumption* kwamba ni mambo ya Muungano kwa hiyo, yatungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mfano wa *Merchant Shipping Act,* sheria imekaa kimya pia, matokeo yake ni kwamba ile sheria haitumiki Zanzibar na matokeo yake ni kwamba meli za Tanzania ambazo zina *operate* kutoka Zanzibar lazima zipate kibali kutoka Bara wakati ile sheria haitumiki kule. Sasa badala ya kuleta *complication* hiyo, ni kitu gani kinazuia Serikali kusema waziwazi kwa nini ifiche, kwa nini isiseme waziwazi kwamba hii sheria inatumika bara na visiwani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ambayo ametoa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, namshukuru sana kwa kutambua kwamba kile kifungu kidogo cha pili hakikuwa kinahitajika. Nashukuru sana kimeondoka. Lakini mimi siridhiki kufuta kile kifungu kidogo cha kwanza kwa hiyo, naomba nitoe hoja kwamba hoja yangu ya marekebisho Bunge liikubali na lipitishe sheria kwa marekebisho niliyopendekeza. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono na Mbunge mmoja. Je, wanaoafiki hoja hii ijadiliwe kwa mtindo ambao Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, amependekeza wasemi ndiyo, wasioafiki waseme siyo! *(Kicheko)*

Narudia tena, wanaoafiki pendekezo la Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na baada ya maelezo ya *Attorney General* waseme ndiyo, wasioafiki waseme siyo. *(Kicheko)*

Nashindwa kutoa uamuzi, naona kama tunalingana. Sasa uamuzi ni wa Mwenyekiti. Tumsikilize mtoa hoja anasemaje maana yake tumekwenda kama sare hivi. Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, Serikali imesikiliza kwa makini sana yale aliyoyazungumza Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na kimsingi tumekubaliana naye.

Sasa hili suala la kuvutana linatushangaza kidogo, lakini nadhani halitaongeza tija kwa Kamati yako ya Bunge Zima. Kwa maana hiyo, pamoja na kwamba Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na *Hansard* itasema hivyo jana alisema sitapendekeza mabadiliko yoyote, lakini binadamu tunabadilika baada ya saa ishirini na nne.

Kwa hiyo, sisi hilo hatulioni kama lina matatizo sana. Lakini ili kuongeza tija ya Kamati yako tunakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai. *(Makofi)*

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea.

Sehemu ya 2

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa nafasi.

Mimi naongelea kifungu namba 7 ambacho ni *Powers of the Board.* Nina maana kwamba wakati nimechangia nilizungumzia kuhusu mizigo kuwa bandarini zaidi ya muda na nikaomba iundwe Tume kufuatilia hoja yangu kwa sababu hata baadaye niliongea na wale ma-*agent* wa Dar es Salaam wote wanasema vitu vinaitwa *storage* wakati *bill of landing* imekuja kwa wakati.

Kwa hiyo, ili kuweza kuweka sawa, nilikuwa nafikiri kwamba Waziri, angekubaliana na hoja yangu kwamba upelekwe uchunguzi kuangalia ni kitu gani kwa sababu tunapata matatizo ya hasara kubwa. Pia wachunguze na mengine kwa sababu kuna wengine wenye meli kule halafu ni mawakala. Sasa hiyo, ingeweza ikachungaza mengi tu ambayo ingeyapata. Ningefikiri labda Waziri angekubaliana na mimi kwa hilo. Sasa sikuona akijibu hilo vizuri. Sasa kwa sababu hapa kifungu kidogo cha 7 kinaelezea kwamba kuna uwezekano wa kuunda Kamati na vile vile Waziri ana uwezo wa ku-*approve minor alterations* ili kuweza kuleta ufanisi vizuri katika bandari yetu na kuwa na uhakika yale ninayosema nimechunguza zaidi ya muda mrefu. Ahsante.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kwa kuwa na uchungu kwa ubora wa huduma za bandari zetu na angependa Waziri aunde Tume iende ikachunguze.

Ningependa kumhakikishia kwamba kuna Kamati ya Kudumu, ambayo inafanyakazi kwa kuzingatia masuala hayo hayo. Kamati hiyo inaitwa *the Shippers Forum* yaani ni mkutano wa kudumu wa watumiaji wa huduma za bandari. Jukumu lao kubwa ni hilo hilo alilozungumzia Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, limefanikiwa sana kupunguza matatizo mengi yanayojitokeza na napenda kukiri kwamba bado hayajaisha, lakini inafanya kazi nzuri chini ya usimamizi ya bodi inayohusika na udhibiti wa shehena ambayo sasa mamlaka hayo yanahamishiwa katika mamlaka mpya ya *SUMATRA*.

Kwa hiyo, hilo limo katika sheria na vile vile katika utendaji siku hadi siku. Kwa hiyo, tutalizingatia na tutalichukua kama utekelezaji katika mfumo tulionao. Nakushukuru. *(Makofi)*

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Sehemu ya 3

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika sehemu ya tatu kuna suala nilizungumzia juu ya gati ya iliyokuwa ya *Tanzania Fertilizer Company (TFC)* ambayo kiwanda hiki kimefungwa na kimebinafsishwa na kimenunuliwa na mtu binafsi. Lakini nafahamu shughuli za bandari yule aliyenunua kiwanda hahusiki na kukishughulikiwa au kushughulikia gati ile. Sasa swali langu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua nini hatma ya ile gati? Kwa sababu naona kwamba ni sehemu *potential* kabisa kwa shughuli za maendeleo. Kila muda unapopita inazidi ku-*deteriorate* na Serikali ilitumia gharama kubwa sana kujenga. Sasa je, Serikali ina mpango gani au itampa mtu binafsi aiendeleze au tusubiri mpaka hii *authority* itakapopitishwa na kuwa sheria ndiyo itaweza kuamua? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gati ya Tanga ambayo ilikuwa inatumiwa na Kampuni ya Mbolea ningependa kusema ifuatavyo kwamba gati hiyo iko katika hali mbaya na sababu kubwa ni kwamba mbolea ni *chemicals* na *chemicals* hiyo imeathiri sana. Sasa ukichanganya na chumvi chumvi ya maji ya bahari basi hiyo, gati iko katika hali mbaya sana, haiwezi kutumika kwa sasa. Sasa iwapo itabidi itumike kwa matumizi mengine ni sawa sawa na kujenga upya au kuikarabati kwa fedha nyingi. Lakini Mamlaka ambayo tunapendekeza iundwe inaweza ikalichunguza kwa zaidi suala hilo na kuona kama kuna faida au hasara katika kuendeleza hiyo gati ambayo ilikuwa inatumika na Kiwanda cha Mbolea.

Kwa hiyo, hatulipuuzi kabisa wazo la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, isipokuwa tutalichukua na kulikabidhi katika Mamlaka mpya kwa kuzungumza pamoja na uongozi wa Mkoa wa Tanga.

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Sehemu ya 4

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nachangia nilieleza juu ya wasiwasi wangu juu ya kutunga sheria ambayo itawapa wafanyabiashara katika nchi hii haki na nguvu ambazo zinazidi wafanyabiashara wengine na nikasema kwamba mfanyabiashara ambaye ataendesha bandari kwa mujibu wa kifungu cha 27 anakuwa na haki ya kuuza tu mali ya mtu bila kuchukua hatua yoyote.

Sasa majibu ambayo nimepata leo hayaniridhishi hata pamoja na mabadiliko ambayo yamependekezwa kwenye hii *second schedule of amendment* ambayo imetolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapendekeza lile neno *operator* katika hiki kifungu liondolewe na badala yake iwe *authority.* Mimi nafikiri wamemvisha mtu kanzu

badala ya kumvisha *kaunda suit.* Sasa mimi hoja niliyokuwa nayo ni kwamba kusiwe na hii *automatic right.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu liko kwenye ile *schedule* ambayo nimetoa na nilikuwa napendekeza kwamba tuegemee zaidi kwenye Sheria ya Mikataba. *Law of Contract Ordinance* ina vipengele ambavyo vinahusu haki za *beillie,* haki za mtu ambaye ameshikilia mizigo ya mtu, ziko wazi kabisa kwenye ile sheria na hakuna sababu yoyote ya kutunga sheria nyingine ili huyu baillie ambaye sasa ni *operator* pale Bandarini apate haki ambazo ni za ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napinga hili wazo la kubadili neno *operator* liwe *authority* kwa sababu nia ya hii sheria tunayoipitisha ni kubinafsisha ile Bandari. Kwa hiyo, hatutegemei kwamba ile *authority* iwe ndiyo inaendesha ile Bandari, tunategemea *operator* ndiye awe anaiendesha na ndiye atakuwa na ile mali ya yule mtu. Sasa Bandari itapata wapi hiyo mali ili iuze wakati ile mali imeshikwa na *operator?*

**MWENYEKITI:** Maelezo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikiliza Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, tumekubaliana naye katika suala la msingi na hili nalo nasisitiza kwamba linanishangaza. Kwa kweli ni kumtetea huyo mwenye meli wa nje ili aweze kuingia kwenye Bandari zetu akwepe aondoke na meli yake tushindwe kumkamata. Kweli Bunge lako Tukufu linataka kuridhia mazungumzo ya namna hiyo? Watanzania watatushangaa sana. Hapa hapa tunaambiwa tunawatetea sana hao wawekezaji kutoka nje, tuwa-*vet,* tuwapekue! Sasa kuna mtu anakuja na meli yake, tunabishana naye kuhusu gharama, tumwachie uhuru wa kuweza kuondoka halafu asitulipe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waheshimiwa Wabunge watuelewe kuhusu hili. Serikali isingependa kukubaliana na Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, maelezo ya nyongeza.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa maelezo mazuri tu. Niongezee kwa kusema kuwa kifungu ambacho tuko sasa hivi, kiko tofauti kidogo tu na kile ambacho hoja yake ya msingi inakuja katika *clause* ya 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, bado Serikali inasema haikubaliani na Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai. Maelezo yake ni mazuri sana lakini chombo hiki pamoja na kwamba kitakusudia kusimamia shughuli zake, lakini bado kina jukumu hilo hilo. *The basic function* itabaki ni ya *Tanzania Ports Authority.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lake mimi nalifahamu kama Mwanasheria kwamba tuna Sheria ya *Contract* ambayo inasimamia utaratibu. Kama nakabidhi mizigo yangu kwako, kuna majukumu fulani ambayo unapashwa uyazingatie. Lakini sheria za Tanzania hazikatazi kwamba unapotunga sheria ya ku-*create* chombo kama hiki ambayo inaitwa *Structury Authorities* kwamba unaweza ukaweka utaratibu unaofanana na wengine lakini uwe ndani ya sheria na huo ndio utakaotawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kusema kwamba, unapotunga sheria unaangalia kule ulikotoka na hapo ulipo. Kifungu hiki kimetusaidia sana katika sheria yetu ya sasa ya *THA.* Kwa wale ambao wanayo sheria, ni kifungu cha 33 ambacho kipo kwenye sheria. *We are not inventing a wheel* na ni vizuri mwenzetu akatuelewa. Kifungu kidogo cha sita cha Muswada huu kinaweka pia kwamba: "Anaweza akaenda kutumia utaratibu mwingine ambao upo akauacha huu." Tungeomba sana mwenzetu atuelewe kwamba chombo hiki kitakuwa kinasimamia, ma-*operators* watafanya, inamaanisha kwamba tunajiondoa kabisa katika usimamizi na uendeshaji wa *Ports* zetu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 5
Sehemu ya 6
Sehemu ya 7
Sehemu ya 8

*(Sehemu zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Sehemu ya 9

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena. Mimi nina swali lingine.

Nilizungumza katika hoja hii kwamba kuna meli ambayo imezama katika milango ya kuingia Pangani na inasemekana meli ile ilizama wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia na imekuwa ni kikwazo kwa kuendeleza Bandari ndogo ya Pangani na hasa vile vile katika kuongoza majahazi na meli ndogo ndogo zinazoingia pale, mara nyingi husababisha hasara na vifo vya watu. Sijui Serikali inasema nini juu ya meli hii kwa sababu nilikwishauliza maswali mengi Bungeni, lakini kikwazo kikubwa ilikuwa ni utaalamu pamoja na fedha na sasa tunapitisha sheria kuipa Mamlaka nyingine shughuli kama hizi, je, Serikali ina kauli gani na hatma ya ile meli na shughuli za maendeleo katika Bandari ile ndogo? Hata Mheshimiwa Waziri alipokuja Pangani juzi nilimwonyesha eneo lenyewe kwa mbali tu kidogo. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyothibitisha Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, mwenyewe nilikuwa

Pangani wiki mbili zilizopita na moja ya sababu ya kwenda Pangani ilikuwa ni kwenda kuona hapo mahali ambapo Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, alinionyesha kwa mbali na akanionyesha maboya na umuhimu wa kuongeza maboya ili kuweza kuingia katika Bandari ya Pangani kwa usalama zaidi. Ningependa kumhakikisha kwamba hili suala tutalishughulikia na itakuwa ni moja ya kazi za Mamlaka mpya ya Usimamizi wa Bandari kulishughulikia pamoja na *SUMATRA* kwa sababu ya suala la usalama. Hatujui kama kuna mabomu katika meli ile, lakini kuna Mikataba ya Kimataifa inayohusu uokoaji wa meli au uvuaji wa meli za namna hiyo, tutazingatia katika kutekeleza suala hili. Ahsante sana.

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 10
Sehemu ya 11

*(Sehemu zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 12
Sehemu ya 13

*(Sehemu zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Sehemu ya 14

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 15

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 2

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Shughuli za Bandari**
***(The Ports Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeufikiria Muswada huu na imeukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Shughuli za Bandari wa Mwaka 2004 *(The Ports Bill, 2004)* kama ulivyobadilishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

*(Saa 6.53 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**HOJA ZA SERIKALI**

**AZIMIO**

**Azimio la Kuridhia Itifaki Kuhusu Uanzishwaji wa Umoja wa Forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Protocol on the Establishment of the East African Customs Union)***

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Azimio la Bunge kuhusu Tanzania kuridhia Itifaki ya Kuanzisha Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani *Protocol on the Establishment of the East African Customs Union.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, chini ya Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Lephy

Benjamin Gembe, Mbunge wa Mpanda Kati, kwa kuchambua Itifaki hii na kukubali iletwe mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 30 Novemba, 1999 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Jamhuri ya Kenya na Jamhuri ya Uganda ilitia saini Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa Ibara ya Pili na Ibara ya Tano ya Mkataba huo nchi wanachama zilikubaliana kuanzisha pamoja, pamoja na mengine Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutekeleza Ibara ya 7 na ya 75 za Mkataba wa kuanzisha umoja huo ambapo nchi wanachama zilikubaliana kukamilisha Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kipindi cha miaka minne tangu Mkataba huo ulipotiwa saini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia makubaliano hayo tarehe 2 Machi, mwaka 2004 Wakuu wa nchi za Afrika Mashariki walitia saini Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa mujibu wa Ibara ya 43 Itifaki itaanza kutumika baada ya kuridhiwa na wananchi wanachama na taarifa ya ridhaa ya kila nchi kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya kuanzisha umoja huu ni kuweka mazingira mazuri ya kibiashara miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kati ya Jumuiya hii na nchi za nje ya Jumuiya hii. Kutekelezwa kwa Itifaki hii kutakuwa kichocheo cha maendeleo kwa wananchi wa nchi za Jumuiya ya Mashariki hasa kwa kupanua soko, kukuza biashara, kuvutia wawekezaji wakubwa na hivyo kupanua fursa ya ajira.

Aidha kuridhiwa kwa Itifaki hii na nchi zote wanachama kutawezesha Itifaki hii kuanza kutekelezwa ndani ya muda uliopangwa. Vile vile hatua hii itawezesha Serikali kuhuisha viwango vya ushuru wa forodha yaani *Custom Duty* vya sasa na viwango vya Ushuru wa Forodha vilivyopangwa kutumika kwenye Itifaki ya Umoja wa Forodha kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa upande mwingine utekelezaji wa Itifaki hii ni hatua muhimu ya kufikia malengo ya kuanzisha kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi wanachama zimekubaliana utekelezaji wa Itifaki mnamo mwezi Januari. Nitarejea! Nchi wanachama zimekubaliana kuanza utekelezaji wa Itifaki mnamo mwezi Januari mwakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe maelezo mafupi, kuhusu Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Itifaki hii ina Ibara ya 44 ambazo zimegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

Sehemu ya kwanza, ni Ibara ya kwanza inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumiwa katika Itifaki. Sehemu ya pili, yenye Ibara ya pili hadi ya nne, inaanzisha Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuelezea malengo na maeneo ya ushirikiano katika umoja huo ambayo ni pamoja na

Kwanza, kupunguza viwango vya ushuru baina ya nchi wanachama, yaani *programme for the elimination of internal talents* ili kufikia kiwango cha asilimia 0 (sifuri) katika kipindi cha miaka mitano tangu mkataba kuanza kutekelezwa.

Pili, wana kiwango sawa cha uhuru wa nje ya eneo la Jumuiya yaani *Common External Service.*

Tatu, wana taratibu za kuhakiki uwasili wa bidhaa, *rules of origin.* Nne, uanzishaji wa mfumo wa misamaha ya kodi, yaani *harmonization of exemption*. Tano, wana mfano wa kisheria na kiutawala wa kuendelea Umoja wa Forodha yaani *Common Customs Management Law* na Sita, uanzishaji wa utambuzi wa bidhaa, yaani *harmonize commodity distraction and quality system.*

Sehemu ya tatu, yenye Ibara ya tano hadi Ibara ya tisa inazungumzia ushirikiano katika usimamizi wa masuala ya Forodha. Kuainisha nyaraka za Forodha na Ushirikiano katika upelelezi na udhibiti wa makosa ya kiforodha.

Sehemu ya nne, yenye Ibara za 10 hadi 13 inahusu uendelezaji wa masharti ya biashara yaani *trade liberalization* ambapo utaratibu wa kuondoa ushuru kwa bidhaa za nchi wanachama umebainishwa. Chini ya utaratibu Kenya itaondoa mara moja ushuru huo kwa bidhaa kutoka Tanzania na Uganda ambapo Tanzania na Uganda zitaondoa ushuru huo kwa bidhaa za Kenya kwa awamu katika kipindi cha miaka mitano. Hili litatekelezwa kwa mtiririko wa kutunza viwango vya sasa kwa mwaka wa kwanza na kufikia asilimia 0 mwaka wa tano.

Aidha, sehemu ya nne inaweka viwango sawa vya ushuru kwa bidhaa kutoka nje ya eneo la Jumuiya na kupiga marufuku vikwazo visivyo vya kodi yaani *non-tariff berriers* katika biashara miongoni mwa nchi wanachama. Nchi wanachama zimekubaliana kuwa na viwango sawa vya ushuru wa bidhaa zinazotoka nje ambavyo ni asilimia 0, 10 na 25. Kiwango cha juu cha ushuru cha asilimia 25 kitafanyiwa tathmini ndani ya miaka mitano kwa lengo la kuangalia athari ya utekelezaji wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano yenye ibara ya 14 hadi ya 19 inaweka Kanuni za kibiashara. Ikiwa ni pamoja Kanuni za uwasili wa bidhaa za *rules of origin* Kanuni dhidi ya biashara isiyo halali *anti-dumping and countervailing come measures* na hatua za tahadhari iwapo uchumi wa nchi wanachama utadhurika kutokana na utekelezaji wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kanuni za uhakiki wa uwasili wa bidhaa, yaani *rules of origin,* nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutumia vigezo vifuatavyo:-

Cha kwanza, bidhaa zinazotengenezwa kwa malighafi yote kutoka ndani ya Jumuiya, yaani *whole produced in East Africa.*

Pili, bidhaa zilizotengenezwa kwa kutumia malighafi kutoka nje, lakini ziwe zimefanyiwa mabadiliko kwa kiwango kikubwa ndani ya Jumuiya yaani *substantial*

*transformation* ili kutimiza kigezo hiki. Inabidi kwanza thamani ya malighafi kutoka nje ya Jumuiya isizidi asilimia 65 ya thamani ya bidhaa kamilifu.

Pili, ongezeko la thamani katika malighafi kutoka nje, yaani *Value added* ifikie angalau asilimia 35 na

Tatu, mabadiliko yaweze kubadili sura ya bidhaa pamoja na nambari maalum ya kutambua bidhaa.

Sehemu ya 6 na 7 zenye ibara ya 25 hadi ya 32 inaweka taratibu za mipango ya kukuza mauzo nje ya nchi, *efforts promotion schemes,* pamoja na maeneo maalum ya kiuchumi yaani *especially economic source.*

Sehemu ya 8 inaelezea azma ya nchi wanachama kuianisha Sera na Taratibu za misamaha ya ushuru wa forodha. Hadi sasa tumekubaliana kuiainisha misamaha ya ushuru wa forodha katika maeneo mengi. Hata hivyo mazungumzo yataendelea kuhusu maeneo machache yaliyobaki.

Sehemu ya tisa na ya mwisho inaeleza mambo ya kijumla yakiwemo namna ya Umoja wa Forodha utakavyoendeshwa. Kuweka hatua zitakazoweka ulingano pale tofauti zinapojitokeza. Hatua na tahadhari pale uchumi mwanachama unapoathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na matumizi ya Itifaki hii. Hizo *sector measures.* Uhusiano wa kibiashara na nchi au taasisi nje ya umoja huu na uhusiano wa umoja huu na maeneo mengine ya ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati kusaini Itifaki hii, nchi wanachama zilikuwa zinaendelea na majadiliano kuhusu maeneo machache ambayo hayakuwa na muafaka kwa lengo la kuihuisha katika Itifaki, kadri makubaliano yatakavyofikiwa. Maeneo haya ni:-

(a) Sheria ya usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani *East African Community Customs Management Act.*

(b) Viwango vya ushuru kwa bidhaa nyeti, *sensitive products.* Hivi sasa nchi wanachama zimekubaliana juu ya viwango vya ushuru kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje isipokuwa baadhi ya bidhaa nyeti ambazo ni mchele, magunia yaani *jute bags,* na ngano.

(c) Suala la nchi wanachama wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa wanachama wa Jumuiya nyingine za namna hiyo. Kwa mfano, pamoja na nchi hizi kuwa wanachama wa Juimuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania ni mwanachama wa *SADC* wakati Kenya na Uganda ni wanachama wa *COMESA.* Jumuiya zote mbili za *SADC* na *COMESA* zina lengo la kuunda Umoja wa Forodha. Kwa kiwango kikubwa maeneo hayo yamepatiwa ufumbuzi na yale machache yaliyobaki yanaendelea kutafutiwa ufumbuzi.Tathmini zilizofanywa zinaonyesha kwamba utekelezaji wa Itifaki hautaathiri mapato ya Serikali wala mazingira ya wawekezaji nchini. Hata hivyo, katika

kutekeleza Itifaki hii kutakuwa na gharama ambazo zitatokana na kuongezeka kwa michango ya nchi wanachama kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi ya Makao Makuu ya Jumuiya kutokana na kuanzisha kwa  Idara ya kuratibu shughuli za forodha na biashara yaani *directorate of customs and freights.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba sasa kusoma Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki la kuanzisha Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, yaaani *(Protocol on the Establishment of the East African Customs Union)* kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Serikali ya Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki kwa mujibu wa Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki uliotiwa saini tarehe 30 Novemba, 1999; na

KWA KUWA kwa mujibu wa Ibara ya pili na ya tano ya Mkataba huo nchi wanachama zimekubaliana kuanzisha pamoja na mambo mengine Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutekeleza Ibara ya 7 na ya 75 ya Mkataba huo ambapo nchi wanachama zilikubaliana kukamilisha itifaki ya kuanzisha Umoja huo katika kipindi cha miaka minne tangu kutiwa saini Mkataba huo; na

KWA KUWA nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walitia saini Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 2 mwezi wa tatu, mwaka huu; na

KWA KUWA lengo kuu la Itifaki hii ni kuimarisha biashara baina ya nchi wanachama kwa kuondoa vizuizi mbalimbali vya kodi na kuweka mazingira mazuri ya kuongeza uzalishaji na kuvutia wawekezaji kwenye eneo la Afrika Mashariki na

KWA KUWA madhumuni ya Itifaki hii ni kuziwezesha nchi wanachama kushirikiana katika kukuza biashara na kuwezesha ukuaji mzuri wa uchumi wa kila nchi mwanachama; na

KWA KUWA kuridhia Itifaki hii utainufaisha Tanzania kwa kupanua wigo wa ushirikiano wa nchi wanachama katika kuleta maendeleo ya wananchi wa Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla; na

KWA KUWA kuridhiwa kwa Itifaki hii na nchi zote wanachama kutawezesha ianze kutekelezwa katika muda uliopangwa ambao ni tarehe mosi Januari, mwakani, hatua ambayo itaiwezesha Serikali kubadilisha viwango vya ushuru wa forodha vya sasa ili viwiane na viwango vya ushuru wa forodha vilivyokubalika kwenye *track* hii;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa Itifaki hii na manufaa yanayoweza kupatikana kwa kupanuka wigo wa ushirikiano katika Sekta za biashara na kukuza uchumi na kwa mujibu wa Ibara ya 63 ambapo Ibara ndogo ya 3 Kifungu (e) ya Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977, Bunge la Tanzania katika Mkutano wake wa kumi na saba, sasa linaazimia kuridhia Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya

Afrika Mashariki yaani *(Protocol on the Establishment of the East African Customs Union)* chini ya Ibara ya pili ya Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. LEPHY B. GEMBE - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu kuridhia Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani *(Protocol on the Establishment of the East African Customs Union).*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 70(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi baada ya kukamilisha kazi ya kulipitia na kupata maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, juu ya Azimio la Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni tukio muhimu baada ya marais wa nchi tatu, Jamhuri ya Muungao wa Tanzania, Jamhuri ya Kenya na Uganda walipotia saini Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Kamati inazipongeza Serikali za nchi za Afrika Mashariki hususan marais wetu kwa kufikia maamuzi hayo muhimu katika kipindi hiki cha utandawazi ambapo hata mataifa makubwa duniani yanayoendelea yanasimamia na kuendeleza uchumi wa nchi zao kwa kuungana kwa kuwa na Jumuiya ya masoko ya pamoja *common market.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono mia kwa mia hoja iliyopo mbele yetu ikizingatiwa kuwa kuanzishwa kwa umoja huu kutaweka mazingira mazuri ya kibiashara miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ndani na nje ya Jumuiya na kuwa kichocheo cha maendeleo kwa wananchi wetu hasa kwa kupanua soko, kukuza biashara, kuvutia wawekezaji wakubwa na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, Kamati ina maoni yafuatayo:-

Kamati inashauri Sheria zote husika katika kuimarisha uhai wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni vema zikafanyiwa mapitio kwa lengo la kuziboresha ili ziendane na wakati. Kamati inashauri suala la nchi za Jumuiya kuwa na wanachama katika Jumuiya tofauti

kama vile Tanzania ni mwanachama wa *SADC* wakati Kenya na Uganda ni wanachama wa *COMESA*. Ni vema likaangaliwa ili kuepuka migongano ya sheria zinazoendesha vyombo hivi. Aidha, Kamati inasisitiza utekelezaji wa Itifaki ni vema ukaanza kutumika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Basil P. Mramba, Mbunge, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Abdisalaam Issa Khatibu, Mbunge, Maofisa kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wote Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati imepitisha Azimio la Kuridhia Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR JUMA OMAR (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MWENYEKITI KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI):** Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni maoni ya kambi ya upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya kuanzishwa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani *(Protocol on the Establishment of the East African Customs Union).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kutoa maoni kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1), Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri katika uwafikiwaji wa hatua hii ambayo ni muhimu katika kukuza biashara kati ya wananchi wa mataifa haya. Vile vile katika kukuza uchumi baina ya mataifa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 2(4)(a) hapa tunadhani uhusishaji na uondoaji wa Ushuru wa Forodha kwa nchi zote tatu sasa kwa upande wetu nadhani Sheria ya Kodi kama ilivyopitishwa na Bunge hili maana yake ni kupunguza mapato ya nchi.

Katika hatua za uainishaji na ushauri wa forodha kwa nchi zetu ni nani atakuwa anafidia hiyo hasara. Kwani hiyo ni sawa na kutoa subsidize tunavyoelewa pale panapotolewa *subsidy* huwa kuna mtu wa kufidia lile pengo. Kambi ya Upinzani kwa hili ni nani atafidia pengo hili itakapotokana na ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuwa Bunge lako Tukufu linaridhia Azimio hili, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kwanza iangalie na kurekebisha mambo yanayosababisha ughali wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini ili Sekta binafsi iweze kuzalisha bidhaa zitakazoweza kushindana na bidhaa kutoka kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, vinginevyo tutaendelea kuwa soko tu. Kambi ya Upinzani inashauri viwango vya umeme, maji pia upatikanaji wake viangaliwe upya. Kwani hii ni

pamoja na nyanja zinazolalamikiwa na sekta binafsi kuhusu kupanda kwa gharama za bidhaa zinazozalishwa hapa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasikitika sana kwa hili, kwani badala ya Tanzania kujiandaa na kujitayarisha vizuri kwa hili la kuingia kwenye Jumuiya kama mshiriki halisi yenyewe, inaongeza kero kwa *TANESCO* kuongeza gharama za umeme, ushuru na malighafi kutoka nchi ambayo ni mwanachama uko pale pale, sasa hapa Tanzania viwanda vyake itafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado katika hili inaonyesha ni vipi Tanzania imejiandaa nalo na ni bidhaa za aina gani zitashindanishwa na bidhaa toka Uganda na Kenya, kwani licha ya ushuru kuwapo bidhaa za Kenya zilichukua sehemu kubwa ya soko sasa bila ushuru itakuwaje? Viwanda vyetu vitafungwa au vipi? Bado tunahitaji tafiti za kina na kuhusisha sekta binafsi kwa hili badala ya maamuzi kuwa lengo la kujinufaisha kisiasa kuliko hali halisi ya wazalishaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhakiki wa uwasili wa bidhaa rules of origin kipengele kipi kinaweza kuonekana ni kigumu kwani kama nguo zimetengezwa Bara la Asia, kwa vile viwanda vya huko vina makubaliano na wafanya biashara wa ndani ya nchi mwanachama, wakaleta kwa kusambaza kwenye masoko ya ndani.

Mifano mingi tunayo, kwani mara nyingi hata wahusika hushindwa kutofautisha bidhaa za China, India, Pakistan na zile za Urafiki na viwanda vingine vya ndani. Kambi ya upinzani inauliza katika soko holela la nchi tatu hizi itakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani inauliza katika uanzishwaji huu wa Umoja wa Forodha nchi mwanachama, akitaka bandari huru itakuwaje? Kwa mfano, Mombasa, Tanga, Mtwara na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inadhani katika ushirika wowote ule una sheria zinazoendesha na pindi mwanachama anapokwenda kinyume kuna Kanuni za kumwadhibu au kumwekea vikwazo. Sasa kama nchi mwanachama wa Jumuiya itatunza au ina sera zinazopingana na vifungu vya mkataba wa ushirikiano, kuna vikwazo vyovyote kwa nchi hii au vipi? Au kuna chombo chochote kitakachosimamia matatizo kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba maelezo toka kwa Waziri. Tofauti ya maendeleo kiuchumi kati ya nchi mwanachama inaweza kupunguza kasi ya mshikamano, wale walio juu kiuchumi wanaweza kuhisi anatumiwa au kufanywa daraja na wengine.

Sasa kuna *workerble composition mechanism* zipi za kuhakikisha wale waliofuta ushuru, kwanza wanafidiwa ili wasihisi huwa wanatumiwa kwa maendeleo ya wengine. Tunaomba maelezo kwa hili pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkataba na maelezo ya Waziri hatujaona kipengele kinachohusu mgawanyo wa mapato na ni chombo gani kitakuwa na mamlaka ya kuidhinisha mganyo huo na katika viwango vipi baina ya nchi mwanachama. Kambi

ya upinzani inaona hiki ni kitu muhimu kuwekwa wazi, wakati umoja huu unaanza kwa maendeleo ya umoja wake ili kuondoa mtafaruku hapo baadaye na kusababisha kuvunjika wakati unahitajika, kama kipengele hiki kitaeleweka na kuwekwa bayana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika hoja hii. Ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wote ambao wameshiriki katika kujadili na katika kuupelekea kusainiwa kwa Itifaki hii. Ningependa vile vile kumpongeza sana Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo ameleta mapendekezo haya kwa ufanisi mkubwa na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii imekuja kwa wakati muafaka hasa tukizingatia kwamba inatarajiwa ianze kufanya kazi mnamo tarehe 1 Januari, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika masuala haya ya uhusiano wa maeneo mbalimbali ni kitu muhimu sana ni kitu muhimu kwa sababu ni kama vile ambavyo naelezwa kwamba inawezesha nchi za jirani katika makundi hayo kuweza kufanya ushirikiano wa maeneo mbalimbali hasa kukuza biashara na kukuza uwekezaji. Kwa hivyo kuongeza mapato ya nchi, mapato ya Wananchi mbalimbali, mapato ya Serikali na kukuza kwa uchumi na Ustawi wa Jamii kwa ujumla.

Azimio hili kama wengi wanavyosema kwamba umoja ni nguvu na hili Azimio lina dhamira ya kuimarisha umoja wetu kati ya sisi na nchi nyingine za Afrika Mashariki. Kama tunavyojua kwamba suala la forodha ni suala muhimu sana na itifaki hii tukiridhia na kupitisha itakuwa ni hatua moja kubwa sana ya kutupelekea sisi katika kukamilisha Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki ambayo tunatarajia kuitekeleza. Kwa hiyo, mimi ningependa kusema kwamba naunga mkono itifaki hii au kuridhia kwa itifaki hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hii ni hatua moja nzuri lakini vile vile ni vizuri tukajiangalia na sisi kwamba tumejitayarisha vipi. Tanzania tuna bahati nzuri ya kuwa na mikataba mingi na jamaa wengi lakini katika utekelezaji mara nyingine tunakuwa kidogo tunakwama. Tukitazama kwa mfano tayari tunatakiwa tufaidi kutokana na mkataba wa *AGOA* lakini bado hatujafaidika inavyotakiwa tunatarajiwa kwa mfano au kushiriki au kufaidi kutokana na *EBA* ya Ulaya lakini bado *EBA* hatujafaidika vya kutosha. Tayari tunatakiwa Tanzania tuwe tunafaidika na vitu vinavyoitwa *GENERAL SCHEMES OF PREFERENCES (GSP).* lakini bado Tanzania hatujachukua hatua thabiti za kuweza kushiriki na haya. Na kama tunavyojua katika Jumuiya yetu hii ya Afrika Mashariki baadhi ya wenzetu wameendelea sana kiuchumi kuliko sisi tulivyo.

Sasa hii itifaki inajaribu kutuweka katika hali ya usawa lakini tusibweteke kwa sababu hizi provisions zilizotolewa za *duty depreciation* kwa muda mfupi. Kwa hiyo,

ni lazima tufanye jitihada kubwa sana sisi ya kujitayarisha ama sivyo kwa kweli tutabaki kuwa soko la wenzetu ama sivyo tutabaki kuwa sisi ni wasindikizaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tahadhari hiyo ni muhimu sana kuchukua kuzingatia hali halisi hivyo ilivyo. Kutokana na hayo nafikiri kuna haja kubwa sana ya sisi kufanya matayarisho ya kutosha ili tuweze kufaidika na soko hili.

Kujizatiti kwetu tunahitaji masuala mawili. Kwanza suala moja kubwa sana ambalo tunalo sisi tuna matatizo ya bidhaa za huduma za kutosha yaani kwa kizungu tunasema *supply constrains* ni muhimu tukafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba tuna bidhaa sisi za kutosha ambazo kwa idadi yake zinaweza kutosheleza mahitaji haya ambayo tunafikiri yatakuwa katika soko hili la Afrika Mashariki na vile vile viwango vyake vya ubora viwango vyake vya ukopeshaji zote na bei zake ziweze kuwa nzuri. Sasa ili haya yaweze kuwa mazuri ni muhimu sisi tukaongeza utendaji wetu katika viwanda vyetu mbalimbali katika shughuli zetu za uzalishaji mbalimbali ili tuweze kuwa na bidhaa za kutosha na bidhaa ambazo zinaweza kushindana kiushindani. Tukumbuke kwamba kwa muda mrefu soko letu sisi kwa kiasi fulani limekuwa linajitazama ndani uzalishaji umekuwa ukitazama ndani ulikuwa ukitazama utaratibu wa allocation distribution kupitia katika *RTC* na vitu kama hivyo.

Sasa katika soko hili ambalo ni kubwa linapanuka wao wenzetu wengine watakuwa wanatazama zaidi ubora wa bidhaa na bei za bidhaa yaani *A Competitive advantage* iliyopo. Pamoja na fursa zote tulizopewa tunaweza kushindwa kutumia fursa hizo kama huduma zetu na bidhaa zetu mbalimbali haziko katika hali hiyo. Kwa hiyo, hilo ni suala la kutazama sana. Vile vile ni vizuri kuchukua hatua thabiti kwa upande wa mapambano makali dhidi ya vikwazo mbalimbali. Tuna vikwazo mbalimbali sisi ambavyo vinatufanya bidhaa zetu zisiwe zinashindana kwa umahiri katika soko la dunia. Tuna matatizo kama vile urasimu, kubweteka, tumezoea kufanya mambo kutazama shughuli za ndani lakini nadhania sasa hivi soko la nje linafunguliwa kwa upana zaidi ni vizuri watendaji wetu katika sehemu mbalimbali hasa katika sehemu za forodha, sehemu za bandari wakaelewa kwamba mambo haya yanatakiwa yafanywe kwa ufanisi zaidi na kwa umahiri zaidi kuliko ambavyo tulivyokuwa.

Kwa upande mwingine kuna haja kubwa sana ya kuchukua hatua thabiti kuboresha miundombinu zetu mbalimbali ili bidhaa na huduma ziweze kutolewa kwa urahisi zaidi. Miundombinu kama umeme, umeme unapatikana sana kwa shida unakatikatika bei zake ni kubwa kidogo ukishindanisha na wengine limezungumzwa suala hili lakini bado lipo na matatizo haya. Maji nayo yana matatizo vile vile barabara nazo pamoja na jitihada kubwa zilizofanywa lakini bado jitihada zinazidi kufanyika kwa mfano barabara ya Tanga Horohoro ni moja ya barabara muhimu ambayo inaunganisha nchi yetu hii na nchi nyingine. Tunashukuru kwamba jitihada zimefanywa imeruhusiwa baadhi ya madaraja tayari na baadhi ya madaraja mengine yatatengenezwa baadaye lakini kuna haja kubwa sana ya kukamilisha barabara ile ili iweze kuwa katika kiwango cha lami ili iweze kufaidisha kufanya nchi yetu na Wananchi wetu wakapata kichocheo kizuri cha kuwafanya wao waweze kuzalisha mazao na kuweza kutoa huduma nyingine ambazo zitatufaidisha katika taifa letu. Kuhusiana na Bandari leo asubuhi tulikuwa tunazungumzia Muswada wa bandari, bandari ya Tanga ni moja ya bandari ambayo tokea

juzi tunazungumza pengine ingeweza kufanya vizuri zaidi kama hatua thabiti zingeweza kuchukuliwa ili bandari ile iweze kupanuliwa na ilizungumziwa habari ya kuipanua ile bandari na kupeleka mwambani lakini ni kitu ambacho kidogo kimesahaulika au katika mpango wetu hakina kipaumbele. Kwa hiyo, inastahili ifikiriwe hivyo ili kuwezeshwa kufanya vile. Tukiunganisha hiyo na masuala mengine ya barabara kuna barabara kwa mfano inayotoka Tanga kupitia Pangani kuja Dar es Salaam. Barabara hiyo ikitengenezwa inaweza kusaidia sana kufungua biashara kutoka Kenya au kutoka Tanzania kwenda Kenya kutoka Dar es Salaam hadi Mombasa na kwenda moja kwa moja kuliko ilivyo sasa hivi. Vile vile ziko barabara nyingine ambazo zinaunganisha nchi zetu hizi muhimu zinafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika , kuhusu reli zetu, kuna suala la reli ya kutoka Arusha mpaka Musoma ni muhimu sana reli hii ikafanyiwa kazi iwapo tunataka kufaidi biashara kati yetu sisi na Uganda ipanuke zaidi. Kwa hiyo, hili suala limezungumzwa muda mrefu na ni muhimu reli ile ikaanza kufanyiwa kazi. Vile vile reli zetu tulizonazo sasa hivi Reli ya Kati na Reli ya Tanga na reli nyingine zile za *TAZARA* ziko lakini haziko katika hali nzuri. Hizi reli hazina budi zikaboreshwa zikawa katika hali nzuri iwapo sisi tutataka kufaidi kuendelea biashara na wenzetu wengine. Ni muhimu bidhaa ziwe zinaenda kwa kasi, zinatoka kwa kasi zinarudi kwa kasi ili pasiwepo na vikwazo ambavyo vitakwamisha mwenendo mzuri wa biashara na uewekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Hamasa na Motisha kwa uwekezaji ni suala muhimu sana hili limezungumziwa katika maeneo mbalimbali, lakini wakati tukizungumzia soko letu hili ni muhimu tukawahamasisha wafanya biashara wetu na wawekezaji wetu wao wenyewe wanaelewa lakini hasa wafanya biashara wadogo na wawekezaji wadogo kwamba hili ni soko maalum lina nafasi za kipekee na ni vizuri tukachukua hatua thibiti ili kuweza kuzalisha kwa wingi vizuri zaidi na sisi au Serikali ikafikiria utaratibu wa kuweza kuwapatia motisha wa kuweza kufanya hivyo. Najua motisha zimetolewa lakini kuna umuhimu wa kuboresha motisha zaidi kutokana na hali ile. Najua humo ndani katika itifaki hii kuna masuala ambayo hayakubaliani na utaratibu wa kutoa *subsidy* maalum isipokuwa pale tunapofanya *export* au *export promotion measures* isipokuwa pale panapohusu *export* lakini hii nafikiri ni suala muhimu ambalo linahitajiwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu, Ufahamu na Mwamko kwa Wananchi wetu kwa ujumla ni muhimu sana ili waweze kuelewa suala hili kwa karibu zaidi ili waweze kujizatiti kuweza kufaidika na suala hili. Mara nyingi nchi yetu inafanya mikataba inachukua suala hili lakini hili suala bado halijaeleweka. Mimi jimboni kwangu ni sehemu ya mpakani tuna biashara kubwa sana kati ya sisi na jamaa wa Kenya pale lakini bado Wananchi wenyewe licha ya maafisa wa forodha hawajawa na ufahamu mzuri juu ya suala hili kwa hiyo kazi kubwa sana inahitajika kutoa elimu kwa Wananchi hasa wale wa mipakani kuhusu jinsi gani ya kufaidika na itifaki hii ya kuendeleza biashara katika nchi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika hili suala la sisi kuwemo humu ndani kama vile watu ambao tumeamua kuogelea. Unapoamua kuogelea ni sharti uvue nguo na vile vile usisite

kutia mguu ndani ya maji ama sivyo maji yale yatakuja kwenda na yatafika daraja utakuja kukuta maji siyo ya kwako. Kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja hii lakini kuna haja kubwa sana ya sisi Watanzania kuwa imara. Sisi Watanzania, Serikali yetu na Wananchi wetu kujizatiti ipasavyo kuchukua hatua thabiti kuweza kufaidika na hili vinginevyo sisi tutabaki wasindikizaji. Sisi tutabaki tunaeleza watu kama mnavyojua wenzetu Wakenya hasa na Uganda kiasi fulani wameendelea sana na wana *exhibition* ya kibiashara, wao ni *aggressive* sana wao ni wabunifu wa masuala mengi ni muhimu kwa watu wetu kuwa wabunifu, ni muhimu kwa Serikali yetu kuchukua hatua ambazo zitawawezesha watu wetu kuwa wabunifu na kuwapandisha uwezo wa kufanya kazi hii kwa vizuri zaidi. Kwa misingi hiyo Mheshimiwa Naibu Spika mimi ningependa kuunga mkono hoja hii nzuri, ambayo imekuja kwa wakati muafaka na sisi Wabunge naomba tuunge mkono hoja hii na sisi tuwe mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba Wananchi wetu, wafanyabiashara wetu, wawekezaji wanalielewa vizuri suala hili na wanalichukulia hatua thibiti ili kuweza kufaidika inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kurudia tena kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika naomba nakushukuru kwa nafasi uliyonipa ili niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza natoa pongezi kwa Wakuu wetu wa nchi hizi tatu kwa kusaini mkataba unaohusu ushuru wa pamoja wa forodha mwezi Machi mwaka huu. Mimi ni muumini mkubwa wa ushirikiano wa kikanda. Kwa hiyo, dhana nzima ambayo imejitokeza katika hoja hii mimi naiunga mkono. Kwa hiyo, ningependa kuanza kwa kusema kwamba naunga mkono hii hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika naomba nielekeze mawazo yangu katika sehemu moja tu ambayo ni zao la chai. Nchi zote tatu ambazo zinaingia mkataba huu zinalima chai, lakini hali ya kilimo na viwanda katika nchi hizi zinatofautiana sana . Nikitoa mfano, Kenya inazalisha kilo milioni 300 kwa mwaka za chai ambapo Tanzania inazalisha milioni 25 kilo hadi 28 kwa mwaka ambayo ni pungufu ya asilimia 10. Ukiangalia orodha ya wakulima wa chai katika dunia, Kenya ni ya nne lakini Tanzania ni ya 14. Kenya ina wakulima wadogo wadogo wa chai 400,000 ambapo Tanzania inajivunia wakulima kama 15,000 tu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika utaona kwamba hizi takwimu zinajisemea zenyewe. Tumejiingiza katika ulingo, tukiwa hakuna ulinganifu. Biashara ni ni ya ushindani, siamini kama tuna *level ground* hapa. Kwa sababu tunaingia kushindana tusije tukaanza kusema refa alikuwa anapendelea upande mmoja. Nakumbuka kauli ya Marehemu Mwalimu Nyerere katika masuala haya ambayo *the ground is not level.* Alikuwa anasema kama unaniweka kwenye ulingo wa masumburi pamoja na Tyson wewe hunitakii mema unataka kuniua tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya ndani chai inayozalishwa inatosha kwa nchi zote. Nadhani wote ni mashahidi kwamba ukienda duka lolote hata Vijijini hutakosa chai. Hii hali tumeiona hapa Tanzania lakini vile vile hata Kenya, kwa hiyo matatizo hapa siyo kufungua mipaka ili chai ya Kenya iingie Tanzania au ya kwetu iende mahali pengine. Kama tunatakiana kheri katika shughuli za uchumi nadhani kinachohitajika hapa ni kwamba sisi kwa pamoja kama nchi za Afrika Mashariki tutafute soko la pamoja. Hii

ndiyo mikakati ambayo tunahitaji yaani kutafuta soko la nje badala ya hali tunayoidhinisha sasa hivi ya kugombea masoko ya ndani. Hivi sasa karibu kilo milioni mbili za chai zinapenya kuingia nchini kutoka nchi jirani hasa kutoka nchi ya Kenya. Tumeikuta hii chai Zanzibar huu wakati mpaka wa Kaskazini ndiyo kabisa lakini hata Songea kuna chai kutoka nchi za Kusini zinazolima chai vile vile.

Chai ya magendo kama tunavyojua kwa kawaida bei yakini rahisi, kwa hiyo watu wanaikimbilia. Kwa hiyo mkataba huu baada ya kusaini ina maana tunahalalisha chai nyingi ya magendo iingie hapa nchini. Hatari ninayoiona ni kwamba viwanda vyetu vitakufa. Shughuli za kilimo za chai, kwa muda mrefu zilikuwa zinaratibiwa na mamlaka ya chai ambavyo utendaji kama tunavyojua haukuwa mzuri. Wakulima walikuwa na malimbikizo ya malipo, pembejeo zilikuwa tabu kupatikana lakini kutokana na sera nzuri ya Chama cha Mapinduzi ya ubinafsishaji, viwanda vilibinafsishwa na tunaona matokeo kwamba vingi vimefufuliwa na vinafanya kazi vizuri.

Malimbikizo ya madai ya wakulima yamelipwa na vile vile wanachangia katika kutengeneza barabara kuna miradi ya wananchi na huduma mbalimbali za jamii. Kwa hiyo, katika maeneo ambayo zao la chai linalimwa wanaita chai ni mkombozi; ni mkombozi kwa uchumi kwa mkulima binafsi lakini vile vile kwa Halmashauri zetu na Taifa kwa ujumla. Kwa hiyo, ninavyoona ni kwamba tukifungua mipaka yetu na chai ikaanza kuingia humu haya maendeleo tuliyoyaona na ndoto tulizonazo kwa wakulima wetu zitaishia si mbali zitaishia hapa hapa. Mheshimiwa Naibu Spika, natambua Serikali kwamba imeondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa chai iliyosindikwa hapa nchini na nashukuru sana kwa hilo. Vile vile kama Naibu Waziri alivyosema ni kwamba kuna mazao au bidhaa ambazo kutakuwa na kodi ambayo itakuwa inapunguzwa mpaka miaka mitano itondolewa kabisa na zao la chai ni mmojawapo. Mategemeo ni kwamba ifikapo miaka mitano basi tutakuwa na uwanja ulio sawa wa kucheza pamoja na wenzetu wa Kenya ambao si kweli. Sasa swali ninalojiuliza ni kwamba kulikuwa na haraka gani ya kusaini mkataba huu kuhusu kipengele cha chai? Hivi ni lazima bidhaa zote zijumuishwe kwamba zianze kwa wakati mmoja?

Hapa tunazungumzia habari za Utandawazi. Kwa tafsiri ya haraka haraka utandawazi maana yake tufungue mipaka ili bidhaa ziingie na kutoka bila ya kuulizwa. Sisi tulio katika nchi zinazoendelea tumepiga sana kelele lakini zile zilizoendelea, zenye viwanda, wametupa shinikizo kubwa kwa vile wao wanaona kwamba utandawazi ndio fursa ya kupata soko kwa ajili ya bidhaa zake. Sasa tujiulize Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba Serikali haikujiuliza kuhusu shinikizo lililokuwa linatoka kwa majirani? Kipengele cha chai kilileta matatizo awali kweli na kukawa na shinikizo kubwa sana kutoka kwa wenzetu. Nadhani masomo tuliyopata kutoka Utandawazi tungejiuliza na sisi kuhusu suala hili .

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninavyoona ni kwamba Serikali ingeangalia upya kuhusu kipengele hiki cha chai. Nilikuwa naangalia katika Kitabu cha *Protocol* ukurasa wa 24 article (19) na ninaomba ninukuu: *"The partner states agree to apply safeguard measures to situations where there is sudden surge of a product imported into a Partner State, under conditions which cause or threaten to cause serious injury to the domestic producers in the territory of like or directly competing products within the territory".* Vile vile naomba niendelee anasema: *"during a*

*transitional period of five years after the coming to force of the protocol where a Partner State demonstrates that its economy will suffer serious injury the result of the imposition of the common external tariff on the industrial inputs and raw materials, the partner state concerned shall, inform the Council in other Partner States through the Secretary General on the measures it proposes to take".*

Nilikuwa napendekeza kwamba Serikali iangalie na *measures to take* niliona kwamba tuhairishe suala hili la kuingiza suala la chai katika *protocol* hii. Mheshimiwa Naibu Spika naomba niishie kwa kuunga mkono hoja hii na nasema ahsante kwa kuniruhusu kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. na pili Mheshimiwa Naibu Spika napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Katibu Mkuu wake na Wafanyakazi wote walioshughulikia hii itifaki na kuileta hapa kwetu ili tuweze kuiridhia. Mimi napenda kuchukua mwanzoni kusema kwamba naiunga mkono mia kwa mia. Lakini baada ya kusema hivyo kuna mambo machache ambayo napenda kutoa maoni yangu. *(Makofi)*

Sisi tumesema kwamba tukianza tu Uganda na Tanzania bidhaa zetu ziende huko Kenya bila kulipa ushuru. Lakini cha kuangalia sana uchumi wetu sasa na Kenya ukoje ukipanda ndege kama unatoka Nairobi ama unaingia utaona vile walivyo na viwanda vilivyo vingi tu lakini sisi hapa kwetu viwanda hamna. Ukitaka kuangalia kama pale *EPZ* tumeenda pale siku moja kwenda kucheki pale tukakuta hata umeme hawaingiza pale hata maji yule aliyejenga hilo jengo analia. Anatuambia bwana hapa hakuna umeme maji hamna halafu nikaangalia kale kajengo nika-*compare* na *South Africa* vijengo kama vile *South Africa* viko zaidi hata elfu kumi sisi ndio pale hata maji hatuna maji hata umeme hamna.

Sasa tunaposema *five years* bidhaa za Kenya zije bila ushuru hapa nyumbani hivi kweli tunaweza kujidanganya humu ndani kwamba *after five years* tutakuwa tume-*bridge* lile *gap.* Mbona vile viwanda ambavyo vinatayarishwa ku-*bridge* hiyo *gap* sivioni. Kwa hiyo, mimi nafikiria kwamba tunaweza kujikuta baada ya *five years* miaka mitano tukakuta tumeingia katika matatizo makubwa sana. Na kitu ambacho kilitakiwa hapa mimi nilikuwa nafikiria kwamba ingelikuwa hata miaka ishirini kwa sababu ukiangalia uchumi wetu na Kenya nilikuwa na soma gazeti la *East African* karibuni wakaorodhesha pale Bajeti yao kuja kuangalia wenyewe Wakenya Bajeti yao ya kwetu ikiwa tegemezi *by 42%* ya kwao ni 6.3% nikajua kwamba huu uchumi wa nchi hizi mbili haufanani. Sasa mimi wasiwasi wangu tutafika miaka mitano na tukakuta kwamba tuna matatizo makubwa zaidi na hatutakuwa tume-*bridge the gap* kama tulivyotarajia. Hii ni kama tunachukulia hili jambo kama jambo la kisiasa lakini uchumi ni kitu ambacho kina *reality.* Nilikuwa nashauri kama inawezekana hii miaka ingeongezwa ama tungetumia *phrase* kwamba tutaangalia *after five years* ili kama tutakuta hali bado ni mbaya tukaweza ku-*negotiate* lakini tukijifunga tutakuwa na matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine la kuangalia sisi Kenya na Uganda ziko *COMESA* sisi tuko *SADC* lakini kuna siku moja Kenya na Uganda watafanya *Custom Union na COMESA* na sisi itafika siku moja tutafanya *custom union* na *SADC* sasa hivi vitu vitaendanaje. Mimi kwa kweli katika kuulizwa kwani nini Tanzania ilijitoa *COMESA* sijapata sababu za kutosha. Ukiangalia kama *movement* ya vitu vitavyokuwa *goods* zina-*move* sisi kwetu hapa ni watu zile nchi za Kiafrika zitakuwa na shida sana na sisi wakati tuna-*move* mizigo yetu kwenda *COMESA* tutapata shida. Nafikiri kwa kweli jamani tuende turudi tena kwenye meza tufikirie upya hivi kweli Tanzania tunataka kujitoa kabisa *COMESA*. Ni sababu gani mbona hatujielezi humo vya kutosha mimi sijapata sababu za kuridhirisha mimi kuweza kuunga huo mkono. Mimi nafikiri kwa kweli tuangalie sisi na nchi za Afrika ya Mashariki lazima tufanye nao kazi kwa karibu. Uchumi wetu na nchi za Afrika Mashariki zinafafana sana desturi zetu sasa ukichukulia kama New Zealand ama *South Africa* uchumi wao ni tofauti sana. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba kwa kweli hii *COMESA* turudi humo. Sikae kwamba tusiwe *SADC* lakini baadaye itakapoanza ku-*rectify* hizi *Custom Union* haya mawili tutajikuta tuko katika hali mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna mazungumzo yanayoendelea yanaitwa: *"Economic Partnership Agreement between E U"* na nchi za Afrika sisi tuko kwenye upande wa *SADC* Kenya na Uganda ziko katika *East Africa Region.* Sasa ukiangalia hata tulipokwenda huko juzi wanasema nyinyi Watanzania tunasema kwamba *"East African Community Countries"* zi-*negotiate as a block* lakini ukifika katika *EPAC* mazungumzo haya hatuwezi sisi tuko *damped* kwenye upande wa *Southern Southern African Countries (SADC)* na hizi ziko *East African.* Lakini sasa hivi ukiangalia walituambia kwamba upendeleo utakaotoa katika hizi nchi zitatofautiana. Kwanza hizi nchi za *East African Region* ni nchi ambazo ni *less developed* sisi tumejikita na nchi ambazo *South Africa* imo. Kwa hiyo, tunaweza kukuta kwamba Kenya wanapewa na Uganda wanapewa *good will* wakati Tanzania ukakuta kwamba imepewa ambayo ni *low* kwa sababu tu tumejikita na nchi ambazo ni tajiri. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri vile vile katika mazungumzo haya ya *EPAC* ambayo lazima yakamilike 2008 mimi nafikiri kwamba tungelikuwa pamoja na nchi za Kenya na Uganda.

Pili lazima tuone maliasili ya Tanzania, ni nchi ambayo ina maliasili nyingi sana. Nchi kama Kenya maliasili yake ni ndogo sana hasa ukija mambo ya *Tourism, National Parks* zao. Lakini wanataka kufanya tu-*trade on equal bases.* Nafikiri hilo lilikuwa la kuangalia tukiachia hiyo *natural resources* yetu tukafungua mipaka kama kule Gorogonja wale wakaingia kwa sababu ni *custom union* wenyewe ndio watafaidi kuliko sisi kwa sababu Serengeti ina kila kitu. Ukija Tarangire, *KINAPA* na sasa wameshafikia kwamba hata mtu akitoka huko alipe *amount* ile ile yaani Mkenya akija alipe kama Mtanzania anavyolipa. Lakini kwa kweli jamani sisi *natural resources* tumeitunza mno sasa watu wakishamaliza yao tunakuja ku-*share equal.* Tuangalie sana kwa pamoja na kusema kwamba naunga hii itifaki kuna mambo mengi ambayo kwa kweli hasa hii ya kutumia miaka mitano tu kwamba watu wanafikiria tutakuwa sawasawa na Kenya ni kitu ambacho tuangalie sana. Tutakuta tuna matatizo makubwa zaidi. Ni kitu ambacho ni lazima tukiangalie kwa undani sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo mimi naunga mkono hoja hii na nafikiri Serikali itaangalia hayo tuliyosema. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kunipa nafasi hii pamoja na kwamba ulishasahau na mimi nilishavunjika moyo nilisharidhika kukaa kitako. Lakini ninakushukuru kwamba kwa kuniulizia na ni kweli niliomba kuchangia asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kunipatia nafasi hii na la pili naipongeza Serikali kwa kuleta Azimio hili muhimu kwa taifa letu na Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki na la tatu naiunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuchangia azimio hili. Nikiwa na sababu zangu ambazo utaziona nitakapo changia kwanza nataka niseme kwamba historia inatueleza kuwa nchi zetu hizi tatu zinahusiano wa asili na wakindugu kabisa. Kwa hiyo, Azimio hili ni imani yangu kuwa litadhihirisha hivyo. Kwa hiyo, ndio maana nikasimama kuliunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema historia inatudhihirishia kwamba sisi ni wamoja. Historia inatuambia kwamba mnamo Mwaka 1885 wazungu walikutana pale Berlin wakagawana Afrika na tukajikuta Kenya, Uganda na Zanzibar tuko chini ya utawala wa Uingereza na wenzetu waliokuwa Tanganyika walikuwa chini ya Ujerumani. Lakini baada ya vita vile vya Mwaka 1914 mpaka 1918 Waingereza na Wajerumani, Wajerumani walishindwa na Waingereza. Vile tu wenzetu waliokuwa Tanganyika ikawa wako chini ya Uingereza.

Kwa hiyo, ukiangalia hili soko letu sisi lilionyesha kuwa sote tulikuwa chini ya utawala mmoja wa Mwingereza. Kwa hiyo, Itifaki hii itaturudisha katika historia na pia itatuunganisha pamoja katika kuleta maendeleo ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo hizo ni sababu muhimu ambazo zimenipa nisimame hapa kuunga mkono Wizara hii na Serikali kwa jumla juu ya Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika azimio letu tunaomba nchi yetu ya Tanzania ni mwanachama wa jumuiya hii kwa mkataba uliotiwa saini tarehe 30 Novemba, 1999. Lakini kidogo nafanya hofu mimi na inawezekana Waziri wa Fedha hayajui haya nataka niulizie jumuiya yetu hii mpya sijui kama kuna Katiba yoyote ambayo inaisimamia au sheria zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hili kwa hofu kwa sababu tulikuwa na jumuiya huko nyuma. Lakini Mwaka 1977 ilivunjika na ilitokea tu pengine sababu za mtu mmoja tu aliamua vile akavunja jumuiya ile na akaingiza nchi katika migogoro mikubwa. Ambayo tunawafanyakazi mpaka leo waliokuwa wa jumuiya ya Afrika ya Afrika wanaidai Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mafao yao.

Kwa hivyo tuangalie jumuiya hii ambayo tumeiunda sasa je itakuwa iko Katiba ambayo inaisimamia au sheria zake ili atakapotokea mmoja kusababisha kuivunja aweze kushitakiwa. Hili kuiepusha nchi nyingine kuingia katika migogoro na wananchi wake. Kwa hivyo hili naamini pengine Waziri wa Fedha atakuwa halijuwi lakini ningetaka kwamba wale wahusika wakuu wakaliangalia wakaweza kulipatia nafasi husika ili kuona usahihi wa kuweza kuidumisha jumuiya yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Azimio hili tumeelezwa kwamba lengo la Itifaki hii ni kuimarisha biashara baina ya nchi wanachama kwa kuondoa vizuizi mbalimbali vya kodi na kuweka mazingira mazuri ya kuongeza uzalishaji kwa kuvutia uwekezaji kwenye maeneo ya Afrika Mashariki nataka nipongeze malengo haya ambayo Serikali na jumuiya yetu imekusudia.

Lakini je wafanyabiashara wetu sisi watajua vile vizuizi ambavyo vimeondolewa kwa hivyo hapa inastahili Serikali na viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwajulisha vyote vile ambavyo vinaonekana ni vizuizi ambavyo vitakuwa vimeondolewa ili wafanyabiashara wetu waweze kuvielewa. Ili kuweza kuwapatia mafanikio katika kuendesha uchumi na maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kuwa taarifa sahihi zitatolewa kwa wafanyabiashara wetu nchini na waliomo ndani ya jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikiri kuwa mipango na malengo ya Azimio hili ni mazuri sana na ninayaunga mkono asilimia mia kwa mia. Kwa hivyo ni jukumu la nchi zetu hizi tatu kuondoa tofauti zetu tulizonazo tuweze kujenga yale ambayo tumeyakusudia kwa faida ya taifa letu na Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. Tunaelezwa vilevile kwamba kuridhia Itifaki hii kutainufaisha Tanzania kwa kupanua wigo wa ushirikiano na nchi uanachama. Katika kuleta maendeleo ya wananchi wa Tanzania na Afrika ya Mashariki kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ni mazuri ni imani yangu kuwa manufaa hayo yatakayopanua wigo huo yatashirikisha pia na Zanzibar. Ni imani yangu kwamba yale maeneo ambayo yatapanua wigo huo yataishirikisha pia na Zanzibar. Ni mara nyingi Mheshimiwa Naibu Spika, tunajikuta Zanzibar tuko peke yetu hatuna uchumi na tunapitisha Miswada hapa na sheria kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini unakuta baadhi ya kazi unaambiwa hii inahusu Tanzania Bara tu, Zanzibar wanatusahau kwa hivyo ningaliomba azimio hili mtusaidie sana msije kuitenga Zanzibar ikakosa kufaidika na Azimio kama hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo nia yangu ni kuunga mkono Serikali ni kuunga mkono Wizara lakini katika jumuiya yetu tuangalie tutakuwa na Katiba ipi au sheria zipi za kuendesha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tusipange mipango baadaye ikaja ikakorogeka kwa upuuzi tu pengine wa mtu mmoja au wa nchi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono azimio hili kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuwashukuru wale wote waliochangia katika azimio hili likijumuisha Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha na Mheshimiwa Omar Mjaka. Kwamba awali ya yote napenda kuwahakikishia kwamba ushauri walioutoa wote utatiliwa maanani na utafanyiwa kazi.

Lakini la jumla ambalo lilijitokeza ni kwamba Tanzania tujikaze kama nilivyosema wakati nawasilisha Azimio hili tumesema kwamba kulikuwa kuna mi-order wa miaka mitano ili kuipa fursa Tanzania pamoja na Uganda kuweza kusafirisha vitu vyao kupeleka nchi nyingine, nchi ya Kenya bila ushuru yaani *zero rates* na hiyo imefanywa kwa makusudi nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mwandoro yale aliyoshauri kwamba tujitahidi kwamba tuwe na miundo mbinu ya kutosha hasa ya maji, umeme, barabara ambayo haya yote yako katika *seat* ya jumuiya Mashariki yanaangaliwa na kuna miradi maalum ya kuisha miundo mbinu hiyo.

Kwa hivyo jambo kubwa la kulifanya sisi watanzania ni kuhakikisha kwamba kweli tunawapa elimu wafanyabiashara wetu na kuanzi sasa tunajitahidi kwamba yale yote ambayo tunahisi ni tofauti na hayatupeleki mbele katika kuongeza kuuza biashara yetu nchi za nje tunayafanya hivi sasa ili tuendelee mbele wote takribani mliyoyatoa ni ushauri na sisi tunayatia maanani na tutaendelea kuyafanyia kazi.

Lakini Mheshimiwa Omar Mjaka, kuhusu suala la Katiba jumuiya ina-*treaty* yake imeelezea kwa urefu kabisa yale yaliyomo katika ile maafikiano baina ya nchi tatu hizi za Afrika Mashariki na kwa sasa hatuwezi tena kusubiri tena kama tunasema tangu tarehe 2 Machi, 2004 wakuu wa nchi hizi tatu wameshatia sahihi mkataba kwamba hii *this East African Customs Union i*anze kazi kuanzia tarehe mosi Januari Mwaka 2005.

Kuhusu suala la chai hivi sasa Wizara ya Ushirika na Masoko inawaelimisha wakulima juu ya ubora wa mazao yao. Chai itakayotoka Tanzania kwenda Kenya itakuwa zero rate, itakayotoka Uganda kwenda Kenya ina *zero rate* na hivi sasa Wizara hiyo imeomba fedha Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba wameshaanza majimbo ya kanda ya ziwa watakwenda mpaka Mbeya na sehemu nyingine vile kuwaelimisha wakulima na wafanyabiashara faida yao katika jumuiya hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mengi waliyotoa ni ushauri na tumeukubali na tutaufanyia kazi na tunashukuru wale wote ambao mmechangia katika hoja mbalimbali za azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*Azimio la Kuridhia Itifaki kuhusu Uanzishwaji wa Umoja wa Forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki liliridhiwa na Bunge*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

**Muswada wa Sheria ya Taratibu za kuwaenzi Waasisi wa Taifa wa Mwaka 2004**
***(The Founders of the Nation (Honouring Procedures) Bill, 2004***

*(Kusomwa Mara ya Pili).*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala chini ya Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, ilikutana tarehe 3 Novemba, 2004 na tarehe 7 Novemba, 2004 na kujadili na kupisha Muswada wa Sheria ya Kuwaenzi na Kutunza kumbukumbu za Waasisi wa Taifa letu, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, pamoja na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko na hadhima ya kuwa na Muswada huu ni kauli mbalimbali za viongozi wa Serikali na chama yaliyotokana na hisia za wananchi wengi asasi mbalimbali, mikutano na maandishi kadhaa ndani na nje ya nchi na mapendekezo ya wananchi kwa ujumla juu ya umuhimi wa kuwaenzi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, kutokana na michango yao mikubwa na ya kipekee waliyoitoa kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wakuwaenzi Waasisi wa Taifa letu umesisitizwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mfano halisi wa kuthibitisha hili ni pale Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, aliposema kwamba kuna umuhimu wa kutunza nyumba na eneo lote la makazi ya Baba wa Taifa na kutamka wazi katika hotuba yake ya tarehe 23 /10/1999 kwamba na naomba kunukuu, nanukuu na hasa kwa vile tumemzika Mwalimu hapa umuhimu wa nyumba hii kuwa historia ya Taifa ni kubwa mno eneo lote hili hapa pamoja na nyumba hii ni kielelezo na kumbukumbu ya milele ya maisha ya Mwalimu na Taifa letu. Hatuwezi kuiacha nyumba hii na eneo hili vihalibike kwa kukosa matunzo. Tutahakikisha tunaitunza ili daima iwe kioo halisi na cha kudumu cha hadhi ya Baba wa Taifa mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mifano mingine inayoonyesha kwamba Serikali ya Muungano na ile ya Mapinduzi zinatilia maanani na kutambua umuhimu wakuwaenzi Waasisi hawa ni kuhadhimishwa kwa tarehe 14 Oktoba, ya kila Mwaka kukumbuka siku aliyofariki Baba wa Taifa Mwalimu Juliusi Kambarage Nyerere na tarehe 7 Aprili, ya kila Mwaka

kukumbuka siku aliyouwawa Sheikh Abeid Amani Karume, kuwa siku za mapumziko na uanzishwaji wa makumbusho ya Mwalimu J. K. Nyerere, kule Butiama na makumbusho ya Sheikh Abeid Amani Karume kule Mwera.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na muongozo wa kutekeleza jambo hili, Serikali iliona ni busara kuwa na sheria inayoweka utaratibu wa namna ya kuwaenzi Waasisi kwani sheria zilizopo za mambo ya kale makumbusho ya Taifa na kumbukumbu na nyaraka za Taifa pamoja na taasisi ya Mwalimu Kambarage Nyerere aliyeiazisha akiwa hai hadhikidhi utekelezaji wa jambo hili kwa mapana yake. Kwa mfano taasisi ya Mwalimu Nyerere inajishughulisha na uendelezaji wa maswali ya amani na maendeleo na pia inahusika na Baba wa Taifa peke yake bila kumuhushisha hayati Sheikh Abeid Amani Karume. Ambaye naye alitoa mchango wa kipekee katika nchi hii kama Muaasisi wa Muungano. Kwa sababu hii Serikali ina wajibu wakuhakikisha kwamba Waasisi hao wote wawili wanaenziwa na Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutokea mwanzo kuwa tuna viongozi wengine nchini ambao wametoa michango muhimu katika historia ya nchi hii na inafaa pawepo utaratibu kwa kuwatambua na kuwaenzi. Serikali imekuwa ikipokea hoja za namna hiyo na napenda kuahidi kuwa Serikali itatafakari kwa makini hoja hizi na kuzitolea msimamo. Hata hivyo kwa kutambua michango ya kipekee ya Waasisi hao wawili kwa Taifa letu. Serikali imeona ni vyema tuanze na utaratibu wakuwaenzi hao wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulisomwa kwa mara ya kwanza Bungeni tarehe *6 August, 2004* na tangu wakati huo watu binafsi na wadau wengine wamepata nafasi ya kuusoma na kuchangia mawazo na maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti na Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa uvumilivu wao wa kuiongoza kamati hii. Naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa michango na maoni yao ambayo imesaidia kuuboresha Muswada huu ambao leo tunapata fursa ya kuujadili. Napenda kuwashukuru wazee wetu wa Chama cha Mapinduzi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano na ushauri wao walioutoa. *(Makofi)*

Shukrani zangu za dhati na za kipekee ziwafikie familia ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, ikiongozwa na wawakilishi wawili ya familia ambayo ni Mheshimiwa Rosemary Nyerere Mbunge wa Viti Maalum na Bwana Madaraka Nyerere ambaye yuko hapa kwa maelekezo ya Mama Maria Nyerere na warithi wengine pamoja na Familia ya Hayati Sheikh Abeid Amani Karume hususan Mama Fatuma Karume na Mheshimiwa Amani Abeid Karume Rais wa Zanzibar. Kwa michango yao ambayo imesaidia sana kuboresha Muswada na kwa kukubali kwao kuunga mkono hoja hii ya Serikali ya kuleta Muswada huu kwenye Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme wazi kwamba lengo la Muswada huu ni kuweka utaratibu wa kuratibu wa kuendesha kusimamia suala la kuwaenzi viongozi

wakuu Waasisi wa Taifa letu na kuhifadhi vielelezo vya kumbukumbu zao kwa manufaa ya Taifa na vizazi vijavyo heshima, utu, amani, utulivu, umoja, demokrasia na maendeleo ya mtanzania ni urithi na utajiri wa Taifa letu ambao umetokana na juhudi, mchango mkubwa na kujitoa mhanga kwa viongozi wetu hawa. Hivyo Serikali kwa niaba ya wananchi ina wajibu na dhamana ya kulinda urithi, heshima, busara na falsafa za viongozi hawa kwa kuwaenzi. Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na utamaduni huu kwa kuzingatia hali ya maisha ya Waasisi hawa ambao waliishi maisha ya kawaida kabisa na si ya kifahari na hawakujilimbikizia mali wao wenyewe au familia zao.

Ili kujenga misingi ya usawa katika jamii yetu. Aidha misingi hiyo inajitokeza katika vielelezo vya kumbukumbu zao za kimaandishi na vitu walivyokuwa navyo. Hivyo madhumuni ya kuwa Muswada huu ni kuhakikisha kuwa hazina waliyokuwa nayo viongozi hawa inaendelea kuhifadhiwa kwa ajili ya kizazi hadi kizazi na kwamba haipotei.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuandaa Muswada huu hatua mbalimbali zilichukuliwa Serikali iliitisha mikutano ya wadau ili kupata michango yao. Wadau walitokana na makundi yafuatayo.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Chama cha Mapinduzi, Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Asasi na Taasisi mbalimbali za Serikali, Bara na Visiwani zenye taalum au utaalam wa maeneo yao na watu binafsi waliopenda kujitokeza. Wadau kwa pamoja walishauri na kupendekeza pamoja na mambo mengine itungwe sheria inayoelekeza kuazisha kituo kitacho hifadhi vielelezo za kumbukumbu za Waasisi hawa ili vilindwa na kudumishwa. Mapendekezo haya yaliwasilishwa Serikali kwa maamuzi na hatimaye Serikali ilikubali mapendekezo ya kutungwa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato mzima wa kuandaa Muswada huu Ofisi ya Rais Memejiment ya Utumishi wa Umma pia ilipata uzoefu wa nchi za China, Marekani na Sweden. Uzoefu uliopatikana umedhihirisha kuwa mataifa mengi duniani ya utamaduni na utaratibu wa kisheria na wa kisera wakuenzi na kuhifadhi kumbukumbu za viongzi wao mashuhuri. Kwa mfano Vyama vya Siasa na vya hiari jumuiya na makundi mbalimbali ushiriki kwa kuanzisha shughuli za kuenzi na kutunza kumbukumbu.

1. Lakini kwa kuzingatia utaratibu wa sheria za msingi zilizowekwa katika jambo hili.

2. Familia ushiriki katika mambo haswa mawili, kwanza kuhakikisha kinachoenziwa na kuhifadhiwa kinazingatia usahihi hali halisi, hadhi ya Mwasisi mwenyewe na uongozi wake, hadhi ya familia na Taifa. Pili ushiriki kwa kuchangia gharama za kuanzishwa kwa wale wenye uwezo na kuendesha vituo kuhamasisha marafiki, ndugu, jamaa na wengine.

3. Uratibu hufanywa na mamlaka za Serikali lakini Serikali au Taasisi haihodhi jambo la kuenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu na maoni mbalimbali yalipatikana ambayo yanafaaa katika mazingira ya Taifa letu yamezingatiwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapa juu. Muswada huu ninao wasilisha ni matokeo ya kuunganisha maoni ya familia za Waasisi, jamii ya watanzania kwa ujumla, Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Taasisi ya Mwalimu Nyerere na Wazee wakongwe wa taifa letu ambao wote walitoa maoni kwa maandishi na kwa maelezo ya mdomo. Masuala yaliyojitokeza katika hatua mbalimbali za kujadili Muswada huu na wadau na ambayo yalionekana yanaendana na maudhui ya Muswada huu yamezingatiwa katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutungwa kwa sheria inayotokana na Muswada huu, dhima ya Serikali itakuwa kuratibu kusimamia kutoa utaalam na kuhamasisha shughuli za kuenzi kwa mashirikiano ili ziweze kuwepo na kurithishwa kizazi hadi kizazi. Dhima ya wadau itakuwa ni kushiriki kikamilifu katika utaratibu wa kuenzi kwa kuwekeza katika miundo mbinu inayostahiki kitaalum, kifedha, majengo, uanzishaji na uendeshaji vituo.

Hii ikiwa ni pamoja na kuchangia uhimilifu endelevu wa kazi ya kuenzi kwa kuzingatia utaratibu utakaowekwa na sheria hii au miongozo na kanuni zitakazo andaliwa kwa ajili ya utekelezaji. Kwa maelezo haya nia ya Serikali si kunyang'anya, kupora, kuhodhi au kufifisha vyombo vingine vilivyopo na vitakavyojitokeza katika suala zima la kuenzi na kuhifadhi kumbukumbu za Waasisi. Badala yake itapenda kushirikiana na taasisi na watu mbalimbali na itakapobidi na kwa kadri ya uwezo itavisaidia kama njia ya kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Muswada huu umegawanyika katika sehemu tisa na mpangilio wake umeainishwa mwishoni mwa Muswada katika sehemu ya madhumuni na sababu. Hata hivyo kwa maelezo mafupi Muswada umezingatia mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Kuanzishwa kituo cha kuhifadhi kumbukumbu za Waasisi wa Taifa;

(ii) Utaratibu wakuenzi na kutunza kumbukumbu za Waasisi kwa kushirikiana na wadau wakuu, taasisi na asasi zilizopo na zitakazojitokeza baadaye katika suala la kuenzi;

(iii) Fursa ya mashauriano na makubaliano kati ya Serikali na familia za Waasisi. Juu ya kumbukumbu za maandishi na vitu vinavyoainishwa kuwa urithi wa kihistoria na orodha yake kuhifadhiwa katika kituo;

(iv) Kuanzisha mfuko wa huhifadhi wa kumbukumbu ambao utachangiwa na Serikali, watu au taasisi binafsi za ndani na nje ya nchi;

(v) Kuwa na uratibu wa suala zima la kuenzi, kuhifadhi kumbukumbu za Waasisi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ukipitishwa utaleta matokeo yafuatayo:-

(i) Hazina waliyotuachia Waasisi hao itaendelea kuwepo bila kupotea.

(ii) Jamii ya Tanzania itaweza kurithishwa kizazi hadi kizazi. Hazina ya mambo ambayo Waasisi hao waliyaasisi na ambayo ndio guzo kubwa ya utajiri na heshima tuliyonayo watanzania.

(iii) Mawazo na falsafa zilizotawala maisha yao zitaendelea kuwa dira na kitovu cha utu, umoja, amani na utulivu, demokrasia na maendeleo ya watu.

(iv) Patakuwepo na ufanisi katika utekelezaji wa kazi ya kuenzi na katika kuhifadhi kumbukumbu zao.

(v) Taarifa mbalimbali zinazowahusu Waasisi hawa zitapatikana katika vituo vinavyojulikana na kwa urahisi zaidi.

(vi) Uthibiti na utaratibu madhubuti wa matumizi holela au ya kibiashara ya majina ya Waasisi.

(vii) Hati miliki na haki miliki za mali zao zitalindwa bila kuingilia uhuru wa familia za Waasisi juu ya mali hizo na hivyo sheria itakayotungwa itaweka misingi na fursa ya kufanya mashauriano hili kufikia makubaliano na wadau wakuu hususan familia, taasisi na asasi za juu. Asasi juu ya kumbukumbu na vitu vitakavyohainishwa kuwa uriti wa kihistoria ambavyo orodha yake itatuzwa katika kituo na hakuna kitakachochukuliwa bila ridhaa ya wahusika. Kutungwa kwa sheria hii kutajengea nchi yetu heshima kubwa na kuimarisha misingi ya utaifa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ninawashukuru na ninawaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (k.n.y. MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO-MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya taratibu za kuwaenzi Waasisi wa Taifa wa Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa niaba ya Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala napenda nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipatia fursa ya kuwasilisha Muswada wa Sheria ya taratibu za kuwaenzi Waasisi

wa Taifa wa Mwaka 2004, *The Founders of the Nation (Honouring Procedures) Bills, 2004.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu Muswada huu ulileta kwenye Kamati yangu pamoja na Miswada mingine ili ushughulikiwe wakati tukiwa Dar es Salaam katika wiki mbili zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za Kamati.

Hata hivyo kutokana na sababu zisizozuilika Muswada huu umejadiliwa hapa Dodoma ambapo Kamati yangu ilikutana tarehe 3 na tarehe 7 Novemba, 2004 ili kuweza kushughulikia na kuukamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vikao hivyo Kamati ilipata fursa ya kusikia maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Dr. Mary Nagu Mbunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma. Kuhusu adhima ya Serikali ya kuuleta Muswada kama alivyoeleza mtoa hoja hapo awali.

Aidha kwa mujibu wa kanuni ya Bunge Na. 69(2) na Na. 88 (6). Kamati ilipata fursa pia ya kusikiliza maoni ya mdau na mwakilishi wa familia ya Baba wa Taifa hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Rosemary Nyerere - Mbunge, katika kikao cha Kamati cha tarehe 3 Novemba, 2004. Ambaye pia alishirikiana na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere - Mbunge na Madaraka Nyerere, katika kikao cha pili cha Kamati hiyo.

Pia Kamati ilipokea taarifa kwa muktasali ya namna familia ya Mwasisi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hayati Sheikh Abeid Amani Karume, livyoshirikishwa kikamilifu katika ngazi ya familia na kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni pamoja Serikali ilivyoihusisha familia ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikiri kuwa katika kikao cha kwanza cha Kamati, baada ya kusikiliza maelezo ya Serikali na maoni ya mdau Kamati iliona kuna busara kuhairisha kikao chake na kuiagiza Serikali iwasiliane tena na wadau hususan familia hizo mbili yaani familia ya Hayati Mwl. Julius K. Nyerere na familia ya Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, ili kuondoa wasiwasi ulijitokeza katika Kamati katika maeneo kadhaa yaliyohusu mswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi ya pekee kuipongeza Serikali na hususan Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Management ya Utumishi wa Umma, kwa kutekeleza maagizo ya Kamati kikamilifu na haraka na kuondoa utata mkubwa uliojitokeza katika kikao chetu cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kamati yangu ilikuwa na vikao viwili kujadili mswada huo katika tarehe nilizozitaja hapo awali. Hivyo basi, kamati yangu ilipokutana katika kikao chake cha pili cha tarehe 7 Novemba kwa ujumla Kamati pamoja na familia ya Mheshimiwa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere ilikubaliana na kazi nzuri iliyofanywa, na marekebisho ya Serikali kama ilivyoainishwa katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa mbele ya kamati na lililopo mbele ya Bunge lako Tukufu sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa faida ya Bunge lako Tukufu, maeneo ambayo Kamati yangu ilitaka ufafanuzi wa kina na kuishauri Serikali kwa kina ni kama ifuatavyo:-

1. Mheshimiwa Naibu Spika, kuweko kwa neno *Revolutional Government of Zanzibar* badala ya *Government of Zanzibar* kama ilivyokuwa katika sehemu ya tafsiri ya mswada.

2. Kutoa tafsiri ya neno *Committee* katika sehemu hiyo hiyo iliyojionyesha hapo mwanzo.

3. Uteuzi wa Mkurugenzi wa kumbukumbu ya Hifadhi za Nyaraka kuwa Mkuu wa Kituo cha Waasisi wa Taifa. Kamati ilishauri kuwa, kwa kuwa Mkurugenzi huyo tayari ana majukumu mengine ingefaa kazi hii apewe mtu mwingine. Hata hivyo Serikali ilifafanua kuwa kazi yake itakuwa ni uratibu tu, na kwamba kutakuwa na kiongozi mahususi wa kituo hicho.

4. Katika Ibara ya 11(4) ya Muswada inayohusu pingamizi linaloweza kuwekwa dhidi ya uwezo Waziri kuharibu nyaraka, mali na kadhalika za Waasisi. Kamati iliona kuwa Ibara hii bado inampa madaraka makubwa sana Waziri kukataa pingamizi na kuendelea na uamuzi wake. Hivyo basi Kamati ilishauri kuwa madaraka hayo yaangaliwe upya na hasa masilahi yanayogusa familia za waasisi moja kwa moja, na pia Kamati ilishauri kuwa pingamizi hilo liendelee hadi hapo Rais atakapotoa uamuzi wake.

5. Katika kurasa za 13 na 14 za Muswada Kamati iliona kuwa kazi zilizopangwa kufanywa na Kamati ni chache, na kwa kuzingatia kuwa kutakuwepo na Bodi, Kamati inashauri kuwa kazi za Kamati zifanywe na Bodi.

6. Katika Ibara ya 23 ya Muswada Kamati inashauri kuwa, ada ziondolewe kwa Watanzania wanaotaka kuingia kwenye Makumbusho ya Waasisi wa Taifa kwa ajili ya kuona kumbukumbu, ili kuwawezesha Watanzania wengi kupata nafasi ya kuingia katika maeneo hayo na kujionea kumbukumbu mbalimbali za Waasisi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni baadhi ya maeneo ambayo Kamati yangu iliishauri Serikali iangalie kikamilifu na kuyafanyia kazi. Kwa bahati nzuri kama nilivyosema tangu mwanzo karibu maeneo mengi yamefanyiwa kazi na kuboreshwa na kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho ambalo liko mbele ya Bunge lako Tukufu kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba nimalizie yale maeneo ya jumla ambayo Kamati yangu imesisitiza na kuishauri Serikali.

1. Pamoja na marekebisho yaliyofanyika, Kamati bado inasisitiza kuwa Sheria inayokusudiwa itofautishe kati ya vitu binafsi vya Waasisi wa Taifa na vya Umma, ili

pasije kutokea usumbufu wa Kisheria wa warithi au familia zao au jamii nzima kwa ujumla.

2. Madaraka ya kuharibu mali au vitu vya Waasisi yaliyoelezwa katika Muswada huu yafanywe kwa kuwasiliana na familia za Waasisi hao kwanza, au baada ya kupata ridhaa za warithi au familia zinazohusika.

3. Kamati inashauri kuwa katika siku zijazo Serikali iangalie pia kuweka utaratibu wa Kisheria, wa kuwaenzi au kuweka kumbukumbu za watu mbalimbali waliotoa mchango makubwa katika Taifa hili kama vile; Mashujaa waliopigana vita dhidi ya Wakoloni na viongozi wa Kitaifa ambao wametoa mchango mkubwa sana kwa Taifa letu.

Aidha Kamati yangu inaridhika na kuliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Muswada huu kutokana na mchango mkubwa sana, na wa kipekee waliotoa Waasisi wetu wa Kitaifa katika medani za Kitaifa na Kimataifa. Muswada huu ni njia mojawapo ya kuwaenzi katika uga wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndio maeneo ya jumla ambayo Kamati yangu ilishauri. Yale ambayo yataendelea kugusiwa na Waheshimiwa Wabunge yataendelea kuboresha maeneo mbalimbali ili Muswada huu uweze kuwa fasaha na kuweza kutumika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda nikushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii muhimu ambayo naamini ni nafasi pekee kwangu, na kwa Kamati yangu kuwaenzi Waasisi wetu wa Taifa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Aidha napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana na kwa dhati, Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Management ya Utumishi wa Umma. Vile vile Katibu Mkuu wa Wizara Bwana Joseph Ruguyamheto na wataalam wote kwa kushirikiana vema na Kamati katika kutekeleza ipasavyo maagizo yote ya Kamati kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha wizara kuwasikiliza wadau katika ngazi ya Wizara na Kamati ya Bunge, kinaonyesha jinsi gani Serikali na Bunge linavyowashirisha Wananchi kwa karibu zaidi katika mchakato mzima wa kutunga Sheria. Ninaomba kwa nafasi nyingine nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu Mheshimiwa Andrew J. Chenge Mbunge, kwa mchango wake mkubwa na kwa kazi yake nzuri sana aliyoifanya mbele ya Kamati hii na hadi kufikisha Muswada huu hapa ulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwashukuru wawakilishi na wadau na hasa kutoka katika familia ya Mheshimiwa Hayati Mwwalim Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, kwa kuukubali Muswada huu na kutoa michango yao ya kina iliyosaidia sana katika Kamati kuboresha Muswada wenyewe. *(Makofi)*

Shukrani za pekee ziwafikie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri walioifanya ya kutumia kila aina ya hekima na busara, na hatimaye kuufanya Muswada uonekane katika sura inayoonekana ndani ya Bunge lako Tukufu. Kuwepo kwa jedwali la marekebisho ni ushahidi tosha wa kazi nzuri iliyofanywa na Wajumbe hao na ninapenda Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwataja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Athumani S.M. Janguo, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru Mbunge, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mjumbe, Mheshimiwa Rosemary K. Nyerere Mjumbe, Mheshimiwa Zahor J. Khamis - Mjumbe, Mheshimiwa Khamis Salum Ali - Mjumbe, Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan - Mjumbe, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga - Mjumbe, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri - Mjumbe, Mheshimiwa Pascal C. Degera - Mjumbe, Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte - Mjumbe, Mheshimiwa Chief Abdallah Fundikira- Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa - Mjumbe, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama - Mjumbe, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba - Mjumbe, Mheshimiwa George F. Mlawa - Mjumbe, Mheshimiwa Raynald A. Mrope Mjumbe, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma Mjumbe, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe Mjumbe, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Masumbuko R.M. Lamwai - Mjumbe, Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare - Mjumbe, Ndg. Hernest Zulu Katibu na Ndugu Charles Mloka - Katibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote naomba nichukue nafasi ya pekee kwa niaba ya Wanakamati na Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kuunga Muswada huu na kuomba kuuwasilisha rasmi mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS UTUMISHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Muswada wa Kuwaenzi Waasisi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya kambi ya upinzani Bungeni napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kutoa maoni ya kambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote Kambi ya Upinzani inampa pongezi Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Muswada huu Bungeni ili uweze kupata baraka zetu. Muswada huu ni utekelezaji wa juhudi zetu za kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu, kwa michango yao mikubwa ambayo imetuwezesha sisi kuwa katika hatua hii ya maendeleo, amani na utulivu wa Taifa letu. *(Makofi)*

Muswada huu pia utaunda chombo kitakachosimamia na kuratibu shughuli zote za utunzaji na uendelezaji wa kumbukumbu za Waasisi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi kubwa na nia njema inayofanywa na Serikali ya kuwaenzi Waasisi hawa, Muswada huu una mapungufu mengi sana ambayo yanahitaji kurekebishwa ili maana na lengo la kuwaenzi Waasisi hawa litimie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada haujali maslahi ya warithi wa Kisheria Waasisi waliokusudiwa na Muswada huu. Kwani umekusudia kuchukua kazi za maandishi na vitu walivyokuwa wanavitumia Waasisi ambavyo vinaonekana vina maslahi ya Kitaifa kama inavyoainishwa kwenye Ibara ya 11(1) ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna tatizo kubwa sana wakati Sheria hii itakapoanza kutumika, kwani Muswada hautoi tafsiri ya maslahi ya Kitaifa. Serikali inaweza kutumia mwanya huu wa msamiati wa maslahi ya Kitaifa hata kama kazi au vitu vya Waasisi hawa vilikuwa vyao binafsi. Muswada huu umelenga kuwafirisi warithi Waasisi na kuwaacha wakiwa maskini bila ya mtu yeyote kuwajali. Hii haina tofauti na matukio yanayofanyika kwenye familia ya wajane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri Muswada huu uorodheshe vitu vyote ambavyo vinataraji kuvichukua kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na sio kusingizia maslahi ya Kitaifa, na kama itaona mali au kitu cha Waasisi ni cha binafsi na Serikali inapenda kukichukua na kukihifadhi, basi wakubaliane na familia za Waasisi kwa malipo kabla ya kuchukua. Kama Serikali itaamua kuchukua nyumba basi iwajengee nyumba kabla ya kuchukua hizo dhamani. Serikali imekuwa na tabia ya kusema vifaa au nyumba za Waasisi zitahifadhiwa kwa ajili ya kumbukumbu za Kitaifa, lakini hatma ya azma hiyo haitekelezwi. Hebu tuulize jumba la mamilioni ya fedha lililotumika kuhifadhi mwili wa Marehemu Mwl. Julius K. Nyerere Uwanja wa Taifa liko wapi sasa? Au limetelekezwa kama thamani mbovu. Kama Serikali imeshindwa kulitunza jumba hilo litaweza kutunza mali za maandishi ya Waasisi hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sheria hii kwa upande wa Zanzibar itakuwa na ugumu kwani Zanzibar wana Sheria ya kuwaenzi Waasisi na viongozi wa juu wa Kitaifa. Kama inavyotajwa na Ibara ya 28 ya Muswada huu na sio kikundi cha Waasisi wachache kama inavyopendekezwa kwenye Sheria hii. Muswada huu unaitambua Sheria hiyo je, ni vipi Serikali itaweza kuratibu kumbukumbu za Waasisi toka Tanzania Visiwani wakati wanayo Sheria yao, na kama kutatokea tofauti ya Kisheria nani ataamua Sheria ipi ifuatwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutakuwa na mgongana wa kiutendaji na taasisi ambazo sio za Kiserikali, zinazohifadhi kumbukumbu za Waasisi hawa ambazo zinatambuliwa na Sheria hii. Kama vile taasisi ya Mwl. Julius K. Nyerere kama tujuavyo wote kuwa taasisi hii iliundwa na Baba wa Taifa Marehemu Mwl. Nyerere kuna nyaraka nyingi ambazo aliziandika baada ya kustaafu Rais na alizikabidhi kwenye taasisi hiyo kabla hajaaga Dunia. Je, itakuwaje kama Serikali itasema nyaraka hizo zinamaslahi ya Kitaifa wakati Mwl. Julius K. Nyerere aliziandika baada ya kustaafu Urais na alizikabidhi kwenye taasisi hiyo? Hivi baada ya Muswada huu kupitishwa taasisi ya Mwl. Julius K. Nyerere itakuwa na ubavu gani wa kuendelea kuhifadhi nyaraka za Mwl. Julius K. Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unawapendelea Waasisi wa chache na kuwaacha wengine. Kuna Waasisi wengi tu ambao waliojitoa muhanga kupigania Uhuru wa Nchi hii. Lakini Muswada huu umejaribu kuainisha Waasisi wawili tu ambao walikuwa Marais.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasababisha utungaji mwingine wa Sheria ambao utaongeza gharama zisizo za lazima kwa Serikali bila sababu zozote. Tunafikiri si vyema kuwa tunatunga Sheria kwa malengo ya kumkusudia mtu maalum, ni vyema tukatunga Sheria zenye kukidhi mahitaji na matumizi ya watu wengi. Maudhui ndani ya Muswada au Sheria ndio yawe bayana nani anastahili au nani mwenye kukidhi sifa za kuitwa Muasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nabu Spika, kambi ya upinzani inashauri kuwa, ni vizuri Sheria hii ingewajumuisha Waasisi wote bila kubagua kwa kubainisha sifa. La sivyo Sheria hii iitwe ya Wababa wa Taifa na siyo Waasisi wa Taifa. Historia ya Tanzani haikuanza na Mwalimu Julius K. Nyerere tu, wapo Waasisi wengi ambao walianzisha *TANU* na Ma-*chief* waliojitolea kwa hali na mali kutetea Uhuru wetu kama vile Oscar Kambona, Dosa Aziz, Patrick Kiumbika, Chief Patrick Kunambi, Abdallah Fundikira ambaye alikuwa Waziri wa kwanza wa Sheria na kadhalika. *(Makofi)*

Ni kweli kwamba Mwalimu Julius K. Nyerere alifanya mambo mengi sana lakini asingeweza kufanikiwa bila kupata ushirikiano kutoka kwa Waasisi wengine. Ni vyema Sheria hii ikawatambua Waasisi wengine hata kwa kuwataja tu katika Sheria hiyo kama Sheria ya Zanzibar inavyowatambua Waasisi na viongozi wa juu wa Taifa.

Pia Kambi ya Upinzani inaonya kuwa CCM isitumie mwanya huu wa kuwaenzi Waasisi wa Taifa kwa ajili ya maslahi ya chama na siyo ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha na naunga mkona hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge muda uliobaki hautoshi kwa kumpa mtu kuweza kuchangi, hasa kutokana na uzito wa Muswada huu, inabidi watu watafakari vizuri, kwa hiyo kufika hapo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3 asubuhi.

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

(*Saa 11.48 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano Tarehe 10 Novemba, 2004 saa Tatu Asubuhi)*